ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake

38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
51.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
52.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
53.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
54.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
55.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
56.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Jimbo la Mpendae
57.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
59. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini

60.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
61.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
62.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
63.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
64.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Rashid Seif Suleiman	Jimbo la Ziwani
66.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
69.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
70.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
71.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
75.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Jimbo la Dole
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka 2012/2013. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Panya Ali Abdalla (Mhe. Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka 2012/2013. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 – Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati

(Majadiliano Yanaendelea)

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla ya kuendelea na mjadala, nashukuru kuchukua nafasi hii kwa kuwashukuru wananchi wote kwa ujumla, kwamba kumbe wananchi wanafuatilia sana shughuli zetu hapa, ili kuona na kujua nini tunafanya kwa ajili yao.

Kwa hiyo, na leo tumepata wageni ambao ni vijana wetu wanafunzi kutoka Skuli ya *Trifonia Academy*, ambayo iko Meli Tano Fuoni na wamekuja jumla ya wanafunzi 70 pamoja na walimu wao 6. Kwa hivyo, nawaomba walimu pamoja na wanafunzi wao wasimame kwa ajili ya kuwasalimia Waheshimiwa Wajumbe. Ndugu walimu pamoja na wanafunzi karibuni sana, ili kuona

shughuli zetu zinavyoendelea na ninawashukuru sana. Waheshimiwa Wajumbe, nawashukuru sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, kwa mujibu wa ratiba yetu shughuli yetu ya leo hii inayoendelea kuanzia jana nategemea tufanye majumuisho leo jioni. Kwa hivyo, niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe mukisaidie kiti, ili tupange *points* zetu vizuri twende kwenye hoja ilioko mezani, tutoe mjadala kwa ajili ya kumsaidia Mhe. Waziri kufafanua, ili hatimae jioni tumudu kumwita Mhe. Waziri kwa ajili ya kufanya majumuisho.

Waheshimiwa Wajumbe, nakushukuruni na majadiliano yanaendelea. Kwa maana hiyo, basi nitangulie kumkaribisha Mhe. Mohammed Haji Khalid na atafuata baada ya hapo Mhe. Nassor Salim Ali.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mhe. Spika, ahsante sana kwa asubuhi hii kunipatia nafasi ya kuwa kiranja kwa kuendeleza majadiliano yetu ya wizara hii ambayo tulianza kujadili tokea jana.

Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuamsha salama tukiwa wazima na kufika hapa kwa ajili ya kuendelea na shughuli zetu.

Mhe. Spika, mimi nataka niende moja kwa moja katika kujadili bajeti hii. Lakini kwanza naomba nimwambie mwanafunzi mwenzangu wa wizara hii, kwamba amepewa wizara, ambayo inabeba maisha ya wanadamu, kwa sababu ndani yake mna kitu maji, ambacho ni chanzo cha uhai na kwa kidunia mna kitu umeme, ambapo kwa dunia ya leo ukikosekana umeme shughuli zote zinakwama. Kwa mfano, hospitali hakuna tiba, majumbani hakuna huduma yoyote, kwa hiyo amepewa wizara ambayo imebeba dhamana ya maisha ya wazanzibari. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, ajue kuwa analo jukumu kubwa kwa wazanzibari na ajitahidi kadri iwezekanavyo aweze kufikia malengo, ili wazanzibari wawe salama katika maisha yao. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nianze moja kwa moja kwenye Mahakama ya Ardhi. Kwa kweli ardhi ni rasilimali kubwa ya wazanzibari na ardhi imebahatika kuwa ni moja katika kero kubwa ndani ya visiwa vyetu.

Mhe. Spika, naomba nikwambie tumepata bahati mbaya wazanzibari, maana yake tuna kero nyingi, tukiondoa zile za Muungano, basi ndani ya serikali yetu pia tuna kero, kwa sababu ardhi, maji, umeme na hata elimu hivi sasa ni kero, kwa hiyo tumezungukwa na kero. Kwa hivyo, ni wajibu wa serikali

kujitahidi kadri ya iwezekanavyo kuweza kuzikabili na kuzipatia ufumbuzi kero hizi zilizotukabili wazanzibari. *(Makofi)*

Sasa nije kama nilivyosema kwenye Mahakama ya Ardhi, ambayo nimeona sehemu ndogo tu kuhusu kesi ambazo zilizofunguliwa hadi mwezi wa Machi mwaka huu 2012. Mhe. Spika, inaonekana kesi za Ardhi zilizofunguliwa ni 188, kwa upande wa Unguja zimefunguliwa kesi 101 na kwa upande wa Pemba zimefunguliwa kesi 87. Kati ya kesi hizi zilizofunguliwa hadi Machi mwaka huu kesi 95 zimefikishwa Mahakamani na kwa upande wa Unguja ikiwa ni 15 na Pemba 80.

Mhe. Spika, katika kesi 95 kwa upande wa Unguja ni kesi 15 tu zilizopatiwa ufumbuzi au zilizohukumiwa na Pemba ikawa 80. Kwa hivyo, tujaalie hawa Mahakimu wa Mahakama ya Ardhi huku Pemba wameripua tu hata wakaweza kumaliza kesi 80, na kwa upande wa Unguja ambako kuna kesi nyingi wakaweza kumaliza kesi 15 tu.

Kwa kweli sijui hii Mahakama inakwenda vipi? Hawa wakawa wamefanya kesi nyingi zaidi kuliko upande mwengine, je hawa wameripua au wanafanya kazi zaidi kuliko upande wa pili, kwa sababu ni jambo ambalo kwa tabia zetu ni kama kinyume nyume, kwamba Pemba kutokee jambo kubwa zaidi kuliko Unguja.

Kutokana na hali hiyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja hapa kufanya majumuisho anieleze huu utendaji wa Mahakimu wa Ardhi wanaofanya kazi kwa pande zote mbili, yaani Unguja na Pemba. Tukitilia maanani kuwa ardhi ina migogoro mingi na inahitaji kupatiwa ufumbuzi, ili kuondoa matatizo yanayotukabili.

Mhe. Spika, Mahakama hii pia inahusika na kutoa Hati Miliki za muda mfupi na mrefu pamoja na Hati Miliki mpya. Hivi sasa kuna maeneo kadhaa ambayo yanadai Hati Miliki na bado hati hiyo haijapatikana, na kusababisha migogoro baina ya watu kwa watu au taasisi na watu ama baina ya taasisi moja na nyengine.

Kwa hivyo, ninaiomba wizara hii ifanye kila linalowezekana kujaribu kupunguza au kuondosha kabisa migogoro hii, kwa kutoa zile Hati Miliki katika zile sehemu ambazo zinahitaji kupatiwa Hati Miliki hiyo.

Nikiendelea na mchango wangu sasa niende kwenye Mamlaka ya Maji. Mhe. Spika, mamlaka hii ni muhimu sana kama nilivyosema mwanzo, kwa sababu maji ni uhai na siku moja nilisema wakati nilipokuwa nikisoma tulifanyiwa *Composition* kwa Kiswahili inayoitwa Insha inayohusu maji na umuhimu

wake. Sasa kwenye *conclusion* ya *composition* hiyo sijasahau jambo ambalo nilisoma kiasi miaka 45 iliyopita na nilisema hivi "*It is only those who lives in desert areas that know the value of water at it's worst"*.

Lakini leo imebadilika, kwa sababu tunajua umuhimu halisi wa maji ni sisi watu tunaoishi Zanzibar, kwani hakuna kipembe hata kimoja cha Zanzibar ambacho kinapata maji kwa uhakika, yaani vile kupata maji katika visiwa vyetu ndio bahati mbaya.

Kwa kweli leo tumefika pahala kwamba maji ikiwa yanatoka basi hiyo ni bahati mbaya, lakini bahati nzuri ya visiwa hivi ni kukosa maji na vile kupatikana ndio mbaya, ilivyo kinyume chake, kukosa iwe ni bahati mbaya na kupata iwe bahati nzuri, lakini kwa sababu wakati mwingi maji hapana, kwa hiyo kuona vile kuona pahala maji yapo hiyo huwa ni bahati mbaya.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba mbaya iwe mbaya na nzuri iwe nzuri na kukosekana iwe ni kwa bahati tu, lakini mara zote iwe maji yanapatikana kwa sababu ni chanzo cha maisha na yanahitajika wakati wote na wala si kwa zamu, kwani maji hayana zamu isipokuwa tunajifanyia tu wenyewe tunavyotaka.

Lakini mwanadamu wakati wote anahitaji apate maji safi na salama, kwa ajili ya matumizi yake yote, kama vile majumbani, mashambani na sehemu nyengine, sasa tukisema maji tunatoa kwa mgao hapa bado kuna kasoro.

Mhe. Spika, tukijaaliwa Ijumaa ya leo hadi Ijumaa ijayo huenda ikawa ni Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, kwa sababu leo kwa hesabu ninayofuata mimi ni mwezi 23, kwa hiyo Ijumaa inayokuja ni mwezi Mosi au Thalathini. Kwa kweli mwezi huu unapoingia Mamlaka ya Maji inazidi ukorofi kugawa maji, badala ya kuwasaidia wazanzibari kupumua kidogo kwenye kero ya maji, wao wanazidisha kero ya maji hasa sisi tunaoishi vijijini.

Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho, atueleze kwamba ione umuhimu wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, na kuwapunguzia wazanzibari kero hii. Nadhani wao hawaoni kuwa ni kero kwani inawezekana katika maeneo wanayoishi wenyewe kuna mtiririko mzuri wa maji, lakini kama wangelikuwa wanaishi ninakoishi mimi, basi wangeliona jinsi watu wanavyoteseka kwa kutafuta maji katika Mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani wakati ambao mabomba ya maji yapo lakini hamna maji. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hili ni tatizo tena kubwa na mara nyengine inakuwa kwa makusudi *created*, kwa sababu wakitaka katika eneo langu maji yanapatikana, lakini wakiamua wasitoe hawatoi. (*Makofi*)

Sasa naomba nizungumzie kuhusu habari ya maji katika Jimbo langu la Mtambile. Mhe. Spika, Mtambile yenyewe, Kangani na Kengeja, naomba nianze nyumbani Kengeja. Kwa kweli Kengeja kuna tatizo kubwa la maji kuliko hata Kangani na Mtambile, kwa sababu wanacho kisima kimoja, ambacho maji yake ni machafu na kwa lugha ya kishamba na wala sina hakika na ushamba huo na hapa upo haya maji tunasema yana chunyu, maana yake rangi yake ni kama yaliyotiwa mafuta vile. Kwa hivyo, kisima hichi kwa ufupi hakifai na hata kama ingekuwa inafaa basi maji yake hayatoshi. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, naiomba wizara hii katika mwaka huu wa fedha na Mhe. Spika mimi si mpigaji wa buti na wala sitopiga buti, kwa sababu kwa mimi nahisi ni kama ninayetwanga maji kwenye kinu, kwani maji ni laini na hata ukiyatwanga hayalainiki, isipokuwa ulaini wake ndio ule ule.

Mhe. Spika, naiomba wizara hii ipange na ipangue au ifanye vyovyote vile, lakini ihakikishe kuwa Kengeja tunapata kisima cha maji ya uhakika.

Mhe. Spika, kijiji ninachoishi mimi kinapata maji ambayo yanatoka Kengeja kwenda Kiwani, na visima hivi vilichimbwa *special* kwa ajili ya Kiwani, lakini maji yake yanapita katika sehemu yangu mimi na ndio maji ambayo tunayotumia.

Kwa kweli siku za mwanzo tulikuwa tunapata maji kwa wingi sana, lakini baadaye hapo katikati maji haya yalibadilishwa mwendo wake na kupelekwa upande wa pili kuna kijiji kinaitwa Mwambe, ambapo wao wanacho kisima chao cha maji nacho pia kiko Kengeja, sasa kisima hichi kinatoa maji kutoka Kengeja kupeleka Mwambe, na visima vyengine vinatoa maji kutoka Kengeja na kupeleka Kiwani, na hivyo vya Kiwani ndivyo ninavyotumia mimi. Sasa hapa katikati watu wa Mwambe walituteka nyara, maji ambayo yanayokwenda Kiwani yaligaiwa kuelekea Mwambe, wakati Mwambe wanacho kisima chao.

Kwa hivyo, Mamlaka hii ya Maji ikawafanya watu wa Mwambe kuwa ni wananchi daraja la kwanza na sisi upande wetu ni daraja la pili, na ikawa sisi maji tunapata kwa nadra au mara nyengine hatupati kabisa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nilipowafuata watu wa Mamlaka ya Maji wa ngazi zote za Pemba na matokeo yake, kila ninapowafuata ndipo ugumu unapozidi, maana

yake labda wanataka wasiambiwe kitu, kila unapokwenda kulalamika siku ya pili hali inakuwa ngumu zaidi. Kwa kweli hivi ndivyo hali ya Mamlaka ya Maji inavyofanyakazi Pemba.

Kwa hivyo, naiomba wizara hii kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba wizara hii ibadilike, kwa sababu wanadai kuwa hawapati malipo, hivi watu watalipa vipi kitu ambacho hawapati kutumia, kwani watu hawawezi kulipia maji wakati ambapo maji yewenye hawayapati. Mhe. Spika, naomba marekebisho ya hali ya juu yafanyike kuhusu suala hili.

Vile vile naomba nizungumzie kidogo kuhusu Idara ya Nishati na Madini. Mhe. Spika, kwenye idara hii kuna suala moja la mafuta ambalo ni moja miongoni mwa kero tulizonazo za Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Baraza lililopita kabla ya hili lililoendelea leo lilifanya mabadiliko makubwa ya kihistoria kuifanya Zanzibar kuwa ni nchi. Kwa kweli hapo tunalipongeza Baraza hili, na tunawapongeza zaidi wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyengine hadi kufikia hatua hiyo. *(Makofi)*

Jambo linalonisikitisha mimi kuwa watendaji nakusudia serikali inahofu kuchukua nafasi yake kama Zanzibar, Serikali ya Mapinduzi inaogopa, inahofu kuwatumikia wazanzibari kuhusu suala hili muhimu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, inaonekana mafuta Zanzibar yapo na maamuzi mengi yameshapitiwa, lakini serikali inahofu tena kubwa sana, nadhani hata ile kuchukia hawachukii, maana yake hii ni haki yetu kuidai, kwa sababu kuna njia tatu, lakini hata ile ya udhaifu kwamba tunanyimwa haki yetu, basi hata hii ya kuchukia serikali haichukii, hivi serikali inatupeleka wapi? Tumeamua nini na tunafanya nini? Kwa hivyo, ningeomba kile kinachoamuliwa kwa maslahi ya wazanzibari kitekelezwe. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi si mpigaji buti, lakini namuomba Mhe. Waziri atoe kauli ya kuturidhisha wazanzibari, na wala sio ya kutupiga changa la macho, lini shughuli hii ya mafuta itafanywa Zanzibar kwa maslahi ya wazanzibari na tuondokane na kuchanga shilingi moja moja kwa ajili ya maendeleo ya visiwa vyetu. Kwa kweli uchumi upo tunaogopa kuufanyia kazi, na hatimae tunaendelea kuwakamua na baada ya kutoka maziwa watatoka damu na mwisho tutawaua. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hili si jambo la mzaha ni jambo la nchi, ambalo ni la maslahi ya wazanzibari, hivyo ni vyema serikali iwaonee huruma raia wake, yaani uwahurumie na kuwatumikia vilivyo.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, unazo dakika 4 kwa ajili ya kumaliza hotuba.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mhe. Spika, naomba nigusie kidogo kuhusu Shirika la Umeme. Kwa kweli shirika hili nalo linahitaji kufanyiwa marekebisho makubwa katika utumishi wake, kwa sababu hili ni shirika la huduma na biashara na zaidi ni biashara kuliko huduma.

Lakini mteja wa Pemba na wala sina hakika wa hapa Unguja, kwa sababu mimi si mkaazi wa Unguja, anaweza kutaka huduma hii ya umeme nitumie Kipemba akatimbwa kweli kweli, pamoja na kwamba biashara ambayo inatia tija, kwa kweli hayo mateso yake unayoyapata hayasemeki, yaani nenda rudi nyingi, kwa nini na hii ni huduma na upande mwengine ni biashara. Mhe. Spika, shirika linahitaji kufanyiwa marekebisho ya hali ya juu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nimalize kwa kumpongeza Mhe. Asha Bakari Makame kwa maelezo yake mazuri aliyoyatoa jana kwa Rais Mstaafu Mhe. Dkt. Salmin Amour Juma, alimwambia kuwa kazi ambazo anazo Mhe. Asha Bakari Makame, wanaume 50 hawaziwezi. Mhe. Spika, ni kweli kabisa Mhe. Asha Bakari Makame namjua tumesoma pamoja ni mtu hodari sana, mambo yake kama alivyosema Mhe. Rais watu 50 hawayawezi wanaume tena sio wanawake, kwa sababu alikuwa ni mwanafunzi mwenzangu na hatimae alikuwa waziri wangu, kwa hiyo utendaji wake naujua vizuri. Mhe. Spika, ahsante sana. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, ahsante sana. Sasa naomba nimkaribishe Mhe. Nassor Salim Ali na baadae Mhe. Mohammed Mbwana Hamad.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi hii ya kuchangia Hotuba ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Kwanza nichukue fursa hii kumshukuru Mhe. Rais wetu mpendwa Dkt. Ali Mohammed Shein, kwa kufikiria na maamuzi yake mazuri ya kumteua waziri wetu kushika jukumu hili ya kuiongoza wizara hii.

Mhe. Spika, mimi nasema maamuzi sahihi aliyoyafanya Mhe. Rais kwa kuweza kumpa jukumu hili Mhe. Waziri. Kwa kweli Mhe. Waziri sote tunamfahamu na kumuelewa ni mtendaji, muadilifu, yaani ni mtu ambaye ni msikivu. Kwa hivyo, Mhe. Spika ni wajibu wetu kusema ukweli na pale ambapo pana matatizo ni wajibu wetu sisi kusema. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwanza nianze na kumuunga mkono Mhe. Mbarouk Wadi Mussa, wakati jana alipokuwa akichangia hapa alizungumza tatizo sugu ambalo linaikabili Wizara hii ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Mhe. Spika, mimi nadhani kuna donda ndugu na tutakuwa tunamchinjia mbuzi wa kafara Mhe. Waziri, wakati yeye kama nilivyozungumza ni msafi muadilifu, msema ukweli na mchapakazi mzuri sana. *(Makofi)*

Lakini kama hatukusema ukweli hapa na kumueleza ukweli Mhe. Rais, tatizo linaonekana wazi kabisa watendaji wakuu ndio tatizo. Kwa mfano, jana Mhe. Mbarouk Wadi Mussa alisema hapa kwamba Katibu Mkuu wa wizara hii ni tatizo. Mhe. Spika, hata uteuliwe wewe pale kwa ajili ya kuiongoza wizara ile, kwa sababu wewe ni muadilifu, mchapakazi, mkweli lakini itakushinda wizara ile. *(Makofi)*

Mzee wangu Mhe. Ali Juma Shamuhuna amekaa pale na tumbo limemuwaka moto, siku mbili tu wizara imemshinda na Mhe. Rais amemuondoa na hata aende nani wizara ile. Mhe. Spika, wizara ile ni nyeti, ambayo inawagusa wananchi na roho ya serikali hii iko katika wizara ile. *(Makofi)*

Lakini wasi wasi wetu unakuja kwamba kila Mhe. Waziri anayekwenda pale siku mbili tatu tukija Barazani kila Mhe. Mjumbe anayekuja hapa anazungumzia kuhusu wizara ile, yaani bajeti zote zinazokuja hapa moto ni Wizara ya Ardhi. Mhe. Spika, nadhani tatizo kubwa pale ni Katibu Mkuu na baadhi ya watendaji, na hilo lazima tuseme na hapa ndipo pa kusema. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Mhe. Rais lazima aangalie na nimemuomba sana Mhe. Katibu Mkuu aliangalie tatizo lake nini? Na ajirekebishe na tuhakikishe wizara ile inakwenda katika hali ambayo wananchi, wapiga kura wetu kule, basi na wao angalau pamoja na sisi humu Barazani tuwe tunakaa na hatuisemi Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Nikiendelea na mchango wangu sasa nije katika Idara ya Nyumba ya Maendeleo na Makaazi. Kwanza nitoe pongezi kwa idara hii kwa kufanya ukarabati katika majengo yale ya Kengeja kule, ambapo Wajumbe wa Baraza hili ndio walilisema hali halisi ya majengo yale, lakini waliitikia wito ule na kuweza kufanyia kazi na angalau hivi sasa nyumba zile zina sura ya kupendeza.

Lakini nyumba zile za maendeleo ambazo alitujengea baba yetu, mzee wetu mpendwa Mzee Abeid Amani Karume, ametujengea majengo yale kila kona ya nchi hii, kama vile ukienda Pemba na Unguja yapo, wananchi wetu wanaishi katika majengo yale. Kwa kweli tokea kujengwa majengo yale baada ya kupata uhuru au Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964, tuko kwenye miaka 48 na tunaelekea katika miaka 50 ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964.

Mhe. Spika, Nyumba za Maendeleo za Michenzani ziko katika mji huu, yako kwenye kitovu cha mji huu na wageni mbali mbali wanapokuja tunakuwa tunajisifia kwamba nyumba hizi anatujengea muasisi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naiomba sana Idara hii ya Nyumba na Maendeleo kuyafanyia ukarabati majengo yale, angalau kuyapiga rangi tunaelekea kwenye miaka 50 ya Mapinduzi Matukufu, basi ikifika hapo miaka 50 ya Mapinduzi Matukufu majengo yale yawe yanang'ara na kupendeza kama ambavyo yalivyokuwa hapo mwanzo. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, alichukue hili na kulifanyia kazi na kuhakikisha kuwa miaka 50 inayokuja ya Mapinduzi Matukufu majengo yale yawe yanang'ara. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nikija kwenye Mamlaka ya Maji. Kwa kweli tatizo la maji bado lipo kwa nchi nzima na hususan Mkoa wa Mjini Magharibi. Mhe. Spika, maji yote yanayokuja mjini yanapitia katika Jimbo la Rahaleo na wala hayamfiki Mhe. Ismail Jussa Ladhu kabla hayajapita Rahaleo. Lakini jambo la kusikitisha na kushangaza Jimbo la Rahaleo lina matatizo ya maji, hususan katika maeneo yale ya Nyumba za Maendeleo, kama vile Nyumba No. 4, nyumba nyengine pamoja na maeneo mengine. *(Makofi)*

Kwa hivyo, katika kushajihisha na kuchangia huduma za maji kwa wananchi mimi naliunga mkono. Lakini hapa Mhe. Spika, kuna tatizo, na tatizo hili mwanzo wakati wanatoa huduma hizi kunawekwa mita katika kuchangia huduma za maji, maeneo ya mwanzo kuweka mita hizi ni maeneo ya Makadara ambayo yamo katika Jimbo la Rahaleo na mwanzo walikuwa wakichangia shilingi 2,000/=. *(Makofi)*

Mhe. Spika, leo wananchi wanyonge wanalipishwa maji kuanzia 12,000/=, 20,000/= na hata 30,000/= kwa mwezi tatizo nini? Wananchi wetu ni masikini. Sasa leo mwananchi analipishwa maji kwa mwezi shilingi 20,000/= au 30,000/= na mwanzo ilikuwa inaelezwa kwamba uchangiaji wa maji utaanzia shilingi 2,000/=, basi angalau isiwe shilingi 5,000/=. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kuliangalia kwa kina suala hilo. *(Makofi)*

Lakini mbali na hayo Mhe. Spika, zile mita zinapoharibika mwananchi yule analipishwa shilingi 50,000/= kwa ajili ya matengenezo ya mita ile, sasa hili ni tatizo na tunawapa mzigo wananchi wetu. Kwa hiyo ningemuomba Mhe. Waziri kulifuatilia kwa kina suala hili ili kuweza kuwapunguzia mzigo wananchi wetu.

Mhe. Spika, nije katika Shirila la Umeme. Shirika la Umeme bado matatizo yetu tunayo, na kila Mjumbe aliyesimama alilizungumza. Mbali na ugumu au

na matatizo ya umeme, wananchi wanaumia, unakwenda kulipa umeme, mwananchi masikini ya Mungu shilingi zake 10,000 lakini anapewa umeme wa siku moja, siku ya pili umeme umekwisha. Hili ni tatizo na ni lazima tuliangalie. Ningemuomba sana Mhe. Waziri tulifuatilie kwa kina suala hili. Kwa sababu hili limezungumzwa sana kwa hivyo Mhe. Spika, tatizo la umeme lipo, ningemuomba Mhe. Waziri tukalifuatilia na kuhakikisha kwamba suala hili linapatiwa ufumbuzi.

Mhe. Spika, nikija katika jimbo langu la Rahaleo maeneo ya Misufuni pale kuna *transformer* nadhani toka niwe Mwakilishi huu ni mwaka wa pili na nusu, lakini nimeikuta *transformer* ile wiki inaharibika, wiki inaharibika, watu wanaunguliwa na vitu vyao. Siku moja mpaka imewaka moto pale katika maeneo ya Misufini. Nashangaa kwa nini inakuwa hivi na wakati taarifa hizi zimepelekwa katika Shirika. *Transformer* ile bado haijatengenezwa, wanakwenda pale inachezewa siku mbili inaungua. Ningemuomba sana Mhe. Waziri kulifuatilia suala hili kwa kina kabisa, kuwaondolea matatizo wananchi wa jimbo la Rahaleo.

Mhe. Spika, haya yanakuja kutokana na matatizo ya ardhi na huku kujijengea jengea ovyo. *Transformer* ile iko karibu na majumba, nadhani na ndio tatizo ambalo inakuwa inaungua mara kwa mara. Ningemuomba Mhe. Waziri kuangalia miundombinu ili kuhakikisha kwamba aidha inaondoshwa *transformer* ile au kutafuta taratibu ambayo itahakikisha tatizo lile linaondoka.
Mhe. Spika, mwisho nachukua fursa hii kurejea tena na kumpongeza sana Mhe. Waziri pamoja na Naibu wake katika kusimamia vyema Wizara hii. Lakini nililolizungumza lazima lifanyiwe kazi na Mhe. Rais ananisikia kwa sababu hapa anatuona na anafuatilia kila kitu, tatizo ni Katibu Mkuu wa Wizara hii. Baada ya kusema hayo naunga mkono kwa asilimia 100.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kwa kuweza kunipa nafasi hii kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Mimi jambo langu la mwanzo ambalo nataka nilizungumzie ni suala zima la Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana.

Mhe. Spika, katika Kamisheni hii ya Wakfu na Mali ya Amana, walikabidhiwa nyumba 78 ambazo nyumba hizo zipo mikononi mwao na wao ndio wanaozishughulikia. Katika nyumba hizi kuna nyumba kiasi au *flat* 19 bado hawajakabidhiwa Kamisheni ya Wakfu. Watu ambao waliopatiwa fidia zao waliofariki, sasa nyumba hizi zinatakiwa zikabidhiwe Kamisheni ya Wakfu na kwa taarifa yako Mhe. Spika, nyumba hizi au *flat* hizi 19 tayari zimeshagaiwa kwa watu wengine. Jambo ambalo sio utaratibu. Japokuwa *flat* hizi 19 warithi wake bado hawajapatikana, lakini kwa utaratibu sio zirudi

katika Idara ya Nyumba au wazikabidhi wao. Ni lazima nyumba hizo *flat* 19 wazirudishe katika Kamisheni ya Wakfu, na wao kama zimeshindikana kupatikana watu wake kwa utaratibu ulivyo *flat* hizi 19 zipelekwe *Baitul Maal*. Nyumba hizi hazikupelekwa na zipo katika Idara ya nyumba bado mpaka leo.

Kwa suala hili Mhe. Spika, si jambo zuri kwa Idara ya Nyumba kuzizuia nyumba hizi na wakaanza kuzikodisha na kodi ile wanachukua wao Idara ya Maji. Ilikuwa kodi iendelee katika Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana. Kwa hivyo nataka nimuulize Mhe. Waziri kama suala hili halijui hiyo ni taarifa na kama analijua Mhe. Waziri atupe maelezo baadae katika majumuisho.

Mhe. Spika, suala la pili ambalo nataka nilizungumze ni suala la *Zanzibar National Plan***.** Suala hili liko zamani la muda mrefu kwamba tunatakiwa tuwe nacho kitu rasmi kabisa. Tuwe na ramani ya Zanzibar ambayo ramani hiyo inaonekana kwamba ni ya muda mrefu. Taarifa zake ziko za siku nyingi, kila siku maelezo yake yanakuwa yanajirudia rudia yale yale ya ramani ya Zanzibar.

Mhe. Spika, ramani ni kitu muhimu sana kwa ajili ya taifa letu. Hili linaweza kutupa taarifa sahihi juu ya tafsiri kamili ya utambuzi wa maeneo ya ardhi. Mhe. Spika, kwa taarifa yako inavyoonesha tangu siku hizo mpaka hii leo, Ardhi bado haijapangwa kwa maendeleo ya jamii. Matokeo yake ikiwa ardhi hiyo bado haikupangwa ni kusema kwamba ujenzi unaoendelea katika ardhi hii ya Zanzibar ambayo haina *plan* ni nyumba ambazo zinajengwa kiholela, zilizokuwa hazina mpango. Ingawa kuna baadhi ya maeneo nyumba zake zimepangika vizuri na linapotokezea jambo linaweza kutekelezeka. Ujenzi wa kiholela ambao uliokuwa haukupimwa, matokeo yake huduma muhimu zinakosekana katika maeneo haya.

Wakati inapotokezea matatizo ya umeme tunahitaji kupata gari za kuzimia moto ambao umetokea pale. Kwa mshangao utaona gari hizo zinashindwa kupita katika maeneo ambayo nyumba zimebanana sana ili wakaweza kupeleka huduma hiyo. Hilo ni tatizo kubwa na mpaka leo suala hili limeshindikana. Mimi nasema majukumu ya Wizara hii ni makubwa sana, nikianza Ardhi ambayo inabeba wananchi, maji yanawabeba wananchi, makaazi yanawabeba wananchi na nguvu ambayo ni nishati ambayo wananchi wanaitegemea. Ni majukumu makubwa sana na yanahitaji uadilifu wa watendaji. Kama uadilifu wa watendaji sio mzuri, haya ndiyo yanayotokezea na tutaendelea kupiga kelele katika Baraza lako Mhe. Spika, kuona hali ambayo wananchi wanajifanyia mambo wanayoyataka, lakini ni kwa uwezo wa watendaji ndiyo wanayoyasababisha haya.

Mhe. Spika, la pili ambalo naweza kuona kwamba nyumba zimebanana namna hiyo kutakuwa na msokotano wa maji ambayo maji yake yatakuwa ni machafu na pengine yatakuwa hayana michirizi ya kupitia maji haya. Mhe. Spika, ningemuomba Mhe. Waziri kwenye suala hili alifuatilie kwa kina ili kuona kwamba Zanzibar imejipanga vizuri katika hali zote.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nataka nilizungumzie ni suala zima la umeme. Tunakotoka sisi tunatoka mbali mbali na hali kila siku tunasema kwamba Zanzibar iwe na maendeleo, tupunguze umasikini kwa wingi sana. Kila tunapokaa hapa tunajadili suala la umasikini. Katika nchi yetu bila shaka watu hawawezi kuishi bila ya maji, bila ya umeme, lakini asili yao umeme ulikuwa haupo, tukaweza kutumia taa zetu za kawaida za kandili na vibatari. Hatimaye tukaanza kuishambulia misitu kwa kutumia kuni kama ni nishati. Tukatumia makaa kama ni nishati, tukatumia mafuta ya taa kama ni nishati. Lakini baadaye tukaona ili tuwe na maendeleo mazuri zaidi ni lazima tupate umeme.

Mhe. Spika, hali ya umeme Zanzibar ni kwamba tumejiunga Tanzania Bara na umeme, lakini hali iliyojitokeza umeme ambao tunaupata kutoka Tanzania Bara miaka ya nyuma tulipiga kelele nyingi sana, kwamba hali ya umeme Zanzibar ni ghali. Lakini kwa sababu umeme huu tunauchukua kutoka Tanzania Bara hatuna namna hata kama utakuwa ni ghali kiasi gani itabidi tuende vile vile wanavyotaka wao.

Mhe. Spika, chanzo hichi cha kufanya umeme ghali ndio ile inayoendelea zaidi katika uharibifu wa misitu juu ya ukataji wa kuni ili watu waweze kupata huduma ya nishati kwa ajili ya kupikia. Kwa hivyo utakuta bado tunaendelea na suala hili na sisi tunaanza kupiga kelele muda mrefu, kusema kwamba umeme Zanzibar ni ghali. Tulizungumzia hapa umeme Zanzibar kwamba tuwe na umeme mbadala. Suala hili naona kwa Zanzibar kwa wizara hii naona haijatupa muelekeo.
Mara nyingi sana tunazungumza juu ya suala la Zanzibar kwamba sisi Wazanzibari tangu tulipokuwa tunaanza kutumia majenereta ambayo ya kutupa nishati hiyo, tukaona gharama ya kutumia majenereta kwa ajili ya matumizi ya mafuta. Gharama zimekuwa kubwa sana, na hata Shirika la Umeme lilikuwa linashindwa kuendeleza. Tukaondoka katika utaratibu wa majenereta, sasa tunatumia umeme huu ambao tunaupata kutoka Tanzania Bara.

Lakini hata hivyo Zanzibar kama ni nchi inahitaji kuwa na umeme wake wenyewe bila ya kutegemea Tanzania Bara. Na wao wataendelea kutuhangaisha kwa bei za kila siku za kupandisha umeme kwa Zanzibar. Kwa

sababu umeme si wetu, wao wanatumia umeme wa *hydro electric power*, kwa hivyo hawa hawana matatizo sana. Bei za Bara na bei za hapa zipo tofauti sana. Kutokana na haya tunahisi kwamba tulitoa muelekeo hapa katika Wizara, na ilikuwa inazungumza utaratibu wa kuwasaidia wananchi katika umeme. Mbali ya nishati hii ambayo tunategemea kutoka Bara lakini hata hivyo kulikuwa na mbinu nyengine za kuweza kupata nishati nayo ni njia ya upepo, njia ya jua, *solar energy* na njia ya umeme wa kawaida. Lakini sasa suala hili limekuwa zito, hiyo *solar energy* hatuioni kutekelezwa, upepo hatuuoni kutekelezwa.

Suala la madai yetu sisi kama Wazanzibari tunasema tuwe na umeme wetu wenyewe. Kwa nini Serikali mpaka sasa hivi inashindwa suala hii kulizungumza au kulitilia nguvu kwamba sisi tunao uwezo. Nakumbuka kipindi cha miaka iliyopita, wataalamu walikuja Zanzibar, walikuja na Pemba wakaangalia katika maeneo ya Mashariki kwa kutumia mawimbi ya bahari Pemba. Uwezekano wa kupata suala zima la umeme lipo kwa sababu ya nguvu ya mawimbi ya bahari.
Kwa nini suala hili halitaki kuzungumzwa, kwa nini suala hili linapuuzwa. Bado tunaendelea sisi kutumia umeme wa majirani, mpaka lini tutaendelea kutumia umeme wa majirani. Ningemuomba Mhe. Waziri je, katika wizara yake suala hili analo. Je, limewahi kuzungumzwa, kama halijawahi je, hajasikia kelele za Wawakilishi katika Baraza hili kwamba wanataka umeme mbadala. Suala hili namuachia Mhe. Waziri atakapokuja atusaidie ili kuweza kutuwekea katika hali nzuri.

Mhe. Spika, katika suala zima la umeme niseme mimi mwenyewe binafsi yangu nimeshakwenda katika Shirika la Umeme kununua umeme. Ni jambo la kushangaza kuanzia baada ya kipindi cha Juni kuingia katika kipindi cha Julai, taarifa za ulipaji wa umeme zimekuwa tofauti kwa wananchi siku hadi siku.

Mimi hapa ninazo risiti nyingi sana ambazo zinaeleza jinsi ya kuwa umeme kila mtu anapewa namna yake. Kuna mwezi wa sita huu umeme wa Shs 10,000/- nilipata *units* 52.6 kwa mwezi wa 6. Ukija katika mwezi wa 7 zilipatikana Units 36 tizama tofauti kutoka 52 mapaka 36. Ninayo risiti nyengine ambayo hii ni ya Pemba inazungumza kwa mwezi wa Julai kwa Shs. 10,000/- zilikuwa 38.5 na juzi siku hii iliyopita umeme wa Shs. 10,000/- nilipata units 31. Angalia zamani kabla ya mwezi huo tulikuwa tunapata *units* 72 au 70 na zaidi, kutoka 70, zikaangukia 50 hata 40 hazikupita zikaangukia moja kwa moja 35, 34, 31, tunauliza hii kwa nini iwe hivyo Mhe. Waziri. Hao watu wako wanatufanyia makusudi.

Mhe. Spika, sisi tunatumia umeme wa LUKU ambao hatudaiwi, kama ingekuwa mtu anadaiwa nyuma ungekuwa unasema kwamba labda nyuma una deni, lakini kwa sasa huna sababu mtu ya kuwa huyu apewe 30, mara nyengine unapewa 50, mara nyengine inakuwa unapewa 31. Suala hili Mhe. Spika, tunaliomba kwa Mhe. Waziri alifuatilie, wananchi wanalalamika sana kutokana na tofauti za umeme kwa *units* kwa kila siku. Akikaa mtu mwengine akibadilisha zamu za ufanyaji kazi na utoaji wa *units* pia unabadilika. Ningemuomba Mhe. Waziri hili suala akalifuatilia na baadaye wakati wa majumuisho atueleze *kaifa* hii ya madukhuli yanayopotea bila ya utaratibu.

Mhe. Spika, uchimbaji wa mafuta na gesi asilia Zanzibar imekuwa ni suala gumu. Na sijui kwa nini suala hili likawa gumu katika uchimbaji. Nakumbuka kipindi kilichopita cha nyuma cha Mhe. Waziri Mansoor, tulizungumza kwa urefu, Sera za Mafuta na nishati zikawekwa, uchimbaji na kila kitu tulikuwa nacho.

Baada ya mwaka mzima hatukuulizwa tena lolote juu ya suala la uchimbaji. Tunasema hili suala la mafuta na gesi asilia ambayo kama itakuwepo, hii ni rasilimali za Wazanzibari. Ni rasilimali yao wenyewe ndio Mwenyezi Mungu alivyotujaalia kwamba sisi hatuna rasilimali nyengine. Mradi wetu mkubwa ni biashara, lakini sisi Mwenyezi Mungu katujaalia mafuta na mafuta tumeyakalia tunayo. Lakini hatuoni raha sisi Wazanzibari baadhi yetu mpaka mradi huu wa mafuta wapewe wenzetu jirani zetu, kwa nini, wakati hii ni haki yetu wenyewe. Mafuta yapo katika ukanda wetu wa Zanzibar, hayapo mahali pengine. Suala hili la mafuta na gesi asilia si la muungano ni suala letu la Wazanzibari ni rasilimali yetu sisi Wazanzibari.

Kuna maelezo hivi sasa ya TPDC inataka kutafuta mafuta. Inahusu nini TPDC kutafuta mafuta Zanzibar. Tuko tayari sisi Wazanzibari kutoa rasilimali yetu. Sisi Waheshimiwa tuliokuwepo hapa katika Baraza la Wawakilishi jukumu hili ni letu sisi Wazanzibari. Kama rasilimali hii itatoka itakwenda kutumiliwa na watu wa nchi nyengine, jukumu hili litakuja kwa watoto wetu tutaowazaa. Kwa sababu watakuja kuuliza rasilimali zao za ardhi ziko wapi, rasilimali zao wa baharini ziko wapi nini jibu tutakalotoa. Tukiwapa wenzetu majirani kutafuta mafuta hata ile leseni kitu cha mwisho itakwenda Tanzania Bara.

Mhe. Spika, Mwenyezi Mungu akitujaalia rasilimali hii tukiipata wenyewe *Wallahi Laadhim* na mimi nasema kutokana na idadi ya *population* iliyopo Zanzibar kila mmoja atavunja kibanda ajenge nyumba ya ghorofa. Kila mmoja katika familia atakuwa na gari yake mwenyewe ya mkewe na wanawe.

Waheshimiwa hili suala sisi hatulitaki, nani anaekataa starehe, nani anaekataa mazuri. Urafiki huu na udugu huu lakini si kwa mafuta. Mafuta ni yetu wenyewe na namuomba Mhe. Waziri hili suala lilete hapa katika Baraza tulizungumze. Kipindi kinachokuja cha Oktoba lilete, mambo ya mchezo wa rasilimali ya Zanzibar kuchezewachezewa na watu wengine hatutaki.

Mhe. Spika, rasilimali Tanzania Bara zipo nyingi sana kuna *tanzanite*, dhahabu, aluminium, gesi na mambo chungu mzima. Tangu mwaka 1984 ilitiwa katika Katiba ya Zanzibar na Katiba ya Jamhuri ya Muungano kwamba mafuta na gesi asilia ni ya Muungano. Je, hii ilikuwa ni ridhaa ya *revolution government*, haikuwa ridhaa ya *revolution government*, haikushauriwa, haikuulizwa imeingizwa tu kwa mabavu. Kwa hivyo kama imeingizwa na sisi tutaitoa. Mafuta ni yao wenyewe Wazanzibari na watafaidika wenyewe na sisi tunataka tupate hichi kitu. Umasikini unatutia unyonge, tumekuwa mwili wetu kama jivu, hatung'ari tena kwa umasikini, tumedumaa. *Wallahi* rasilimali ipo pale kila siku atakuja huyu, atakuja huyu, mara tutaambiwa ngoja kwanza sijui kaja nani tuzungumze kidogo. Watu wanachukua muda, huku Tanzania Bara wanaendelea kutafuta mafuta na gesi asilia, kila siku *day after day* na sasa wanataka kuja na TPDC walitaka kuifanya *Tanzania Petroleum Development Corporation* iwe ya muungano maana iwe na nguvu zaidi, wakati ni kitengo tu ambacho hakipo katika muungano. Lakini kimepewa nguvu ili kije hapa kitafute mafuta *yaguju!*, mafuta haya hatuyatoi, mafuta ni ya Wazanzibari na rasilimali hii, watoto wetu watakuja kufaidika baadae.

Mhe. Waziri tunakuomba kwenye suala hili sisi Wazanzibari hatuko tayari kwa mafuta yetu kuwapa watu wengine hatutokuwa tayari wala hatuko tayari kwa suala hili. Mhe. Waziri tunakuomba ulichukue hatua kwa haraka ili kipindi cha Oktoba kinachokuja hapa utwambie hali halisi, na sisi tutaleta hoja hapa katika Baraza kipindi kinachokuja. Kwamba tulijadili hili suala.
Mhe. Waziri nakushukuru sana Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipatia nafasi na naunga mkono hotuba ya Waziri mia kwa mia. Nakushukuru.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi kuweza kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Mhe. Spika, mimi nitachangia kuhusu masuala ya ardhi katika Mkoa wa Mjini Magharibi.

Mhe. Spika, naanza katika jimbo la Mfenesini kuna sehemu inaitwa Selem, naiomba serikali iwafikirie wananchi waliokuwa wanalima katika mashamba yale na wanaishi katika maeneo yale wamepewa viongozi. Naiomba serikali iandae utaratibu mzuri ili kuona sehemu ya mashamba hayo na wao

wanapatiwa. Nikija katika sehemu ya jimbo la Dole, na wao pia wana matatizo hayo hayo ya ardhi.

Mhe. Spika, nikiendelea katika mashamba ya Selem wananchi wengi mashamba hayo wameanza kutumia tangu mwaka 1964, lakini leo hii katika maeneo yale wamenyang'anywa na wamepewa viongozi.

Nije katika suala la umeme. Umeme umepanda bei kubwa wanyonge hawawezi kuhimili kulipa. Kwa hivyo naiomba serikali iangalie tena hali hii ili kuona wananchi wetu wanaweza kumiliki. Shirika la Umeme liwe na mipango madhubuti ya kuwafahamisha wananchi juu ya ukatikaji wa umeme mara kwa mara. Hili ni tatizo umeme kila wakati unakatika lakini hakuna sababu. Naomba serikali na hili ilifuatilie ili tuone sababu iko wapi.

Mhe. Spika, kuhusiana na umeme mdogo, hili nalo ni tatizo kwani linawatia hasara watumiaji wa umeme kwa kuungua vitu vyao. Mwananchi wa chini kila siku ikiwa vitu vyake vinaungua tunamtia hasara, mwenyewe kakusanya pesa zake kenda kununua kitu halafu baada ya muda kinaungua kutokana na umeme hili ni tatizo.

Mhe. Spika, nije kwenye maji, kwenye maji Ramadhani inakuja tatizo la maji hasa katika Mkoa wa Mjini Magharibi, tatizo la maji ni kubwa wanawake tunapata tabu, tunahangaika kwa kutafuta maji, hatulali hatujui maji haya lini tutapata kwa uhakika. Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja aje kunieleza kuhusu huu mradi. Hotuba yake ilitwambia kuna mradi sasa nilikuwa ninamuomba aje kutwambia mradi huu utaisha lini ili na sisi tuondokane na tatizo hili la maji.

Tatizo hili la maji Mhe. Spika, kusema kweli sijui tuseme vipi kwa sababu kipindi kilichopita pia tumelizungumza lakini bado maji katika maeneo yetu wengine tunatumia visima, na hivyo visima havina uhakika, kwa hivyo tunaomba Mhe. Waziri aje kutwambia tatizo hili litaisha lini.

Mhe. Spika, kusema kweli mimi baada ya kutoa mchango wangu huo naunga mkono hoja mia juu ya mia.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii adhimu na mimi kuweza kuchangia hotuba ya Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetujaalia hapa leo tumekuja na afya njema na kuja kulitumikia taifa letu. Vile vile nichukue fursa hii adhimu kumpongeza sana Waziri pamoja na watendaji wake kwa kutuandalia hotuba nzuri ambayo inatupa matumaini kwa ajili ya maendeleo ya 2012/2013.

Mhe. Spika, mimi naanza moja kwa moja ukurasa wa 9. Mhe. Waziri ametueleza katika hotuba yake kuwa kuna mafunzo ambayo wanapewa wafanyakazi, sasa mimi kwa sababu nipo hapa kwa niaba ya wanawake nilikuwa naomba kumuuliza Waziri anipe mchanganuo wa kujua wanawake wangapi ambao wameweza kunufaika katika mafunzo haya. Nasema hivi kwa sababu sisi Zanzibar tumekubaliana kimataifa kwamba tumuwezeshe mwanamke, tuna mkataba wa kimataifa ambao unasema kumu-*empower woman* sasa hapa tunataka *data* za kuonesha kweli yale ambayo tumeyakubali kimataifa tunayatekeleza. Na hili nalisema kwa Mhe. Waziri wa Ardhi lakini na mawaziri wengine wapo ningeomba taarifa zozote ambazo zinakuja hapa zinazohusiana na wafanyakazi basi zitoe mchanganuo wa wanawake na wanaume ili tusaidie katika kutoa *data* zetu za baadae.

Baada ya hapo Mhe. Spika, nakwenda katika ukurasa wa 11 ambao unazungumzia utayarishaji na utoaji wa hati. Mhe. Waziri mimi kidogo nimeshtushwa na kauli ambayo imesema kwamba kuna baadhi ya wananchi kwa bahati mbaya wamekuwa wakikengeuka sheria hiyo kwa kuhaulisha ardhi bila ya kupitia katika bodi, na wamekuwa wakiomba hati ya haki ya matumizi ya ardhi, hapa naona pana matatizo. Na tatizo lenyewe ni la utendaji, huyu mtu ambaye anakiuka sheria lakini wakati huo huo anapewa hati anaipata wapi. Ikiwa katika utendaji hawa watu wote wanatoa kitu kimoja lakini akienda katika taasisi moja anapewa moja kwa moja bila ya kuangalia kama taasisi nyengine imemruhusu. Ina maana kwamba hizi ofisi zetu hazina *coordination*, hapa pana udhaifu wa utendaji na huu tumeuona katika taasisi nyingi sana.

Mhe. Waziri kamati yangu ilikaa pamoja na watendaji wa taasisi mbali mbali ambazo zinahusiana na masuala ya ardhi pamoja na mazingira pamoja na uwekezaji. Kwa bahati mbaya siku tulokutana nao pamoja na watu wa Wizara ya Fedha tukakuta kwamba kuna udhaifu mkubwa wa *coordination* ya watu hawa.Taasisi ya Uwekezaji kuna masuala ambayo hawayajui ambayo wamesema kwamba sisi sio tuliotoa ruhusa, sisi sio dhamana wa hili, tumewarudisha tukawaambia nendeni mkakae inavyoonesha kuna udhaifu mkubwa katika *coordination* baina ya hawa watu. Na hili ndilo linalosababisha kwamba watu wanakiuka sheria. Ikiwa mtu anatakiwa aende kwenye taasisi tano lakini anakwenda kwenye taasisi moja tu na akafanikikiwa ina maana kwamba watekelezaji ndio wanaokiuka sheria na sio yule mtu.

Mhe. Spika, nataka kuzungumzia mahkama ya ardhi na matatizo kwa ujumla ya ardhi. Mhe. Spika, nimepata vile vile kutembelea maeneo mbali mbali katika kamati yetu na tumegundua kwamba kuna matatizo makubwa ya ardhi,

lakini matatizo haya wenyewe wanasema kwamba yanasababishwa na wakubwa. Sasa hapa Mhe. Waziri usiniulize mkubwa gani kwa sababu simjui lakini hiyo kauli ndiyo inayosemwa na wananchi. Lakini naamini kwamba hawa watu wanajua wenyewe. Inasikitisha sana kwamba tumekwenda Uroa tumekuta eneo la makaburi la wananchi limechukuliwa na muekezaji. Mhe. Spika, inasikitisha sote sisi tuna wazee wetu waliotangulia mbele ya haki, sote sisi tuna ndugu zetu waliotangulia mbele ya haki, hakuna mmoja kati yetu sisi atakayefurahi kuliona kaburi la ndugu yake au la mzee wake limefukuliwa akapewa muekezaji akajenga hoteli.

Mhe. Waziri nakuomba uende Uroa ukawasikilize wale wananchi wa Uroa tatizo lao ni kubwa, wamesema wanamwachia Mungu. Ikiwa sisi ndio tumechaguliwa kwa ajili ya kusimamia haki za wananchi hawa basi tusifike huko tuwatendee haki Mhe. Waziri nakuomba sana hili ulisimamie. Lakini licha ya hayo Mhe. Waziri mimi nimeona matatizo mengi ya ardhi yamejitokeza kwa sababu nyingi.

Moja ikiwa ni elimu, elimu kwa wananchi, wananchi wengi bado hawajakuwa na elimu ya kutosha inayohusiana na ardhi, Mhe. Waziri hii ni kazi ambayo inatakiwa ifanyike kwa nguvu sana kuhakikisha kwamba wananchi tutumie kila mbinu, Mhe. Waziri usione tabu kutoa kifungu cha fedha kuwapa asasi za kiraia kutoa elimu hii uwezo wanao. Asasi za kiraia wana uwezo wa kutoa elimu hii wape nafasi hiyo. Katika maeneo yote, katika majimbo yote katika wilaya zote zipo asasi zinazoshughulikia masuala hayo. Kutana nao Wizara yako itoe iwape uwezo asasi hizi waweze kutoa elimu. Bila ya hivyo Wizara yako Mheshimiwa haiwezi kufanya kazi.

Mhe. Waziri mimi nilikuwa na wazo jengine ambalo ninafikiria sasa hivi umeshafika wakati wa kulifanya, tuna Mahkama ya Ardhi, lakini Mahkama ya Ardhi ipo moja ninavyotambua mimi, sasa matatizo ya ardhi yapo mjini na yapo vijijini. Lakini tuna Mahkama za Wilaya, Mhe. Waziri kwa nini sasa hivi katika kila Mahkama ya Wilaya tukaanzisha *desk* ambalo litakuwa linashughulikia kesi za ardhi tu.

Mhe. Spika: Maelekezo yako yaelekeze kwa Spika.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mhe. Spika, ninashukuru kwa kuniongoza; ninachokisema tuwe na *desk* maalum ambalo litakuwa linashughulikia masuala ya matatizo ya ardhi, na tuwe na Jaji pamoja na wanasheria ambao wana uwezo waweko Wilayani kwa ajili ya kushughulikia kesi za ardhi. Hii itapunguza gharama, hii itapunguza ucheleweshaji wa kesi hizi. Kwanza kwa sababu gharama watu ambao wako mjini kuanza kufuatilia kesi ambazo zipo maeneo ya mbali itakuwa ni vigumu. Lakini leo Wilayani pale pale watakuwa

na uwezo mkubwa wa kushughulikia kesi zile na hasa ikiwa wale watu ambao wanashughulikia kesi zile wapo karibu na wale waliohusika na hizo kesi. Kwa hivyo Mhe. Waziri mimi naomba tufanye hili na ninaamini kwamba tukifanya hivi kwa upande mmoja tunaweza tukafanikiwa haraka, ikiwa kama kesi imeshindikana basi itapelekwa mbele ya mahkama nyengine ambayo inashughulikia. Lakini kwa hapa tuanzie katika Wilaya.

Mhe. Spika, naomba niende katika ukurasa wa 17, ukurasa wa 17 Idara ya Mipango ya Miji na Vijiji. Mhe.Spika, Waziri katueleza mipango mingi ambayo wamekusudia kuifanya katika kupanga, uhifadhi, uendelezaji na matumizi endelevu ya ardhi yetu. Lakini Mhe. Spika, mimi hapa kidogo nina hofu na nina wasiwasi, kwamba mipango hii tunayoipanga ni mingi lakini utekelezaji wake kuonekana kwake kwa kweli ni mdogo mno. Mpaka sasa hivi hii mipango lakini ukitizama ukweli ni kama alivyosema ndugu yangu Hamza *business as usual*. Bado hakuna kigezo, hakuna kitu ambacho ni *visible* tukakiona tukasema kweli hapa wamefanya, bado kabisa.

Sasa sijui Mhe. Waziri kwa hili atakuja kutueleza nini. Mipango ipo tunaambiwa kwamba kuna mashirika mbali mbali ambayo itatoa misaada lakini bado hatujaona, na sisi wengi tunaridhika kwa kuona bila ya kuona ukimwambia mtu kwa maneno watu wameshachoka maneno sasa hivi, hiki ni kitabu tu lakini watu wanataka kuona ukweli. Wapangaji wanapokaa ofisini wakapanga, wanapanga tu lakini wanampangia nani, wanawapangia wananchi, hao wananchi ndio wanaotizama wakasema waka-*appreciate.*

Leo hapa Wajumbe wengi wamezungumzia suala la nyumba ambazo zimejengwa baada ya Mapinduzi ya Zanzibar na marehemu mzee Abeid Karume anasifiwa na ataendelea kusifiwa daima, kwa sababu yeye hakusema tu bali katenda. Mhe. Spika, tuone kinachofanywa kwenye karatasi haisaidii kabisa.

Mhe. Spika, mimi nakwenda katika ukurasa 25 naendelea kuna Idara ya Upimaji na Ramani. Mhe. Spika, hapa zimetolewa *data* kwamba mpaka sasa hivi viwanja vimepimwa 303 viwanja hivyo 154 kwa ajili ya makaazi, 15 kwa ajili ya huduma za jamii, 45 kwa taasisi za serikali na maeneo 77 kwa kilimo na kumi na mbili kwa ajili ya vitega uchumi. Mhe. Spika, mimi nataka kujua vigezo vilivyotumika katika kugawa viwanja hivi, nasema kwa sababu.

Mhe. Spika, katika viwanja 303 ni viwanja 15 tu ndivyo vyenye huduma za jamii, sote tunajua huduma za jamii maana yake nini hapa. Tunakosea pakubwa katika kumi na tano viwanja vya huduma ya jamii Mhe. Waziri akija hapa anieleze vigezo vyao wanavyovitumia, kwa sababu mara nyingi tunaona

miji mipya inakosa sura ya upya haipo kwa sababu vitu muhimu vinakuwa hamna.

Mheshimiwa nimesimama hapa siku ya Wizara ya Wanawake, Watoto na Vijana na Ustawi wa Jamii nikazungumzia suala la vijana kuwa na maeneo maalum kwa ajili ya shughuli zao mbali mbali za vijana. Sasa nataka aje aniambie katika miji hii kuna viwanja vingapi walivyotengewa vijana kwa ajili ya kufanya shughuli zao za vijana niambiwe hapa. Vijana wetu wanaingia katika mambo mabaya Mhe. Spika, kwa sababu hatuwatengenezei, aje aniambie hapa tunataka kung'arisha miji yetu, aniambie kuna bustani ngapi katika maeneo haya ikiwa kuna makaazi kuna bustani ngapi.

Lakini hizi huduma kumi na tano ni zipi? Kwa sababu huduma zipo kwenye mambo mbali kuna afya, kuna elimu, kuna usafiri zote katika maeneo yetu mengi yaliyojengwa hata sehemu za *parking* hamna, nyengine mpya hamna na watu kila siku wananunua magari mapya sasa sijui hivi hasa vigezo vilivyotumika ni vigezo gani. Mhe. Waziri nakuomba sana ukija hapa utwambie vigezo hiki na hiki na hiki ndio kinachotumika na ni mji gani mpaka sasa uliopangwa ikiwa kama ni Tunguu ni mji mpya au mwengine basi haya mambo yote yamo ndani ya miji ile ambayo tayari tumeipanga.

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii adhimu kumpongeza sana Waziri pamoja na watendaji wake kwa kutaka kutuletea sheria ya kuanzisha Shirika la Nyumba. Mhe. Spika, mimi ninawapongeza sana lakini nataka kutoa indhari hapa kwamba likianzishwa Shirika hili, kuwe kuna Shirika ambalo litakuwa kweli ni Shirika sio tuweke watu kwenye ma-*desk* wakae lakini watekelezaji hakuna. Tunaanzisha Shirika tuwe na hakika kwamba shirika hili litasaidia katika kutoa nyumba zenye bei nafuu kwa wananchi wa Zanzibar, hiyo ndio maana ya shirika hili. Leo shirika hili likianzishwa, nyumba zikianza kujengwa tunataka wananchi ndio wapewe kipaumbele katika kupata nyumba hizi zenye bei nafuu. Na sio watu ambao wana uwezo wa kupewa au ikiwa kama wana siasa au ikiwa kama wafanyabiashara.

Mhe. Spika, namwambia Mhe. Waziri kwa sababu katika ugawaji wa ardhi hakuna haki, kuna watu wapewe umuhimu katika kupewa makaazi, tuna wataalamu wetu wengi serikalini ni wazanzibari lakini hawana makaazi, hizi ndio faida ambazo wanaweza kuzipata. Tuna madaktari, tuna walimu hizi ni *benefit* ambazo kwa kweli wanatakiwa kuzipata.

Mhe. Spika, kwa kuwa umeniambia muda wangu umeshamaliza, mimi la mwisho nataka kuzungumzia kuhusu suala la upandaji wa umeme. Mhe. Spika, umeme unapanda, lakini unapanda kiholela, unapanda bila ya wananchi kuarifiwa, unapanda bila ya wananchi kujua kwa nini umepanda,

hatuwatendei haki wananchi. Umeme ukipanda Mheshimiwa una *desk* lako la *PR* toa taarifa, Shirika hili lina taarifa za kutosha linaweza kuwaambia wananchi kwa nini umeme umepanda. Leo umeme umepanda kiholela wananchi maskini ya Mungu wanachanganyikiwa nje, Mheshimiwa sijui nani anapandisha hii bei ya umeme.

Kwa sababu wakati unapandisha huduma kama hii muhimu lazima uwafikirie wale ambao wanapata kima cha chini cha mshahara kwanza watamudu kulipa huu umeme. Kama hukuwafikiria hao ina maana huu umeme sio kwa ajili yao, huu umeme ni kwa wale ambao wanapata pato kubwa. Umeme umepanda vibaya Mhe. Waziri sana na wananchi wanalalamika.

Lakini la mwisho Mhe. Spika, nifungie suala la maji, najua kama serikali yetu inafanya jitihada zote za kuhakikisha kwamba wananchi wake wanapata maji, lakini bado utekelezaji si mzuri, kweli matatizo ya maji yapo na *data* zinazotolewa tunaambiwa kwamba asilimia kubwa ya wananchi sasa wanapata maji nina wasiwasi na hizo *data.* Lakini nina wasiwasi kwa sababu tunaposema kwamba kilomita fulani wananchi wa Zanzibar hapo zamani walishazoea wote kama una maji uko mfereji ndani ya nyumba na maji yanatoka ndani ya nyumba tulivyozoea, tumezaliwa tumeinukia tunaona maji yanatoka ndani ya nyumba. Sasa kinyume hatuyaoni maji hilo ndio tatizo lenyewe. Sasa tukihesabiwa *miles* tukiambiwa mpaka kufikia *miles* fulani maji yanapatikana tutaendelea kusema kila siku bado.

Sasa Mhe. Waziri ninakuomba sana suala la maji lipewe kipaumbele, maji ndio kila kitu kwa mwanadamu kila siku tunayatumia maji, lipe kipaumbele suala hili tuhakikishe kwamba kwa kweli watu waseme sasa hivi suala la maji limeondoka Zanzibar. Tunayo maji mengi sana, vyanzo vya maji ni vingi sana tuvitumie.

Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii na ninaiunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ninamtakia kila la kheri Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kuweza kufanikisha hii bajeti ambayo wameileta mbele yetu.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, ninakushukuru kupata nafasi ndogo kabisa ya kuchangia hotuba ya Wizara hii inayoendelea kuchangiwa. Mhe. Spika, kwanza nianze kwa kusema kuwa tunapopitisha bajeti yale yaliyomo kwenye bajeti na tunayoyaunga mkono kwa asilimia mia moja hutarajia kuwa yatatekelezwa. Na sisi tunapotembea katika majimbo yetu hujifakharisha na kujifaragua kule kwa yale ambayo tumeshapitisha hapa. Lakini Mheshimiwa ninasikitika kwamba mambo mengi huwa yanabakia katika vitabu tu na utekelezaji hakuna.

Mhe. Spika, nianze mfano wa usambazaji wa maji vijijini. Mhe. Spika tukiangalia kitabu cha bajeti kilichopita yaani cha mwaka 2011/2012 katika ukurasa wa 52 kifungu cha 92 kinachohusiana na huo usambazaji maji vijijini. Kwa ruhusa yako naomba niisome kilivyoeleza.

'Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China imekubali kuchangia jumla ya dola za kimarekani milioni moja na laki tano kwa kazi za uchimbaji wa visima zaidi ya 30 pamoja na ujenzi wa matangi, utiaji pampu na ulazaji wa mabomba ya inchi 6 na inchi 4 katika maeneo 24 Unguja na Pemba. Kwa maelezo zaidi angalia kiambatanisho (i) kiko ukurasa wa 88'. Na mule nimekuta eneo la Mtambwe Kaskazini na Kisiwani ni moja katika hayo. Na ukitizama kitabu hiki cha bajeti tunachoendelea nacho ukurasa 48 kifungu 107 kinachohusiana na usambazaji wa maji vijijini kinaeleza kuwa kwa ruhusa yako Mhe. Spika, naomba kunukuu.

'Wizara yangu inatarajia kuendelea na mradi unaofadhiliwa na serikali ya Jamhuri ya watu wa China ambayo inatarajia kuchangia jumla ya dola za kimarekani milioni moja na laki tano'.

Huku iliyopita milioni moja na laki tano na huku inakuja milioni hiyo hiyo moja na laki tano na vijiji vilivyotajwa takriban ni vile vile. Linalonisikitisha ni kuwa safari hii Kisiwani hamna, lakini Mtambwe Kaskazini iko tena nauliza kwanza milioni moja nukta tano dola hizi za kimarekani ni nyengine au ni zile zile. Halafu Mhe. Spika, tukiangalia tuna matatizo makubwa ya maji katika vijiji vyetu, na tunasikitika tunajitahidi sana lakini tunapewa tamaa tu na wala hakuna linaloendelea.

Mhe. Spika, kwa mfano kwa baadhi ya vijiji katika jimbo langu nitakwenda shehia baada ya shehia kama ifuatavyo:

Tukija Mtambwe Kaskazini hiyo inayotiwa katika bajeti kila siku kuna vijiji vya Mtambwe Mkuu, Chekea, Kidundo, Kiapaka, na Chanjaani kote hakuna maji. Ukija shehia ya Mtambwe Kusini kuna vijiji Makongeni, Mitambuuni, Kinazini na Mawika vyote havina maji, na tukienda katika Shehia ya Piki maji yalikuwa yanapatikana Bwagamoyo, Matuuni na Mchangani lakini kwa sababu ya utengenezaji wa barabara paipu zimekatika hakuna maji. Shehia ya Kisiwani kuna Kisiwani yenyewe, Mleteni, Machuga, Tunduuni na Malindini kote hakuna maji, hii ndio hali ilivyo.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri mimi ninaomba kwa sababu hii ni serikali ya wananchi, na wananchi wanalipia kodi na sisi Wawakilishi wao huwa tunajitahidi kufika wizara zinazohusika kuomba huu msaada. Naomba tufikiriwe ili wananchi wapungukiwe na upungufu huu wa maji. Wengine

kwa bahati mbaya kwa mara ya mwanzo hivi sasa tunashindwa hata kutembea katika baadhi ya vijiji kwa kufuata kuwa kilivyosema kitabu cha bajeti ni sawa halafu mambo yale hayakutekelezeka.

Jengine Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba niendelee na umeme wa vijijini. Hii kama nilivyoanza katika vitabu vyote viwili cha mwaka 2011/2012 na hiki tunachoendelea nacho cha mwaka 2012/2013, na ukurasa ni huo huo mmoja wa 59 na maneno takriban ni yale yale yanaeleza kama ifuatavyo kwa ruhusa yako Mhe. Spika.

Kitabu kilichopita ni kuwa Mhe. Waziri alisema katika kitabu chake kwa kueleza kuwa, "kwa mwaka wa fedha 2011/2012 wizara yangu kwa kushirikiana na Shirika la Umeme itahakikisha kuwa itakamilisha kusambaza umeme katika vijiji vilivyosalia, kutokana na kumalizika kwa Awamu ya Nne ya mradi huo uliofadhiliwa na Serikali ya Norway" ama katika jimbo langu ni vijiji vingi tu, lakini kijiji kilichopata ni kijiji cha Machengwe na sisi baada ya kuchangia fedha nyingi sana.

Lakini kuna Matumbi hakuna umeme, Mleteni hakuna umeme, Machuga, Tondoni hakuna umeme, Malindini hakuna umeme. Si hivyo tu, kuna vijiji vyengine kama mfano Mtambwe Mkuu, Chekea, Chanjaani, Mkanjuni, Kivumoni, Mitambuuni na hata Kinazini. Hii ni mbaya sana, kitabu kimesema kitakamilisha kitahakikisha kitakamilisha lakini hakuna hata kijiji kimoja.

Kitabu cha safari hii ukurasa huo huo wa 59 kazi ya usambazaji umeme vijijini imeendelea kutekelezwa kwa Mfuko wa Shirika la Umeme pamoja na Mpango wa Wanavijiji hadi kufikia kataja vijiji 25 hapa, ambavyo wananchi na wao wamechangia sasa sera imebadilika. Mimi Mhe. Spika, kwa hili naomba niambiwe ukweli hasa msimamo wa wizara hii ni upi, kwa sababu watu wanahitaji umeme ukienda wanakupimia wanakwambia uchangie, hebu tuangalie katika vijiji vyote hivyo mimi nitachangia vingapi. Ukija kwenye maji ndio hivyo hivyo hebu tuangalie tutapeleka wapi.

Kwa hivyo, nakuomba kukueleza Mhe. Spika, kuwa Mhe. Waziri anapotoa maelekezo basi atwambie kweli kwa sababu sisi tukitoka hapa tunaipeleka *message*, na *message* isipotekelezwa tunaonekana kama si wafuatiliaji, wanatutia aibu na wanatukashifisha katika majimbo yetu.

Jengine Mhe. Spika, kwa ruhusa yako nichangie kidogo kuhusu nishati na madini. Mhe. Spika, kipindi kilichopita tulisomewa kitabu hiki tukaambiwa sera ya nishati Zanzibar ilikamilika na kupitishwa rasmi na Baraza la Mapinduzi Disemba hiyo, na baadae sera hiyo ililetwa katika Baraza lako tukufu Januari 2010 kwa kupata baraka za Wajumbe.

Halafu ikaeleza Mhe. Spika, ‘suala la utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia limepewa kipaumbele bado msisitizo umewekwa katika kuihuisha nishati hii kuwa ni muhimili mkubwa wa uchumi wetu’, cha mwaka jana kitabu hiki. Halatu akaendelea, “na kwa kuwa uchumi huo sio suala la Muungano”. Washughulikiaji wa rasilimali ya nishati haupaswi kuwa suala la Muungano na bila ya kuitoa katika orodha ya Muungano liko pale pale. Hiki ni kitabu cha bajeti cha mwaka uliopita tukashukuru kutokana na kazi tuliyoifanya na kitabu kilivyoeleza tukaona mambo yamekaa sawa.

Lakini tulipoangalia kitabu hiki tulichonacho ukurasa wa 52 Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nisome kimeeleza kuwa, “Wizara inaendelea kufanya juhudi ya kuwapatia mafunzo wafanyakazi wa idara hii, ili kuweza kukabiliana na upungufu wa wataalamu wa fani ya nishati ikiwemo utafutaji na uchimbaji wa mafuta hapa Zanzibar. Hata hivyo, kampuni ya *Ras El Khaimah Tanzania Ltd*, yenye Makao yake Makuu *UAE* ilikubali kugharamia mafunzo kwa Wazanzibari wenye sifa na tayari Wazanzibari wawili wanaendelea na masomo yao na wengine wanatarajiwa kwenda masomoni mara tu taratibu za safari zitakapokamilika”. Kampuni iliyotajwa hapa ni Kampuni ya *Ras El Khaimah.*

Sasa Mhe. Spika, juzi nilisoma gazeti hili nililonalo hiyo kampuni ambayo inachangia kutusomeshea watu wetu, nasoma kipande kifupi tu sisomi yote kama juzi Mhe. Spika kwa ruhusa yako, ni kuwa Kampuni moja ya Canada, *Antrim Energy* inasemekana imepewa na Shirika la Maendeleo la Mafuta Tanzania (*Tanzania Petroleum Development Corporation TPDC*) haki ya kuanza kutafuta mafuta Zanzibar. Hatua hii imefungua njia ya kuanza tena kazi ya utafutaji mafuta kwa mkataba wa kugawana kinachozalishwa (*Production Sharing Agreement*) kisiwani Pemba, ambayo ilikwama kwa miaka kadhaa.

Stephen Greer, Rais na Kiongozi Mkuu wa Kampuni ya *Antrim Energy* amesema, kufuatia kutiwa saini kwa mkataba huo Kampuni ya *Ras El Khaimah Gas Tanzania* Ltd na Kampuni ya *NOR Energy AS* ya Norway zimeingia mkataba unaoipa RAK haki ya udhibiti huo mkataba wa *PSA* kwa Pemba na Unguja. Sasa utaona Mhe. Spika, hii ndivyo hali ilivyo, huku imetajwa kuwa inasomesha watu wetu kwa habari ya mafuta na kitabu kinaeleza vizuri, lakini huku kuna matayarisho wanakuja kuchimba mafuta. Sasa Mhe. Spika, mimi nasema ni lazima tuwe wazi na kama jambo haliwezekani ni bora wananchi wakaelezwa likafahamika.

Mhe. Spika, hapana asiyejua kuwa sote kwa pamoja tulipitisha kuwa mafuta yasiwe katika mambo ya Muungano japo kuwa yamo katika *item* ya 15 ya

Katiba ya Muungano. Leo Mheshimiwa kama kweli kuna watu hawathamini jambo hili nasikitika kusema kuwa wanataka kuitia nchi hii katika mgogoro mkubwa sana. Uchimbaji wa mafuta tunajua una mambo ya kufuatilia, kuna mambo ya mazingira na kadhalika, na kuna mtu kujua kuwa hii nchi ni yake.

Wenzetu katika Katiba yao wanasema hii si nchi, sisi katika Katiba yetu hii ni nchi na ni nchi yetu ina mipaka yake na kila kitu. Sasa kuchimbwa mafuta katika eneo la Zanzibar ni kuchimba mafuta katika nchi yetu, ninaloomba Mhe. Spika, sisi tunafanya kazi ya kuhamasisha watu wetu kuhakikisha kuwa mafuta hayachimbwi, na kwa sababu serikali hii hivi sasa ni serikali ambayo wananchi ndio wenye mamlaka ya kuongoza nchi yao na wao ndio waliotutuma hapa kutwambia sisi tueleze kuwa mafuta yasiwe ya Muungano, wala tusikubali kuchimbwa kuwa ni ya Muungano, ni lazima tufuate kauli za wananchi.

Sasa ikiwa kuna wenzetu bado wanakwenda nayo haya sisemi kwa kificho, lakini kwa siri siri na halafu tukaona tu kunatoka mambo ambayo hayafahamiki *Wallahi* inatutia wasiwasi, na kwa mimi binafsi na naamini na wenzangu walio wengi wako tayari kuipinga Bajeti hii ya serikali kama hatukupewa taarifa rasmi hasa kuhusu mafuta kuwa ni mali yetu. Serikali pia kuona kuwa itahakikisha kuwa itaondolewa katika Muungano kama ilivyoahidi katika vitabu vilivyopita, na kama tulivyopitisha katika Baraza lako tukufu na mwenyewe ukiwa ni Spika wa kikao hicho tulichopitisha.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba sana na namnasihi Mhe. Waziri kama wengine kuwa kwa suala hili leo au kesho akija kutoa majumuisho tupate uhakika wa suala lilivyo tusivunganevungane. Wengine walisema hapa, kama fulani mimi najua kama serikali haijui, ile si lugha nzuri. Hivi ni watu tumechaguliwa kuwasimamia wananchi ni wao pamoja na rasilimali zao. Tunajua hatuna uchumi wa hivyo, tulipotegemea ni hapa kwenye mafuta lakini panachezwa vibaya, mafuta na gesi asilia tunasema ni ya Muungano lakini wenzetu wameshapata ma–*trillion* ya mapesa wala hakuna lolote kilicholetwa isipokuwa hivi sasa wanajidai kudai, mnamdai mtu ambaye hatujamkopesha kitu. Kwa hivyo, ni lazima tuamue na hili si ka kulifanyia masihara. Mhe, Spika, vyenginevyo tutaitia Zanzibar katika hali ya hatari na sisi kwa kutetea haki hatuogopi kuipeleka huko.

Jengine Mhe. Spika, naomba kupata ufafanuzi, Hii wizara ina majukumu makubwa na tunajua kuwa humo kwenye wizara tunakuwa na bodi zinazoendesha sekta kadhaa za wizara. Katika kutafuta tafuta nimekuta mambo ambayo yanaweza kuwa sahihi au pengine sivyo kama ninavyoyaona mimi, lakini naomba nipatiwe maelezo.

Kuna Bodi hii Mhe, Spika, ya Usajili wa wasanifu, wahandisi na wakadiriaji majengo. Bodi hii imemaliza muda wake kwa taarifa nilizonazo tokea Februari mwaka huu na haijachaguliwa nyengine na nasikia inaendelea kufanya kazi. Inatumia pesa za wavuja jasho, ningeliomba kujua kwa nini Bodi imemaliza kama inaendelea kufanya kazi na kwa nini kusifanywe harakati ya kuwekwa bodi nyengine kama maelekezo yetu tunavyopewa.

Ya pili katika wizara hii kuna bodi ya usajili wa wakandarasi nayo imemaliza muda wake mwezi huu ulioita na bado haijaendelea kufanya kazi zake, kwa vile taasisi inayohusika huwa haifanyi ki mpaka na Bodi ipitishe baadhi ya mambo. Kwa hivyo, ningeliomba kujua kwa nini na bodi hii nayo mpaka sasa hivi inafanya kazi wakati imemaliza muda wake.

Labda la mwisho Mhe. Spika, kwa sababu ya wakati ni kuwa katika wizara hii kuna Idara ya Ujenzi. Idara ya Ujenzi ninavyojua mimi walikuwa na moja ya *account* yao ambayo ilikuwa ni *Deposit Account,* ambayo walikuwa wanaweka fedha zao kwa zile kazi wanazoajiriwa kutoka nje ya wizara, na ilikuwa inaingiza fedha nyingi sana tu. Lakini kwa bahati mbaya *account* hii imefungwa na kazi zinazofanywa na Idara hii ya Ujenzi zile ambazo fedha walikuwa wakiweka katika *account* hii iliyofungwa zinaingia katika *account* ya serikali. Nataka kujua kwa nini iwe hivyo. Mhe. Spika, nashukuru.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, naomba nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Mhe. Spika, mimi leo nitakuwa na mchango mfupi sana kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kiwani ili nikuachie nafasi upate watu wengine.

Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mhe. Waziri kwa jinsi alivyotoa hotuba yake nzuri, hotuba ambayo ameihifadhi kwenye kitabu maalum na hotuba ambayo itatoa kumbukumbu kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, kwenye kitabu hiki nje kabisa Mhe. Waziri ametuwekea picha ambayo Mhe. Rais anaangalia mitambo ya maji katika Mkoa wa Mjini Magharibi kama kwamba Rais hajui kwamba kuna mitambo ya maji pale Mkoa wa Mjini Magharibi. Mimi nadhani ingekuwa busara Mhe. Waziri akatuwekea picha ya Rais anafungua angalau mfereji wenye kutoa maji, badala ya kumuonesha picha ya kuangalia mitambo ambapo wananchi wa Zanzibar hatupati maji si mjini wala vijijini kama inavyotakiwa.

Jengine Mhe. Spika, niseme kwa haraka haraka kwenye suala la Shirika la Umeme mimi sina maneno kwa sababu umetutuma tufanye uchunguzi na ukweli wa hili utaonekana mwezi wa 10 tukijaaliwa. Kwa hivyo, naomba wenzangu watulie ukweli wa uhai, usahihi, ubadhirifu na umakini mtauona

Inshaallah mwezi wa 10 kwenye Ripoti ya Kamati Teule chini ya *PAC* ambapo bila shaka kamati yetu itawasilisha.

Sasa nizungumzie kwenye ukurasa wa 11 wa kitabu cha hotuba ya Mhe. Waziri kwenye Idara ya Ardhi na Usajili. Mhe. Salum Nassor aliyepita amehoji uhalali wa bodi iliyopo na amesisitiza kwamba bodi imemaliza muda wake tangu mwezi wa pili lakini wanaendelea kufanya kazi na naomba Mhe. Waziri kwa nini hadi leo hajateua bodi nyengine. Lakini kuna usimamizi wa ukodishwaji wa ardhi tumeambiwa kwamba kuna mikataba 61 ya ukodishwaji wa ardhi tayari imetoa saini miongoni mwao mikataba 40 ni hoteli, miwili kwa ajili ya vituo vya mafuta, mmoja kwa ajili ya Kiwanja cha kufurahishia watoto, mmoja kwa ajili ya skuli, 12 kwa ajili ya wageni na mikataba mitano kwa ajili ya viwanda.

Mhe. Waziri namuomba mimi anipatie orodha ya mikataba hii na utupatie kopi kama Wawakilishi ili tujue mikataba hii imetiwa kwa utaratibu gani na vipi mmezingatia maslahi ya Wazanzibari.

Mhe. Spika, jengine ambalo naomba niseme kwamba mimi ni mmoja kati ya watu waliobahatika sana kutembea hapa Unguja kwa ajili ya kufanya utafiti wa tatizo la ardhi, kuanzia Kusini Unguja – Kaskazini Pemba Micheweni. Nimefanya hivyo kwa sababu Mwakilihi anatakiwa akizungumza aseme jambo ambalo lina mashiko. Kwa hivyo, kweli nimeambatana na Mhe. Hamza Hassan Juma na Waheshimiwa wengine kwa ajili ya kuangalia ukweli wa matatizo ya ardhi. Kwa nini tukafanya hivyo?

Kwangu mimi au kwetu sisi kama Wawakilishi kiongozi akitoa kauli hilo linakuwa ni agizo au ni amri, Rais akisema jambo kwangu mimi nachukulia kama ni agizo au amri. Mhe. Spika, leo hii ukitwambia sote kwamba humu tuvae kofia kila mtu atavaa kofia. Kwa sababu kauli ya kiongozi ni amri, sasa Rais anapotoa kwangu mimi na wale wote wanaojua maana ya kauli ya Rais hiyo ni amri wala si ombi. Kwa hivyo tukaona tutembee uangalie kwa nini kauli ya Rais haithaminiwi, tumegundua kwamba haithaminiwi kwa sababu hawa anaowapa kauli ndio waliofanya hili tatizo.

Mhe. Saleh wa Jimbo la Rahaleo alisema pale kwamba kuna haja ya Katibu Mkuu ndio tatizo aa, mimi nasema Katibu Mkuu na Wizara zake ni tatizo, na ndio maana kauli za Rais zitasemwa redioni, magazetini hazina utekelezeji. Kwa sababu hao waliokusudiwa kutekeleza kauli hizi ndio tatizo.

Mhe. Spika, tangu enzi za Mhe. Burhan Saadat Haji alipokuwa Waziri nimefanya utafiti kulikuwa na afisa mmoja pale kwenye Idara ya Ardhi mtu wa *lease* alikuwa na mashaka sana, alitia hasara sana serikali baadae

akaondoshwa. Alipoingia Waziri mpya katika awamu hii huku waziri aliyekuwepo mwanzo alimuondosha kwa matatizo, ameitia hasara sana serikali kwa mikataba, kwa *lease* ambazo hazina maslahi ya umma aliondoshwa kwa muda wa miaka minane. Alipoingia Waziri mpya Mhe. Ali Juma Shamuhuna alimrejesha yeye mwenyewe watakuwa wanajijua huko, na tena akapewa lile lile eneo la *lease* ndio *speed* hii ya kesi za ardhi zikaongezeka. Tafsiri yake hii aliwekwa kwa ajili ya maslahi ya watu fulani.

Mhe. Spika, sitaki itaje jina lake lakini bila shaka mwenyewe anajijua na watendaji wa mamlaka hiyo watakuwa wanamjua, lakini tangu alipofika kwenye idara hii kesi za ardhi zimezidi. Sasa Mhe. Spika, najiuliza kwa nini tuwapatie fedha za maendeleo watu hawa, kwa nini tuwapatie fedha za matumizi ya kawaida hawa.

Mhe. Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kiwani naunga mkono kila ambaye amesema tuunde Kamati Teule na mimi binafsi nitakuwa sipitishi Bajeti hii kama Waziri hajakubali kuunda kamati teule. Tuunde Kamati Teule kwa ajili ya kumsaidia Rais.

Katika hili Mhe. Spika, naomba nipatiwe ufafanuzi kama kweli kauli ya Rais ni muhimu na kama kweli kauli ya Rais inasikilizwa Mhe. Waziri unambie. Mwanakwerekwe kuna *plot* Nam.139, *plot* 292 tayari zimeuzwa zinatolewa hivi karibuni na tayari watu wamejenga ukuta, wakati Rais tayari ametoa kauli kwamba jamani zuieni. Hivi Mhe. Spika nchi hii mkubwa nani? Kama si Rais anayeongoza nchi hii nani mkubwa? Rais anazungumza hadharani mbele ya umma watu huwa wanatoa hati. Sasa kwanza Mhe. Waziri nakuomba unambie *plot* Nam. 139, 292 tayari limejengwa ukuta maeneo ya Mwanakwerekwe kapewa nani hasa baada ya kauli ya Mhe. Rais kuzungumza.

Mhe. Spika, pia naomba Mhe. Waziri atusaidie katika bajeti iliyopita nilisema hapa kwamba tunakusudia kujenga nyumba kule Mwambe kwenye kiwanja cha Mkubwa, wasaidizi wangu wamenambia tayari jana wamepeleka mawe, nimeamua nijenge najua nitashitakiwa, lakini yatazuka mengi. Kwa nini mgeni apate eneo Mwambe mtu wa Mwambe asipate eneo Mwambe. Kwa hivyo, nimeamua nijenge pale nishtakiwe ili Mahkama ya Ardhi wataona sasa umuhimu wa kumjali mzalendo, wataona hati muhimu lazima apewe mzalendo, haiwezekani mgeni kupewa eka 14 kimya kimya wakati Wazanzibari wenyewe hawashirikishwi wala hawajui.

Mhe. Spika, nimeanza kupeleka mawe na ukinipa posho hapa napeleka mafundi na najenga *foundation*. Nina hakika nitashitakiwa lakini ndio

demokrasia lazima ujitolee kwa ajili ya maslahi ya wengi. Kwa hivyo napeleka mawe najenga kwa *speed foundation* baadae serikali itaamua.

Mhe. Spika, jengine ambalo ni muhimu sana mimi nilikwenda kwenye eneo moja nikashangaa sana, wizara hii ilimpelekea barua mwekezaji kwamba ameshindwa kulipa *lease* kwa busara kubwa mwekezaji akalipa *lease* ya kawaida na *penalty* yake. Tarehe 24/02/2010 alilipa US$ 5400 kama *lease* ya kawaida akalipa na *penalty* US$ 6000 na kidogo kwa jumla kwa mujibu wa risiti hii ya serikali amelipa *lease* hii kwa US$12 karibu na mia sita. La kushangaza Mhe. Spika, hii ni mwaka 2010, mwaka 2011 ninayo barua hapa ya Mhe. Ali Juma Shamuhuna ni waziri, tarehe 6/6/2011 mwaka mmoja baada ya kulipwa *lease* na matakwa yao jamaa kafutiwa ardhi. Hii sio hadithi nimekwenda mimi mwenyewe na Mhe. Hamza Hassan Juma mpaka kwenye *site*, sijaota, sijalewa na hata sigara sivuti.

Kwa hivyo, wewe unamwambia mwekezaji kwamba lipia *lease* na *penalty* amelipa baada ya miezi sita unamfutia nchi gani inafanya mambo hayo duniani. Mhe. Spika, Baraza hili lingetegemea baada ya kufutwa hii irejee serikalini, *Wallahi* naapa na mimi Muisilamu amechukua mtoto wa kiongozi, mimi ningetegemea tumemnyang'anya Mzungu hapa si pao kiasi tumnyang'anye basi irejee kwenye serikali, amepewa mtoto wa kiongozi. Ndani ya Wizara hii hii ya Maji hadi tutoe ile tume kwa nini tuwape fedha watu hawa, mtu yeyote ataepitisha fungu hili bila ya kuunda tume ya kumsaidia Mhe. Rais Mwakilishi huyo hafai, Mwakilishi yoyote nasema wazi wazi atakaetoa fungu la fedha wizara hii kuwapa watu namna hii watu ambao hata Rais hawamuheshimu huyo Mwakilishi hafai. Hatuwezi kila siku Rais kuzungumza tu, nyinyi mashahidi Mhe. Spika.

Juzi Kizimkazi Rais kwa mara ya mwanzo anapokelewa kwa mabango, tangu lini mambo hayo. Kwa hivyo, Mhe. Spika, nawasisitiza Wawakilishi wenzangu fungu hili anasimamia Katibu Mkuu fedha asipewe. Kwanza Mhe. Spika, mimi niseme wazi kabisa ana mafuta kuliko ya *OK* ya kupikia, kwa hivyo kwa nini tumpe fedha mtu mwenye mafuta.

Mhe. Spika, nikitoka hapo nimekwenda tena na Mhe. Hamza Nungwi kuna eneo lenye urefu wa mita 600 wamegawana watu wanne wala si wageni ni Wazanzibari viongozi, Rais anatoa kauli itekelezwe, haitekelezwi bwana.

Mhe. Spika, baada ya kutoka Nungwi nimekwenda Kendwa ndani ya Jimbo la Mhe. Naibu Waziri wa Wizara hii anajua kuna matatizo hasemi, sasa mimi nawasemea kwa nini mimi Mtumbatu nawasemea Watumbatu wenzangu. Watu wamechukua maeneo ndani ya makaburi, Mhe. Saleh Nassor Juma kule nyuma anawaita Koho, Koho hula maiti Mhe. Spika, mtu sasa anachukua

ardhi ndani ya makaburi, Mhe. Naibu waziri hasemi kitu, lakini yeye ni serikali hasemi, lakini mimi *back bencher* nasema kwamba watu wanaonewa.

Kwa mara ya mwanzo Mhe. Spika, nimeziona risasi ambazo zimepigwa kwa ajili ya mapambano ya wananchi na vikosi, mimi nilikuwa sijaziona risasi, niliziona risasi nne ambazo wananchi wenyewe wameziokota, kama watu wanatetea haki yao serikali inasema lazima tutumie nguvu hii nchi gani, Wazanzibari wende wapi, mambo haya yangefanywa Zimbabwe na nchi nyengine sio Zanzibar. Kwa hivyo, Mhe. Spika, tukibaini kwamba kuna viongozi kama mawaziri wanasaidia wawekezaji kutunyang'anya basi mara hii tutawataja, nasema wazi. Kama Naibu Waziri ameshirikiana na wawekezaji kufanya hujuma nitasema wazi kwamba huyu kafanya hujuma nafanya utafiti, kwa sababu alipoambiwa nakwenda aliwaambia msimwite Mhe. Hija Hassan, nimefika na nimepewa pweza kilo sita Mhe. Spika. Lakini tukibaini kwamba kweli unashirikiana na wawekezaji kufanya hujuma hii nitakutaja hadharani kwa sababu hii ndio demokrasia, si CCM si *CUF* hii haikubaliki. Mimi nimeambiwa tu kwamba kuna sentensi moja ya CCM kwamba ibeni nitanyamaza kimya, kama kuna sentensi moja ya CUF ibeni basi nitanyamaza kimya. Lakini hatuwezi kufanya mchezo huu Mhe. Spika.

Mhe. Spika, kwa kumalizia na kuheshimu muda wako najua unataka kumpa mtu mwengine na ninakuheshimu sana katika hili, naomba kusema kwamba Wawakilishi tafadhilini muna dhima, na Mtume (SAW) amesema kwamba *kila mmoja ni mchunga na kila mchunga ataulizwa alichokichunga mbele ya Mwenyezi Mungu,* fungu hili lizuiliwe lisipitishwe wala hatumuadhibu Babu Rama. Mhe. Rama ni mtu safi. (*Makofi*).

Nilikwambieni ni mtu na nimefanya utafiti tangu apewe wizara kuna ma-*files* zaidi ya 40 hajatia saini. Huu ni ushahidi kwamba yeye ni safi. Ma-*file* yapo juu ya meza na yeye atashangaa nimepata wapi habari hizi, nimefanya utafiti lakini anasema ninatulia ninafanya uchunguzi. Hii ni dalili ya usafi. Kwa hivyo hatumuadhibu Mhe. Waziri lakini lazima awaondoshe watu. Mhe. Spika, asipowaondosha yeye Wawakilishi watamuadhirisha, jambo ambalo si zuri katika utawala wa sheria.(*Makofi*).

Mhe. Spika, baada ya hayo siungi mkono hoja. (*Makofi*).

Mhe. Shawana Bukheit Hassan: Ahsante sana Mhe. Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijaalia kwa kunipa uwezo na afya nikaweza kusimama katika Baraza lako tukufu asubuhi ya leo.

La pili nikushukuru wewe mwenyewe kwa kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati inayohusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2012/13.

Tatu Mhe. Spika, nimpongeze Mhe. Waziri kwa hotuba yake, lakini pia nimpe pole kwa kazi ngumu na wizara nzito yenye majukumu mengi, lakini *inshaallah* Mwenyezi Mungu atamjaalia na kumsaidia.

Mhe. Spika, baada ya pongezi hizo nianze mchango wangu mimi katika Idara ya Ardhi. Mhe. Spika, suala hili la ardhi limekuwa ni tatizo kubwa katika nchi yetu. Kila anayesimama katika ukumbi huu analalamikia suala la ardhi. Kweli suala la ardhi ni suala zito kwa sababu suala hili kila Mjumbe anakuwa na malalamiko yake. Hata mapinduzi yetu kwenye suala moja lililochangia nchi yetu hii kufanya mapinduzi moja ni suala la ardhi.

Mhe. Spika, suala hili Mhe. Marehemu Mzee Abeid Karume alipotoa ardhi akawapa watu eka tatu, na kwa bahati nzuri ardhi ilianza kutolewa katika Jimbo la Dole kwenye Shehia ya Dole. Lakini pamoja na kuitoa ardhi katika maeneo mengi tu na kuanzia hapo Dole, lakini aliacha maeneo mengine yafanye shughuli nyengine na watu wafanye shughuli zao za kilimo wajipatie riziki. Alifanya hivyo kwa makusudi kwa kujua kuwa ardhi hata tukikatiana sote hatuwezi kuenea.

La kusikitisha Mhe. Spika, hivi sasa hali tunayokwenda nayo haitaki kuonekana ibaki tupu. Kila mahali ambapo pana ardhi ya serikali ipo wazi basi hapo wataingia watu wakatiane maeneo wachukue, watu waliokuwa katika maeneo yale ambao ni maskini wa Mungu ndio wanaoishi wakapata rizki wao na watoto wao, lakini matokeo yake ardhi ile yote itakatwakatwa wagawane watu.

Hivi tunategemea hawa wananchi wetu tunaokwenda nao kila siku na shida hizi na zile wakati ikifika iwe hivi. Leo ardhi yote tunawanyang'anya tunagawana sisi, hivi tunategemea wananchi hawa waishi katika mazingira gani.

Mhe. Spika, mimi ninadhani tufike wakati sasa masuala tena ya kugawana ardhi hebu tuyaangalie upya na ikiwezekana sisi ambao tunapata rizki pia kwa maeneo mengine, na tushapata tulichopata kama eka tatu au sita, tuache tena jamani, mtu anachukua eka 18, 20, au 30, huu utaratibu unatoka wapi. Hawa wananchi wetu wataishi vipi.

Mhe. Spika, hili ni tatizo na utaona kila mmoja analizungumza na kila mmoja analirudia, kwa sababu ni suala ambalo linatia uchungu. Tukienda katika vijiji vyetu linakuwa ni tatizo kubwa na zito.

Mhe. Spika, ninachoomba kwa kuwa hili suala hivi sasa Mhe. Waziri alitazame kwa nguvu zake zote, na ikiwezekana ayaangalie yale maeneo yote, na akipata nafasi tumchukue na kutembeza katika maeneo yetu aone hali halisi ilivyo.

Mhe. Spika, pia kuna tatizo hili la kuonekana kuwa uchelewaji wa hati umekuwa kama tatizo sugu. Kwa hivyo mimi ningelimuomba Mhe. Waziri ajitahidi kadri ya uwezo wake kama alivyoeleza katika kitabu chake, hizo taratibu anazoziandaa hivi sasa za kupatiwa watu hati kwa haraka wapatiwe, wakiwemo na wananchi wa Dole katika kijiji cha Kijichi.

Maana yake pale kuna wenzetu wakubwa walipatiwa maeneo yale haraka haraka hati ikapatikana, lakini hawa ambao waliochukuliwa maeneo yao mpaka ikafikia na wao wapewe maeneo badala ya yale waliyokuwa wakulima, lakini hadi hii leo mwaka wa pili hawajapata hati miliki, hawajui wafanye nini, kule walikokuwa wakilima maeneo yameshachukuliwa na eneo ambalo hivi sasa wamepewa hati hawajapata wanasuasua tatizo limekuwa kubwa.

Mhe. Spika, ningeomba hili na ingewezekana pia kama una uwezo wa kunieleza kuwa watapatiwa lini hati hizi, si vibaya ili na wao wakawa na moyo wa imani zaidi katika nchi yao.

Mhe. Spika, katika suala hilo hilo la ardhi ningelimuomba Mhe. Waziri hebu atusaidie kutupatia taarifa ya agizo alilolitoa Mhe. Rais waliosababisha matatizo wakaambiwa wamalize, lakini hebu atusaidie kutwambia ni mangapi yamepatikana ufumbuzi mpaka hatua hii. Ningeliomba sana hilo Mhe. Spika.

Jengine Mhe. Spika, tunaomba katika eneo hilo hilo la Kijichi, eneo lililobakia kama nilivyokwishasema wakishapewa hao waliopewa, eneo lilibakia watu kugawiana tena iwe basi, liachiwe watu walime.

Mhe. Spika, nikiendelea niende ukurasa wa 42 kuhusu Mamlaka ya Maji. Mimi niipongeze serikali na wizara kwa jumla kwa jitihada wanazofanya. Lakini Mhe. Spika, bado mimi ninapata mshangao na tatizo kwa kuona jitihada zote hizi zinazofanywa lakini hazileti matunda, tatizo ni nini. Kuna mdudu gani huku Mamlaka ya Maji.

Visima kila siku vinachimbwa lakini kila vinapochimbwa visima lakini matokeo yake hatupati ile faida hasa ya kuona, kwa kuwa visima hivi vilivyochimbwa basi mafanikio yake ni haya. Mwanzo tulipoambiwa vinachimbwa vile visima kwa ajili ya Mkoa wa Mjini/Magharibi, na kwa bahati nzuri visima hivyo vilichimbwa ndani ya jimbo langu. Wamechimba Kizimbani, Kianga, Kinuni mote humo mumechimbwa visima lakini matokeo yake hatuoni hasa ile tija ya visima hivi.

Lakini pia tunaambiwa miundombinu nayo imeleta matatizo. Sasa hebu tuambiwe hasa, kama visima vimechimbwa miundombinu ina matatizo, ni hatua gani mpaka sasa hivi ni maeneo mangapi ambayo miundombinu imeshatengenezwa basi angalau watu wawe na tama kuona kwa kuwa hivi visima vilivyochimbwa katika miundombinu iliyoharibika eneo fulani na fulani mpaka sasa hivi limetupa matumaini.

Mhe. Spika, tungeomba sana hili Mhe. Waziri atusaidie ili wananchi wetu wapate moyo na tamaa kuweza kuamini kuwa serikali yao na nchi inapata kufaidika na lile ambalo tatizo wanalo.

Mhe. Spika, pia ningeomba Mhe. Waziri akija hili anisaidie. Sisi katika jimbo letu kama nilivyosema tuna visima vingi sana, na tuliambiwa visima hivi pamoja na kufaidika na maeneo mengine lakini na ndani ya jimbo letu tutafaidika. Kwa mfano visima vilivyochimbwa Kianga. Tuliambiwa kuwa maji yale yatakwenda mpaka Welezo, yakishafika Welezo vijiji vitakavyofaidika ni kijiji cha Kinuni, Kimara, Msikiti Mzuri pamoja na Gudini.

Lakini mpaka hivi sasa vijiji vilivyofaidika ni viwili tu. Vijiji hivyo ni Kimara na Kinuni. Jee lini Msikitini Mzuri na Gudini ambao vipo nyuma ya kituo cha Polisi cha Mwera itaweza kufika huduma hiyo ya maji. Ningeomba nalo atusaidie atakapokuja kutupatia majibu.

Jengine Mhe. Spika, tuliambiwa kisima ambacho kimechimbwa Kizimbani kitasaidia kijiji hicho, Masingini na Mtofaani bondeni. Lakini mpaka hadi hii leo hatujaona hatua yoyote ambayo imesaidia. Tumeambiwa kuwa ipo *valve* ya kwenda Kizimbani kule, lakini hatujui hatua gani hivi sasa inaendelea. Masingini ndio *akhasi*, Mtofaani nako ndio halikadhalika.

Kwa hivyo ningeomba sana Mhe. Spika, Mhe. Waziri atusaidie hili pia na kijiji cha Kipange kiliambiwa kitafaidika na kisima hiki. Lakini pia katika kisima kilichochimbwa Kianga tuliambiwa pia na kijiji kimoja ambacho kipo katika eneo la kati kati baina ya Kianga na Dole, nacho kiliambiwa

kitafaidika. Kwa hivyo nacho tungeambiwa ni lini nao wataweza kufaidika na maji hayo.

Mhe. Spika, nikiendelea niende kwenye ukurasa wa 55 katika Shirika la Umeme. Mhe. Spika, shirika hili mimi nichukue nafasi hii ya kuwapongeza kwa dhati kabisa kwa kweli wametimiza uungwana kwa mara hii, wameweza kutimiza ile ahadi ya Rais ya kututilia umeme katika Skuli ya Kianga na kijiji cha Kianga ambapo *transformer* ilikuwa imeekwa mahali ambapo sio pazuri, lakini *transformer* hiyo hivi sasa imeshaondolewa imeletwa katika kijiji, na sasa hivi umeme umesambaa. Ningeomba tu hatua zilizobakia wamalizie.

Lakini Mhe. Spika, baada ya pongezi hizo pia ningeomba yale maeneo ambayo tulichangia Wabunge na Wawakilishi wa Jimbo la Mfenesini na Dole, zikapatikana karibuni shilingi milioni 25 ili kuweza kutiliwa umeme katika eneo la Mndo uweze kusambaa Mndo Mapinduzi na Mkanyageni na maeneo mengine. Basi tungeliomba sana kwa kuwa hii kazi iongezeke *speed* kidogo kwa sababu watu wale wamevumilia muda mrefu, kipindi kirefu, awamu kwa awamu zinakwenda hawajafaidika na huduma hii ya umeme. Kwa hivyo ningeomba sana madhali fedha tumetoa na zimebaki ni chache, na ule mchango wao ambao waliosema tuchangie ili huduma iweze kuwafikia wale tuliowakusudia.

Mhe. Spika, pia katika kijiji cha Kwagoa Bumbwisudi tumechangia hapo jimbo letu Mbunge na Mwakilishi shilingi milioni 21 tumeshazitoa, lakini pia nayo huduma hii katika kufikisha umeme huo umekuwa nzito. Kwa hivyo madhali fedha tushatoa basi wenzetu wajitahidi nao ili wale tuliowakusudia waweze kufaidika na jambo ambalo tumewapangia.

Mhe. Spika, jengine ni kuhusu suala la nguzo ambazo tulitia katika kijiji cha Kiwambangoma, Bumbwisudi na Kagera kiliopo Mwera. Walitwambia watu wa shirika kwa kuwa nguzo hizi kwa sasa hivi hazifai, sio nzuri lakini tutakubadilishieni hizi nguzo, kwa hivyo tunaomba kama ahadi yao walivyoahidi ya mwaka jana ya kuwa watatusaidia pale tunapojisaidia. Kwa hivyo sisi tushajisaidia na wametwambia kuwa nguzo hazifai, hivyo tunawaomba waje watutilie zile na kutubadilishia zile nguzo na sisi wenyewe halikadhalika tutajitahidi kuweza kusaidiana kuona masuala ya waya tunafanyaje. Lakini nguzo tunaomba waje watutilie kwa sababu ni muda mrefu na wao suala hili halijaweza kupatikana.

Mhe. Spika, kwa kumalizia ukurasa wa 60 kuna jadweli ya vijiji vilivyoambiwa vimeungiwa umeme. Sasa katika kuangalia nimeona kwa kuwa pamoja na nguvu za wananchi na shirika limesaidia. Sasa ningeliomba

Bumbwisudi na Dole wametusaidia kiasi gani katika hizi fedha ambazo walizosema wao wamechangia.

Mhe. Spika, kwa kuheshimu muda wako ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ijapokuwa hii chache kuweza na mimi kutoa mchango wangu, isipokuwa ninamuomba Mhe. Waziri ajitahidi na Mwenyezi Mungu atamsaidia, na sisi matatizo yetu yakazidi tutakwenda katika wizara yake na tungeomba sana atupe mashirikiano na sisi tutampa mashirikiano ili tuweze kufanikiwa.

Baada ya hayo ninashukuru tena kwa mara nyengine, na ninataka rasmi kwa kuwa mimi hotuba hii ninaikubali asilimia mia moja. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Farida Amour Mohamed: Ninakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii na mimi nikachangia machache katika hotuba hii ya Waziri wa Ardhi, Maji, Makaazi na Nishati.

Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha kusimama hapa nikiwa na afya njema. Nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake jinsi alivyoichambua hotuba yake hii makini.

Lakini pia nimpe pole Mhe. Waziri kutokana na mzigo mkubwa aliotwikwa wa wizara hii iliyobeba maisha ya Wazanzibari, lakini Mwenyezi Mungu atakusaidia *inshaallah*.

Mhe. Spika, mimi ninataka nianze moja kwa moja kwenye Mamlaka ya Maji. Mhe. Spika, *maji ni uhai*. Maji ni kila kitu kwenye maisha ya binadamu. Mhe. Spika, naomba unisamehe hili ambalo ninalotaka kulisema, kwa sababu katika Kanuni zetu haziruhusu kurudiarudia lakini jambo lolote ambalo kuwa ni tatizo basi litazungumzwa na kila mtu mpaka liondoke tatizo hilo. Kwa hivyo maji ni tatizo bado.

Maji ni tatizo hasa katika maeneo ya vijijini na maji yakiwa ni matatizo hata mfumo wetu wa maisha wa kutafuta maendeleo ndani ya nchi unakosekana. Kwa nini niseme hivyo? Katika hili wanawake ndio tunaopata idhilali kubwa katika kutafuta maji. Tuwaonee huruma wanawake katika vijiji vyetu. Wanawake wanaondoka asubuhi kwenda kufuatilia maji masafa marefu na vilima kwa kukosa maji ya mfereji safi na salama, ambayo Mhe. Rais katika hotuba yake alilithibitisha hili kama maji safi na salama ni kipaumbele katika nchi yetu, lakini kwa bahati mbaya baada ya kupata maji tunapata idhlali ya maji.

Kwa hivyo Mhe. Waziri ninakuomba sana katika hili uwaonee huruma wanawake katika kutafuta maji, kwa sababu katika watu waliohamasisha na kuhamasika kwenye kujiendesha kwa kujikwamua kimaisha ni wanawake. Lakini hawawezi kujikwamua kwa kukosa maji.

Maji yana ma-group mengi. Kuna maji ya matumizi ya nyumbani. Kuna maji pia ya kuendeshea angalau biashara zao ndogo ndogo za vikundi vyao. Akinamama wana vikundi vyao vya ushirika vya mboga ili kujikwamua na kuwapa wepesi akinababa katika maisha. Lakini hili linashindikana kwa kukosekana maji ndani ya maeneo.

Kwa hivyo Mhe. Waziri ninakuomba sana katika vijiji vilivyokuwa vinakosa maji na ninataka niunge mkono hotuba ya Mhe. Mjumbe Mhe. Salim Abdalla kutoka Jimbo la Mtambwe, vijiji vyote vile alivyovizungumzia Mheshimiwa havina maji, na Mhe. Spika, kwa taarifa yako ukitembelea katika maeneo haya, kama ni kipindi cha sala unaona huruma hata kumwambia mtu ya kutilia udhu kutokana na shida ya maji waliyokuwa nayo.

Mhe. Spika, katika viambatanisho vyake kwenye hotuba yake kuna maeneo mengi kaeleza jinsi ya safari za nje na ndani za wafanyakazi wetu kwa kwenda kusoma, safari za muda mrefu na muda mfupi na za kila pahala. Sasa kimtazamo wangu na imani yangu mimi ninavyojua, safari zile ni za kimasomo si safari za kutembea na kutembea pia ni kusoma.

Sasa wale wenzetu fedha nyingi zinazotumika za serikali kwa safari zile, tunataka matunda yake tuyaone hapa. Kwa sababu serikali kila siku inapiga kelele, tumenunua mashine ya maji, mabomba ya maji lakini sasa tatizo ni nini ikawa maji hayapatikani na watu kila leo wanapewa fursa za kwenda kusoma, na ukisoma ndio unaona kule unakokwenda, unatembea na kuona jinsi ya wenzetu wanavyokwenda na kuendesha maisha. Hili Mhe. Waziri nakuomba sana ulichukulie kwa sababu sisi tunapitisha bajeti hapa, vifungu wanatoka kwenda kusoma, wanatoka kwenda kutembea na ndio kusoma kwenyewe, lakini faida yake inakuwa ni ndogo kuliko ile hasara tunayoitoa. (*Makofi*).

Mhe. Spika, maji haya haya yanakuja katika mambo mengine. Katika maji haya kuna watu wale wachache wadogo kwa matumizi ya nyumbani, vijiji hivyo vilivyokuwa maji yanapatikana wanalipia shilingi elfu mbili kwa mwezi. Cha kusikitisha watu wale wanaolipia shilingi elfu mbili kwa mwezi wakichelewa miezi mitatu tu hawajalipa basi wanakatiwa ule mfereji au wanafungiwa maji.

Lakini sasa katika kutembelea kwetu kwenye taasisi mbali mbali za serikali kamati zako za Baraza la Wawakilishi Mhe. Spika, tunagundua madeni makubwa mno yanayodaiwa baina ya taasisi na taasisi. Tunapopitisha bajeti zetu tunapitisha kila taasisi kifungu cha maji na umeme. Sasa inakuwaje malipo yale ikawa hayalipwi na hawakatiwi lakini wanaokatiwa ni watumiaji wadogo wadogo. Inauma sana Mhe. Spika. Naomba sana taasisi zinazodaiwa zilipe kama tunavyopitisha vifungu vya maji hapa na wao walipe Mhe. Spika. (*Makofi*).

Mhe. Spika, baada ya kutoka hapo kwenye maji naomba niingie kidogo katika Idara ya Nyumba. Mhe. Spika, katika idara hii kuna mambo muhimu. Kwanza tumpongeze sana na kumshukuru kwa dhati kabisa Marehemu muasisi wetu Rais wa Zanzibar Marehemu Abeid Amani Karume kwa kuwajengea Wazanzibari nyumba za kuishi.

Sasa cha kusikitisha nyumba zile zimejengwa kwa muda mrefu kwa nia safi, lakini baada ya kuondoka yeye hapa duniani, ile imani yake kwetu tunaidharau tunaifanya haina maana na hilo halifai Mhe. Spika.

Sasa nyumba hizi zina mambo mawili na matatu. Kwanza utunzaji wake. Nyumba zile ni dhaifu, mbovu, zinatisha, hata kupanda zile ngazi zake nyengine basi unaziogopa, unaona mimi nikipanda tu nitaanguka. Katika bajeti hapa pia hukuta kuna sehemu matengenezo madogo madogo ya nyumba, zile nyumba bado hazijafanyiwa matengenezo.

Ukienda ndani ya Wilaya yangu ya Wete katika nyumba zile za majumba makubwa pale Mtemani ni hatari kuzipanda juu zile nyumba, utaona sasa hivi utaanguka. Kwa hivyo Mhe. Waziri ninakuomba sana katika hili, kama umeamua kuzifanyia matengenezo kwa kuenzi maneno ya mzee wetu na imani yake aliyoifanya kwetu, basi zifanyiwe matengenezo ya kweli, sio zichukuliwe pesa ziende zikapakwe rangi, pagongwe pahala pabovu, halafu ionekane imetengenezwa, hiyo itakuwa bado haijatengenezwa Mhe. Spika.

Halafu Mhe. Spika, katika nyumba hizo hizo kuna kodi za watu. Zile nyumba kuna wanalipia kodi, lakini umiliki wa zile nyumba Mhe. Spika, aliyekabidhiwa mwanzo katika nyumba zile pengine kauza, kakodisha. Yeye alipewa nyumba ile kwa shilingi elfu tisa, kampa mtu kwa shilingi laki mbili, sasa inakwenda zaidi ya mikono miwili au mitatu au minne. Sasa yule mdhibiti aliyepewa mwanzo ile nyumba anakosekana.

Sasa ile si haki. Yule aliyekabidhiwa nyumba ile anatakiwa yeye mwenyewe awe nayo kwa sababu zile nyumba hazikupewa kuwa ni biashara, yeye ampe huyu na yule. Matokeo yake ni kukosekana hata kwa ile kodi yenyewe, ule

ukusanyaji wa kodi unakuwa mgumu kwa sababu ukienda wewe unamtafuta fulani unaambiwa hapa hayupo. Sasa hilo ni tatizo Mhe. Spika. Naomba sana Mhe. Waziri afuatilie kikamilifu jinsi ya watu waliopewa nyumba zile ni nani na nani anayezisimamia mpaka sasa.

Mhe. Spika, katika udhibiti huo huo usimamizi wa nyumba hizo lazima zisimamiwe vizuri ipasavyo. Ingawaje kuna tume imeundwa na tume ile ninafikiri karibu ni mwaka wa pili sasa ya kufuatilia nyumba zile, wengine ndio wanagoma kulipa wanasema wao wamepewa na Marehemu Mzee Abeid Karume, sasa inaonekana mpaka leo utendaji ule umekuwa ni mdogo na hauonekani jibu lake. Halafu la kusikitisha zaidi nyumba zile zilijengwa kwa ajili ya kuwapa watu maskini, lakini cha kusikitisha Mhe. Spika, nyumba zile waliopewa ni matajiri, ni watu wenye pesa zao, wale maskini hawana pa kuishi lakini wale wanaokaa ndani ya nyumba zile ni wale wale, na ni viongozi wakubwa wanaonekana ndani ya nyumba zile. Hilo linasikitisha si vizuri jamani, tuwaonee huruma wananchi wetu wa chini Wazanzibari waliokuwa hawana hata pa kuishi, sio kung'ang'ania sisi kila kitu Mhe. Spika.

Nikitoka hapo Mhe. Spika, naomba niingie kidogo katika Idara ya Ardhi. Kila aliyesimama hapa keshalalamika sana kuhusu mambo ya ardhi. Mhe. Spika, Mhe. Waziri mbali ya kukupa pole na kukwambia una mzigo mzito uliopewa, na mzigo utaanza duniani mpaka kesho mbele ya haki, Mwenyezi Mungu asikufikishe huko, uweze mzigo huu utatue hapa hapa.

Mhe. Spika, suala la ardhi limekuwa sugu ndani ya nchi yetu. Suala hili limekuwa gumu sana. Wanawake wenzetu walikuwa na maeneo ya ardhi wanayotumia kwa ajili ya kilimo kujipatia rizki, anakuja mkubwa fulani mwenye uwezo wake anawanyang'anya. Jamani tunakwenda wapi ndani ya nchi hii.

Nani atatuhurumia kama si nyinyi viongozi wetu Mhe. Spika. Hivyo naomba sana Mhe. Waziri atakapokuja hapa atufafanulie vizuri nani mwenye kudhibiti hasa aliyekuwa na uwezo wa kupewa hii ardhi, na nani mwenye kunyang'anya, na mwenye kunyang'anya ardhi hii atapewa adhabu gani.

Mhe. Spika, kwa vile wenzangu wameshazungumza mambo mengi kuhusu haya haya yaliomo kwenye hotuba hii, kwenye Shirika la Umeme mimi sisemi kitu kwa sababu mimi mwenyewe ni Mjumbe wa Kamati ya PAC, ninafikiri ripoti yake itakapokuja yamo mengi na yataonekana *inshaallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu, lakini ninasisitiza tena Mhe. Waziri matatizo ya ardhi na migogoro ya ardhi utusadie sana Wazanzibari.

Ahsante nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nilikuwa ninapenda sana kila Mjumbe apate nafasi ya kutoa mchango kama alivyoomba Mhe. Waziri baada ya kusoma bajeti yake, ili hatimae tupate ufafanuzi kutoka kwake Mhe. Waziri ili tuweze kupitisha baadae kwa kadri itakavyoonekana inafaa vifungu vya wizara hii.

Wachangiaji wamekuwa wengi. Nilifikiri tungeweza angalau kumi na mbili au kumi na tano lakini haikuwezekana. Kwa hivyo niwaombe radhi Waheshimiwa Wajumbe kwa sababu tupo nyuma sana ya ratiba yetu, wengine hatutopata nafasi. Kwa hivyo kama kuna utaratibu wa kuweza kutoa michango kwa maandishi kwa Mhe. Waziri basi niombe sana wafanye hivyo.

Wajumbe ambao kwa muda ulivyo, watakosa nafasi ni pamoja na Mhe. Rufai Said Rufai, namuomba radhi sana, Mhe. Abdi Mosi Kombo nakuomba radhi sana, Mhe. Abdalla Juma Abdalla maulana nakuomba radhi sana, Mhe. Ussi Jecha Simai hayupo, lakini Mhe. Saleh Nassor Juma *Wallah* nakuomba radhi sana ili upate nafasi ya kumpelekea kwa maandishi mchango wako. Vile vile Mhe. Hassan Hamad Omar nakuomba radhi, Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi hivi sasa hayupo lakini pia namuomba radhi, Mhe. Viwe nilikuwa namtafuta sana nimpe muda japo mdogo kwa sababu hajachangia sana bajeti mbali mbali lakini kwa bahati mbaya hayupo pia namuomba radhi. Pia Mhe. Mussa Ali Hassan mheshimiwa wangu nakuomba radhi.

Sasa basi baada ya maelezo hayo nawaomba Waheshimiwa Wajumbe tuwasikilize upande wa serikali. Kwanza nimuombe Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, halafu baadae Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, naomba nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii na mimi niweze kuchangia kidogo katika hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Mhe. Spika, mchango wangu utakuwa zaidi katika suala la Mahakama ya Ardhi. Kuna Waheshimiwa Wajumbe wengi walizungumzia suala hili la Mahakama ya Ardhi, lakini zaidi ni Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Mohamed Haji na Mhe. Bi Mgeni na wao walichangia kwa kina zaidi.

Mhe. Spika, naomba niseme yafuatayo, kwamba Mahakama ya Ardhi ni kweli kwamba ni mahakama ambayo iko katika Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Lakini Mahakimu ambao wanaiendesha mahakama hiyo, wanatoka katika mahakama zetu. Tuna matatizo kweli katika Mahakama ya Ardhi, lakini matatizo haya Mhe. Spika, tumejaribu sana kuyapunguza na kuyatatua.

Kwanza kesi za mahakama hii ni nyingi, sio kama zile alizosema Mhe. Mohamed Haji, kesi zile ni kwa mwaka huu tu. Lakini tulikuwa tuna kesi nyingi katika kipindi cha miaka ya nyuma. Kesi hizo kwa sababu ya umuhimu wake ndio ikatubidi tuongeze mahakama. Kwa hapa naomba kumueleza Mhe. Bi Mgeni kwamba yeye alisema kwamba kila wilaya tuwe na mahakama kama hii.

Mhe. Spika, hivi sasa tuna mahakama nne za ardhi, ingawa moja haijafanyakazi vizuri kwa sababu bado kidogo tunaikamilisha. Kuna Mahakama ya Ardhi ambayo iko Mjini Magharibi, kuna Mahakama ya Ardhi ambayo iko Kaskazini 'A' Gamba, kuna Mahakama ya Ardhi ambayo iko Wete na Mahakama ya Ardhi ambayo iko Chake Chake. Tumechagua maeneo hayo kwa sababu hayo ndio maeneo muhimu na ni maeneo ambayo kesi nyingi za ardhi zinakuwepo. Tulipata matatizo kidogo pia kwa sababu ya mahakimu.

Mwanzo Mhe. Spika, tulikuwa na mahakimu wawili, lakini kutokana na wingi wa kesi hizi tukateuwa mahakimu wengine wawili na hivi sasa tuna mahakimu wanne katika mahakama hizi.

Hakimu mmoja yuko Chake Chake, hakimu mmoja yuko Wete, mahakimu wawili wako Mjini Magharibi, kwa sababu ile mahakama ya Gamba bado kidogo kuanza kazi hasa, lakini baadae tutaipatia hakimu wake. Katika kesi hizi mahakimu hawa Mhe. Spika, tuliwasisitiza kwamba kesi ambazo lazima wazipe umuhimu wa mwanzo ni kesi zile ambazo ni za nyuma sana na tunafuraha kusema kwamba angalau kwa kiwango kikubwa kidogo, kwamba zile kesi za nyuma nyingi zimemalizika, ingawa bado nyengine zipo.

Kwa hivyo ndio maana Mhe. Mohamed Haji alipozungumza kwamba kesi za Pemba 80 zimeshughulikiwa na Unguja kesi 15, lakini sio hizo tu ni kwa sababu ya zile kesi za nyuma ambazo zilikuwa ni nyingi mno sana, na kesi zile takriban zilikuwa ni kesi 300, na hizi karibu nyingi zimeanza kushughulikiwa na kumalizwa. Kwa hivyo, Mhe. Spika, hilo ni tatizo moja ambalo nilisema nilizungumze.

Lakini la pili, kwa nini hizi kesi zikachukua muda mrefu kuna sababu nyingi. Kwanza matatizo tuliyonayo ni ya mashahidi. Mashahidi wengi Mhe. Spika, wanapoitwa katika kesi hizi huwa hawaendi kwa sababu ni kesi zinazohusiana na mipaka, wakati mwengine zinazohusiana na mali kuhaulisha mali. Matatizo ya watu wetu Mhe. Spika, unayajua, wako sana katika masuala ya dini. Sasa mtu ukimwita kwenda kutoa ushahidi, analeta mambo mengi ambayo kama hatukupata ushahidi basi mahakimu wetu nao haiwezekani

kutoa maamuzi. Kwa hivyo, hii ndio sababu moja kubwa ambayo mashahidi wanatucheleweshea katika kesi hizi.

Suala la pili ni la mahakimu, nao ni kutokana na kesi nyingi mawakili hawa hawa hasa Pemba, mawakili lazima watoke Unguja wengi. Kwa hivyo, kutokana na hayo mawakili huwa hawafiki kwa wakati uliopangwa, na mara nyingi hupelekea kesi hizi ziakhirishwe. Lakini hata hivyo tunajitahidi Mhe. Spika, kwamba kesi hizi nazo tuzipe umuhimu wa mwanzo.

Suala la tatu Mhe. Spika, hakimu ambaye tulikuwa naye tulikuwa naye Mjini Magharibi, bahati, sisemi bahati mbaya, lakini hakimu wetu mmoja wa kesi hizi ni mwanamke na matatizo ya wanawake tunajua katika suala zima la uzazi. Wakati hakimu huyo alipokuwa mjamzito, kila mara ni lazima achukue mapumziko, kwa hivyo kesi ni lazima uziakhirishe na baada ya kujifungua na kupata salama, kuna likizo la uzazi ambayo sina uhakika kama hivi sasa amesharudi. Lakini pia hii nayo inachukua muda mkubwa wa kwamba kesi hizi zinaakhirishwa na ndio maana utaona kwamba hapa kesi za Unguja kidogo ziko nyingi kutokana na tatizo hilo.

Kwa vyovyote vile Mhe. Spika, ni kwamba kweli kesi za ardhi ni nyingi tumeziona na hivi sasa tunasubiri mambo haya ya bajeti yamalizike ili tuweze kuongeza mahakimu ambao *specifically* watashughulikia kesi hizi. Mbali na hawa wanne ambao wapo hivi sasa, lakini nia hiyo ya kuongeza mahakimu ipo na hiyo tutaitekeleza kwa kadiri inavyowezekana.

Mhe. Spika, hili suala la Gamba nalo tunalishughulikia. Gamba pale Mhe. Spika, unajua utaratibu wa mahakama ni lazima kuwe na utaratibu wake, vyumba vile vya kujenga na nini. Hilo tumejitahidi na hatua ambayo tumefika ni kubwa na naamini katika kipindi hiki kinachofuata tukijaaliwa baada ya kukamilika haya, basi suala lile la kuanzisha mahakama pale tunaweza tukalianzisha katika kipindi hiki kinachofuata.

Katika Wilaya nyengine Mhe. Spika, kidogo itakuwa ni tatizo, kwa sababu inategemea uanzishaji wa mahakama. Ni lazima uanzishe mahakama ambapo utapata kesi, huwezi tu kuanzisha mahakama kiwilaya wakati kesi zinazokwenda ni mbili au tatu kwa miezi mitatu au miezi minne. Kwa kweli pale itakuwa hatuwatumii mahakimu ipasavyo.

La mwisho ambalo napenda niseme Mhe. Spika, ni kwamba pale Pemba hasa Wete napo pana matatizo kidogo, ambayo na haya tumeshayaona. Kwa sababu hakimu aliyepo pale, tumempa majukumu mawili. Kwanza ni kushughulika na kesi za kawaida na pili ni kushughulika na kesi za ardhi. Kwa hivyo, ana mzigo mkubwa, kwa hivyo hili tumeshaliona na hivi sasa

tuko katika matayarisho angalau tukianza katika kipindi cha mwaka huu mpya wa fedha, huyo hakimu ambaye anashughulikia kesi za kawaida basi tumuache katika eneo hili hili la kesi za kawaida, na tumpate hakimu mwengine na yeye ashughulikie kesi zinazohusiana na kesi za ardhi.

Kwa hivyo, kwa ujumla Mhe. Spika, napenda niseme kwamba suala hili ni kweli lipo, lakini tumejitahidi kulipunguza na mwaka huu wa fedha unaoanza tukijaaliwa tutaendelea kulipunguza kwa kutafuta mahakimu, ili kuongeza uzito katika maeneo hayo ambayo Waheshimiwa Wawakilishi wamesema.

Mhe. Spika, cha kusisitiza ni kwamba sio kesi hizi tu ambazo amezitaja Mhe. Mohammed 188, lakini ajue tu kuwa kulikuwa kuna kesi nyingi zinazofika 300 za ardhi, na hizo tumejitahidi kwa kuwataka mahakimu wasikilize kesi hizi tu na kuwapa kipaumbele wadau ambao wanahusika na kesi hizo. Hayo yamefanyika na ndio maana kesi hizo zikapungua mpaka kufika 188 na tutajitahidi Mhe. Spika, kama iwezekanavyo ili tuweze kuzipunguza, kwa kadri inavyowezekana.

Baada ya hayo Mhe. Spika, napenda nimpongeze Mhe. Waziri kwa maelezo yake na hotuba yake na *challenges* ambazo anazipata, lakini naamini kwamba Mhe. Waziri ni mtendaji mzuri na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atamjaalia kheri. Baada ya hayo napenda kuunga mkono hoja. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria. Nafasi ya mwisho kwa kipindi hiki naomba nimkaribishe sasa Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, kwanza baada ya kukushukuru kwa kunipa na mimi fursa ya kuchangia na mimi niseme wengi wamempa pole Mhe. Waziri, lakini mimi nimpe pongezi, kwa sababu najua kapewa mzigo huu anajulikana kwamba yeye ni hodari katika sekta zote za matunda ya mapinduzi. Kwa hivyo, na hili kapewa moja la elimu na sasa hivi akaonekana apewe mengine manne sijui matano haya, na mimi namuamini sina wasi wasi naye kwamba anaweza akayatekeleza.

Mhe. Spika, kwa sababu ya muda nilikuwa naomba nichangie katika maeneo matatu tu madogo. Eneo la kwanza ni suala la maji. Niliwasikia Waheshimiwa Wajumbe wengi wamezungumza kuhusu suala la maji, lakini tulilizungumza sana katika ugawaji wa maji. Lakini naomba kutanabahisha kwamba maji yatagaiwa baada ya kuzalishwa. Hata yakigaiwa kama hatukuyatumia vizuri hata yakiwa mengi namna gani hayatotosha. Kwa hivyo, mimi nilisema nichukue fursa hii kuwatanabahisha Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wa Baraza la Wawakilishi, lakini na pia wananchi kwa jumla.

Mhe. Spika, nasema hili kwa sababu ya uzoefu nilioupata tokea wakati wa utoto, wakati tunasoma pale Wete kwa Maalim Rashid Chuo cha Mbuyuni. Wakati wa kutia udhu alikuwa ana kipimo kwamba haturuhusiwi kutia udhu kwa maji ya zaidi ya kibaba kimoja. Yaani alichokuwa anasisitiza ni kwamba tusifanye israfu ya matumizi ya maji hata katika jambo la ibada. Yeye alikuwa na kipimo ni kopo, lakini kwa sababu ya pengine utoto hatukufahamu maana yake, lakini alikuwa anatumia msemo wa kwamba usitie udhu kwa maji zaidi ya kibaba kimoja. Pia tulikuwa haturuhusiwi kutia udhu katika ile mifereji, ni lazima ukinge kwenye kopo ukae pembeni utie udhu. Wakati ule Wete Bubujiko maji yalikuwa mengi, Gawani yalikuwa tele. Maji kutoka Masipa nadhani yalikuwa yakijaza matangi ya Semani bila ya wasi wasi, kwa miaka hiyo ya mwanzoni mwa miaka ya 1970. Mhe. Spika, lakini sijui wachache tunaokumbuka kutanabahishana matumizi ya maji bila ya israfu katika wakati huu.

Mhe. Spika, hapo nyuma tuna Msikiti wetu. Leo nadhani yale madoo mawili yanayowekwa yanatosha kutia udhi kwa watu wengi tunaokwenda pale. Lakini Mhe. Spika, kesho ukiweka mfereji yakiwa yanatoka kwenye mfereji, basi tutatumia mara 20 ya yale ambayo tunatumia sasa hivi. Sasa nilikuwa naomba kwamba tutanabahishane katika hili, maana hata katika ibada tunatumia maji mengi, lakini huko ndio tumesisitizwa tusiwe na israfu katika matumizi ya maji ambalo ni jambo muhimu sana.

Mhe. Spika, kuna baadhi ya nchi nyengine wanafanya hata *regulation* kwamba unajiuliza, hivi Msikitini ni lazima utie mfereji wa nusu nchi. Mwengine anafungua maji anaangalia kwanza ndio anasukutua, hata ukitizama keshatumia lita 20 kwa kutia udhu mara moja. Sasa haya ni mambo ambayo mimi nasema ni mfano, lakini kwa sababu maji ni *resource* ambayo nayo ukiitumia itakwisha. Hata tujaalie tutizame kwenye mahoteli vile vile, mahoteli mengi yako katika sehemu ambazo ni za mwamba kwa *coral*, lakini unakuta lile jiwe lenyewe limefanya mbolea kwa kutiliwa maji, kwa sababu wametumia maji kwenye mahoteli bila ya kizuizi, bila ya kipimo, bila ya kuambiwa haya maji uliyotumia kiasi chako ni haya kwa matumizi haya. Kwa hivyo, na *regulation* ya matumizi nayo mimi nadhani ilihitajika ni muhimu sana.

Suala jengine ambalo nitalichangia kwa ufupi tu, kuhusu suala la migogoro ya ardhi. Niseme tuna tatizo la msingi Mhe. Spika, na hili nimelisema mara nyingi kwamba katika suala la ardhi migogoro ni mingi kuliko vile tunavyoifikiria, lakini hatuwezi kuendelea kuwa na migogoro ya ardhi. Juhudi mbali mbali zimechukuliwa, Waheshimiwa Wawakilishi hapa kama wanaona bado na wao wanaweza kufanya juhudi kusaidia kutatua kwenye hili, ni sawa.

Mimi wasi wasi wangu Mhe. Spika, ni kwamba na naomba nitanabahishe hii *generalization*, maana ukisema mgogoro wa ardhi tunaotaka sisi kuuchunguza ni lazima tujiulize tunakusudia upi. Mimi na Mhe. Omar Yussuf tunadaiana ardhi pia nao ni mgogoro tunaotaka kuuchunguza au ni mgogoro wa namna gani. Kwa hivyo, uamuzi wowote tunaotaka kuufanya ni lazima tuwe na *definition*, tuwe *specific.* Kama Mhe. Hamza Hassan hapa kaleta na mifano kwamba kuna ardhi fulani. Mhe. Hija Hassan na yeye kaeleza pia. Kwa hivyo, mimi nadhani chochote unachotaka kufanya na kwa sababu migogoro mingine iko mahakamani, iko migogoro mingine ya ulalamishi vile vile. Nasema katika hili ni vizuri tuwe makini, kwa sababu tunaweza tukafika pahala kutokana na matatizo yaliyopo kwenye ardhi. Kwa sababu ardhi yetu haijapimwa, hakuna mwenye warka, ulalamishi uko mwingi vile vile, wengine wameuza baadae wanarudi wanadai. Nasema katika hili ni vizuri tuwe makini sana, ni tatizo gani ambalo limeshindikana, halishughulikiwi, haliko mahakamani na kweli ni tatizo ambalo linahitaji kushughulikiwa.

La mwisho Mhe. Spika, alitaja Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa suala la shamba la Mhe. Saidi Iddi Bavuai liliopo Buyu. Wasi wasi wangu ni kwamba kwa namna alivyoliweka likibaki vile vile linaweza likatoa picha kama kwamba serikali sasa inamnyang'anya na yeye ardhi yake, kitu ambacho nadhani kama ni shamba hilo ninalolifahamu basi nadhani inawezekana sio picha sahihi.

Mhe. Spika, mimi nakumbuka suala ambalo linahusu shamba la Mhe. Saidi Iddi Bavuai, kama ni lile linalohusu mgogoro wa Shakani, basi Mhe. Spika, una historia ndefu. Ulianza mwaka 1988 wakati bwana Ahmed Sharif maarufu wanamwita Sharif, alipokwenda *branch* kutaka kusajili vipande vyao vinne yaani vishamba yao vinne kwamba ni haki yake. Shamba ya Shangazi yao Mwanayamu, lakini na kina Bavuai nao wakasema aah! Huyu ni Shangazi yetu na sisi tuna haki ya kurithi. Kwa hivyo, wakenda mahakamani kudai mirathi ya vishamba vyao vinne, sijui Buyu Pwani, Buyu Chongoleani, Buyu Bigilini. Sasa mgogoro uliokwenda mahakamani ni huo, ili kuamua nani anarithi, na Mahakama Kuu ndivyo ilivyoamua hivyo. Lakini ilipokuja sasa kurithishwa ndio ikaja sasa Shakani yote nzima ikaonesha kama ni ya kwao, wakati walidai vishamba vinne na hapo ndipo ulipoanza mgogoro wa suala hili.

Kwa hivyo, mgogoro huu bahati mbaya umekuwa mgumu sana kuutatua kwa sababu mbali mbali. Hata Dk. Salmini Amour Juma Rais Mstaafu, aliwahi kuunda tume na tume ikathibitisha kwamba kweli katika haya madai yao wameingilia mashamba mengi ya watu. Ikaja ikaundwa tena tume ya pili na Mhe. Rais Mstaafu Mhe. Aman Abeid Karume ikathibitisha hivyo hivyo, mahakama ikapeleka watu kwenda kuthibitisha kwamba kweli pale kuna

mgogoro, lakini kilichoharibika ni katika uamuzi wa mahakama katika suala hili.

Kwa hivyo, mimi nadhani Waziri hatokuwa na jibu kuhusu suala hili, kwa sababu sio yeye aliyemnyang'anya. Huu ni mgogoro ambao uko mahakamani na nadhani suluhisho litaishia mahakamani. Sasa tukimtaka waziri nadhani tutakuwa tunampa kazi ambayo sio ya kwake. Sasa kama kuna suala la kulizungumza hili, tunaweza hata tukakutana na wanaodai ili tukalizungumza na tukaona wapi linaweza likatatuliwa kwa njia zile zile za kisheria zilizotatuliwa.

Mhe. Spika, naomba tusitowe *impression* kama kwamba serikali inamnyang'anya muasisi huyu, nadhani tutakuwa tunatoa picha ambayo sio sahihi. Mhe. Spika, baada ya kusema hayo nilisema na mimi nichangie ili kusaidia labda mawazo yangu katika masuala haya.

Baada ya kusema hayo na mimi naunga mkono hoja na ninaomba Waheshimiwa Wajumbe, tuunge mkono hoja hii, ili tumuwezeshe Mhe. Waziri ili aweze kuyafanyia kazi yale ambayo yanatukwaza, yale ambayo ni matatizo. Mimi naamini ana uwezo huo na nina amini ana nia hiyo na naamini mengi anaweza akayashughulikia na ushahidi ni pale atakapokuja yeye mwenyewe kuyaeleza. Ahsante sana. *(Makofi).*

Mhe. Spika: Mhe. Mwanasheria Mkuu nakushukuru. Nawashukuru pia Waheshimiwa Wajumbe, hasa baada ya Mhe. Mwanasheria Mkuu kumaliza, akasema Mhe. Waziri huyu ana uwezo na nia ya kufanya vizuri.

Basi baada ya hayo jioni Waheshimiwa Wajumbe niwaombeni kwamba tumsikilize Mhe. Naibu Waziri kwa namna atakavyojipanga, halafu baadae tumsikilize Mhe. Waziri kwa ajili ya majumuisho.

Baada ya hayo basi naakhirisha kikao hiki hadi saa 11:00 jioni leo.

(Saa 6:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 Jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano Yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kama tulivyokubaliana pale kipindi cha asubuhi, kwamba majadiliano ya hivi sasa kwa Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, na baada ya hapo atakuja Mhe. Waziri mwenyewe, karibu sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, ahsante. Kwanza nianze na kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataalla* kwa kutuwezesha kukutana hapa tena jioni hii tukiwa salama. Vile vile nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuzungumza machache katika kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. *(Makofi)*

Pia nimshukuru sana Mhe. Waziri wangu wa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban kwa mashirikiano makubwa sana aliyoyajenga kwangu. Mhe. Spika, bila ya kuwasahau wafanyakazi wote wa wizara hii kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa mimi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi sitozungumza mengi kwa vile Mhe. Waziri atakuja kutoa ufafanuzi zaidi juu mambo yote yaliyozungumzwa katika michangio ya kuichangia hotuba hii. Lakini nataka niliseme suala linalohusiana na Shirika la Umeme, hususan katika hili tatizo lililojitokeza katika kipindi kifupi hapo Shirika la Umeme, linalohusu tatizo la ulipaji wa umeme usiokuwa wa uhakika.

Mhe. Spika, kwanza nikiri kwamba tatizo hili ni kweli limetokea katika Shirika letu. Lakini tatizo hili limesababishwa na mitambo yetu, ambayo tunayotumia kwa ajili ya malipo ya umeme. Kwa hivyo, naomba niwahakikishie wananchi kwamba suala hili tumeliona, na tayari limeshafanyiwa marekebisho tokea tarehe 10 mwezi wa Julai, 2012. Hivyo, nawaomba wananchi wasiwe na wasi wasi juu ya hili, na tunategemea kwamba tutakwenda vizuri katika kuwapa huduma hii wananchi, na tunategemea kile watakachokilipa ndicho watakachokipata.

Vile vile tukiliangalia suala la ulipaji wa umeme. Kwa kweli baadhi ya wananchi wanapobadilishiwa mita zao kwa wale wanaotumia mita za kawaida na kufungiwa mita za TUKUZA, baadhi ya wananchi hao ndani ya mita zao za kawaida zinakuwa na madeni makubwa. Sasa shirika langu baada ya kwisha kumfungia mita nyengine mteja, basi huwa inafanya tathmini ya kile kiasi ambacho anachodaiwa, na kufanywa malipo ule wakati anakwenda kulipa au kununua umeme kwa mita yake ile aliyofungiwa kipindi hichi anachoendelea.

Kwa mfano, kama analipa shilingi 10,000/=, basi hukatwa deni la shilingi 5,000/= ndani ya shilingi 10,000/= na kupewa umeme wa shilingi 5,000/=. Kwa hivyo, naomba wananchi na hili nalo walielewe kwamba lipo, na hiyo ni njia moja ambayo itatusaidia sisi shirika letu na kuweza kuliendesha shirika hilo.

Mhe. Spika, sasa naomba nizungumzie kuhusiana na suala la umeme mbadala. Kwa kweli wachangiaji wengi waliochangia katika hotuba hii wamelizungumza hili, na niseme kwamba serikali suala hili inalo na inalifanyia kazi. Lengo la serikali ni kuleta umeme mbadala Zanzibar. *(Makofi)*

Kwa hiyo, niseme kwamba kabla ya kuleta umeme mbadala, basi ningeomba sisi viongozi pamoja na wananchi tujifunze katika kutunza miundombinu yetu hususan hii ya umeme. Kwa mfano, tukiangalia kuna tatizo la wizi wa umeme, tatizo hili lipo na wengi wanalielewa tatizo hili, kwamba baadhi ya wananchi huwa wanafanya vitendo vya kuiba umeme.

Lakini tuelewe kwamba kufanya hivi ni kulihujumu Shirika la Umeme, na hatimaye shirika litashindwa kujiendesha, na kesho tutasimama hapa tuseme shirika hili limeshindwa kujiendesha kwa sababu wafanyakazi wa shirika wezi. Kwa hivyo, naomba suala hili tulifahamu na tujitahidi sisi viongozi kama Wawakilishi tuwe katika mstari wa mbele katika kulinda tatizo hili kwa wananchi, ili wasiibe umeme kiholela. *(Makofi)*

Vile vile katika suala la kutunza miundombinu yetu, kuna wananchi wengi tu ambao huwa wanafanya vitendo vya kuhujumu miundombinu yetu, hususan ya kuchimba mchanga maeneo ambayo imepita miundombinu hiyo ya umeme.

Mhe. Spika, naomba ikumbukwe pale kinapofanyika kitendo kile ikiwa wewe Mwakilishi tayari unayo habari ya tukio lile linalofanyika na ukashindwa kuchukua hatua, basi ukumbuke kwamba athari itakapotokea watakaoathirika ni wananchi, Shirika la Umeme, pamoja na serikali kwa jumla. Kwa hivyo, nawaomba sana Waheshimiwa Wawakilishi tunapopata taarifa ya uharibifu wa miunombinu hususan katika yale majimbo yetu, basi sisi tuwe makini na tusimamie katika kuliokoa shirika letu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, si kuhusiana na uchimbaji wa mchanga tu, tutakumbuka kipindi cha nyuma baada ya kutokea shoti ambayo iliharibu *cable* yetu, basi umejitokeza wizi mkubwa wa kuibiwa nyaya za umeme. Kwa mfano, nyaya zile zilikuwa zikiibiwa katika maeneo ya mjini pamoja na mashamba. Sasa sisi Wawakilishi tukumbuke kwamba, ili tuwaongoze watu wetu vizuri, basi tuwalinde katika kufanya mazuri. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nawaomba Wawakilishi tujitahidi juu ya hilo, na linapotokea tushirikiane na tuhakikishe kwamba tunailinda rasilimali yetu hususan kwa kuilinda Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nikiondoka katika suala la umeme sasa niende kwenye suala la migogoro ya ardhi. Suala hili limezungumzwa na Mhe. Hija Hassan Hija na alieleza kimuhtasari tu, kwamba maeneo ya Nungwi pamoja na Kendwa kwamba kuna migogoro mingi ya ardhi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, niseme kwamba suala hili si kwa maeneo ya Nungwi tu au Jimbo la Nungwi, isipokuwa niseme ni kweli na tunakiri kwamba migogoro ya ardhi ipo. Lakini naomba niseme tofauti na vile alivyozungumza Mhe. Hija Hassan Hija, kwamba Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati anaelewa hayo na wala hasemi lolote juu ya migogoro hiyo. *(Makofi)*

Kwa hivyo, naomba nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba kusema ndio huku, na kila pale ninapojibu swali linalohusiana na migogoro ya ardhi, basi mwanzo mimi nakiri kwamba migogoro ya ardhi ipo. Lakini serikali iko tayari kuishughulikia migogoro hiyo. Kwa maana hiyo, naomba nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba Mhe. Naibu Waziri hakunyamaza juu ya migogoro hiyo. *(Makofi)*

Kwa uthibitisho zaidi kwamba sikunyamaza, naelewa mgogoro uliokuwepo ndani ya Kijiji cha Kendwa. Mhe. Spika, kuna kijana mmoja ambaye nitamtaja kwa jina moja la James ambaye kijana huyu amekodishwa nyumba, ambayo iko maeneo ya *beach* na watu wa Kendwa. Sasa baada ya kukodishwa nyumba hiyo amelipa vizuri kipindi cha miaka mitano, kila baada ya mwaka alikuwa akilipa vizuri.

Lakini kuendelea katika kipindi cha mwaka wa 6 na 7, kijana huyu ameshindwa kulipa na kila wanapokwenda wenyewe kudai haki yao ya malipo, basi huyu kijana alikuwa anachokifanya ni kuwababaisha na kutolipa kodi hiyo.

Kwa kweli suala hili limeletwa wizarani, baada ya kuletwa wizarani tulimwita huyo kijana kwa kumtumia barua, lakini kijana huyo baada ya kumtumia barua hiyo hakufika wizarani na wala hatukupata jibu lolote kwake, pengine hakufika kwa sababu gani kama vile ni dharura au vyenginevyo.

Mhe. Spika, naomba nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba suala hili bado wizara yangu haijashindwa na inalishughulikia, na tutamuandikia barua nyengine ya wito, kama ikishindikana kuja kuzungumza naye, basi wizara yangu itachukua hatua zinazofaa na tutahakikisha mgogoro huo unapatiwa ufumbuzi. Vile vile si kwa huo tu, pamoja na migogoro mingine yote iliopo, sisi tupo tayari kuishughulikia, na niseme kwamba wizara yangu haijashindwa kabisa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, niwaombe Waheshimiwa Wawakilishi kwamba bado tuendeleze mashirikiano, na sisi wizara tuko tayari kushirikiana nao, kwa chochote watakachotuongoza, basi hatuna tatizo na tutashirikiana, ili tuhakikishe kwamba Serikali yetu ya Mapinduzi Zanzibar inakwenda vizuri na inawatendea haki wananchi wake kwa misingi yote inayostahiki kuishughulikia. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nimalizie kwa suala la maji. Kwa kweli tatizo la maji pia tunakiri kwamba lipo. Lakini niseme kwamba wizara yangu inajitahidi kulishugulikia tatizo hili, na bado hatujachoka kulishughulikia tatizo hili. Kwa hivyo, tutashirikiana na Waheshimiwa Wawakilishi kila pale ambapo kuna tatizo, basi tutakapopewa taarifa sisi tuko tayari kushirikiana nao. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nawaomba zaidi Waheshimiwa Wajumbe wasituwekee ngumu katika bajeti hii, kwa sababu pale watakapotuwekea ngumu na kutopitisha bajeti yetu hii, sijui tutaweza kutatua vipi matatizo haya tuliyoyazungumza. Kwa hivyo, niwaombe sana Waheshimiwa Wawakilishi, kwamba tushirikiane na bajeti yetu tuipitishe vizuri bila ya matatizo yoyote, hapo ndipo tutakapoweza kuyatengeneza na kuyashughulikia majukumu yetu. *(Makofi)*

Baada ya hayo machache Mhe. Spika, mimi mwenyewe binafsi naunga mkono pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Nungwi hotuba hii kwa asilimia moja. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, anarekebisha. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwa asilimia mia moja. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, katika kiungo kibaya ndani ya mwili wa binadamu ni ulimi. Kwa kweli ulimi ukikosea unaweza ukakufikisha pahala pabaya sana. Kwa hivyo, alipokosea kusema asilimia moja yeye Mhe. Naibu Waziri, kwa kweli ilikua kwamba ulimi umeteleza. Lakini nashukuru kwamba ametafakari na kuja kusahihisha hilo.

Waheshimiwa Wajumbe, sasa naomba nimkaribishe Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati karibu sana. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia tena kunipa afya, na kuja kusimama hapa kwa mara nyengine tena kwa ajili ya kutoa ufafanuzi au

majumuisho ya hapa na pale kwa Waheshimiwa wenzangu Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, tangu jana mpaka leo naweza kusema kwamba nimepita katika ule utaratibu ambao niliupata mara ya mwanzo nilipokuwa Mjumbe katika Baraza la Wawakilishi. Kwa kuwa Baraza Mhe. Spika wewe unajua kwamba jambo la kwanza kabla hujaanza shughuli za Baraza unapatiwa semina, kwa hivyo tangu jana nimepata mafunzo mengi sana na ninawashukuru wenzangu kwa kunifundisha mambo mengi sana juu ya wizara hii. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, naona ni kama mwezi mmoja tangu kuingia katika wizara hii na kupata mafunzo haya, basi kwangu mimi naona ni mwanzo mzuri na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atanisaidia na nitashirikiana nao hawa katika shughuli zetu hizi za kuendesha serikali na kuwatumikia wananchi wenzetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, wizara hii imepata wachangiaji 23 na hao ndio waliozungumza. Kwa hivyo, napenda niwatambue kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Rashid Seif Suleiman (Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi),
2. Mhe. Jaku Hashim Ayoub,
3. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali,
4. Mhe. Ismail Jussa Ladhu,
5. Mhe. Asha Bakari Makame,
6. Mhe. Omar Ali Shehe,
7. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk,
8. Mhe. Hamza Hassan Juma,
9. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa,
10. Mhe. Fatma Mbarouk Said,
11. Mhe. Ali Salum Haji,
12. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa,
13. Mhe. Panya Ali Abdalla,
14. Mhe. Nassor Salim Ali,
15. Mhe. Farida Amour Mohammed,
16. Mhe. Suleiman Hemed Khamis,
17. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa,
18. Mhe. Mgeni Hassan Juma,
19. Mhe. Salim Abdalla Hamad,
20. Mhe. Hija Hassan Hija,
21. Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria,
22. Mhe. Mwanasheria Mkuu
23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan na

24. Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. (*Makofi*)

Mhe. Spika, hao waliochangia kwa kusema. Lakini waliochangia kwa maandishi ni 14 naomba niwatambue kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika,
2. Mhe. Mussa Ali Hassan,
3. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak,
4. Mhe. Salma Mohammed Ali,
5. Mhe. Shadya Moh'd Suleiman,
6. Mhe. Mlinde Mbarouk Juma,
7. Mhe. Marina Joel Thomas,
8. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi,
9. Mhe. Ashura Sharif Ali,
10. Mhe. Hassan Hamad Omar,
11. Mhe. Abdalla Juma Abdalla,
12. Mhe. Rufai Said Rufai,
13. Mhe. Bikame Yussuf Hamad,
14. Mhe. Abdi Mossi Kombo.

Mhe. Spika wote hawa waliochangia kwa maandishi, na wale waliochangia kwa kuzungumza, wamenisaidia sana katika kazi ambayo nakusudia kuifanya katika wizara hii, na kwa kweli wamenifunua macho sana, tena nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, masuala au hoja 113. Kwa kweli kama hoja 113 ikiwa nitazijibu hapa muda wetu huu ni saa mbili na kidogo utamalizika. Kwa hivyo, nitawaomba waheshimiwa Wajumbe wanisamehe kwa kujibu kila hoja, kwa sababu kwanza sina utaalamu wa kujibu kila hoja katika wizara hii, nakiri kabisa na muungwana ni kukiri. *(Makofi)*

Vile vile baadhi ya hoja kwa kweli zinahitaji ufuatiliaji wa karibu na nyengine unaweza kuzijibu mara moja, kwa sababu ni hoja nzito na huwezi kuzipuuza, kuzidharau na wala kuzibeza kwa namna yoyote. Kwa hivyo, nadhani Waheshimiwa Wajumbe watanistahamilia sana katika hilo, na nitajibu baadhi ya hoja maana hazishi hizi, hoja 113 sio mchezo ni nyingi mno.

Mhe. Spika, unajua baada ya kuzungumza hapa kujibu hoja unangojewa kwenda kucheza mchaka mchaka wa kunyanyuka na kukaa kwa buti. Sasa na hiyo pia inahitaji stamina ya aina yake. Kwa hiyo, hapo pia nitaomba Waheshimiwa Wajumbe wanisamehe na nijibu zile ambazo nitakazoweza kuzijibu na nyengine nizichukue kwa ajili ya kwenda kuzifanyia kazi na *In*

shaa Allah Mwenyezi Mungu atatuwezesha tutafanya vizuri. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika, kabla ya kusahau nawaambia wenzangu wafahamu kwamba, tunachotaka ni kurekebisha baadhi ya mambo katika wizara yetu hii. Sasa watakaponipa nafasi, basi nadhani Mwenyezi Mungu atanisaidia kwa kushirikiana na wao, kurekebisha hayo mambo ambayo wanayaona yana matatizo, lakini wakinizuilia nafasi, sijui tutarekebisha vipi, maana yake ni sawa kwamba umewekwa uwanjani na ukaambiwa uwanja huu unatakiwa usafishe. Sasa unapita kusafisha uwanja mtu anakuvuta nyuma na kukwambia njoo kwanza, kwa hiyo niachie nisafishe huu uwanja. Mhe. Spika, ukinivuta nyuma huku au ukinigonga miguu, maana siwezi kwenda, uwanja utanishinda kusafisha ule. *(Makofi)*

Nadhani wenzangu hawa watanipa hiyo nafasi ya kufanya hii kazi, ili tuweze kufika pale tunapokusudia, na hilo ni suala muhimu kabisa katika masuala yetu haya. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba nianze na hoja chache kidogo zilizotolewa, na nachagua zile moja moja na wala sitojibu zote Mhe. Rashid Seif Suleiman (Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi), ameulizia baadhi ya hati zimefanyiwa kazi na nyengine bado hazijafanyiwa kazi.

Mhe. Spika, kwenye hotuba yangu nilieleza kwamba mikataba mingi inayowasilishwa kusainiwa na waziri huwa haistahiki kusainiwa na yeye, kisheria waziri anasaini Mikataba ya Ukodishaji wa Ardhi pamoja na Hati za Matumizi ya Ardhi iliyogaiwa na serikali tu, na mikataba mingine yote inatakiwa kufuata taratibu za uhaulishaji na hatimaye usajili wa ardhi, ambao haumuhusishi Mhe. Waziri.

Kwa kweli kwenye hotuba yangu nimeshukuru sana kwamba Msajili wa Ardhi ameteuliwa. Kwa hivyo, hivi sasa suala la Waziri kufanya kazi ya kusaini mikataba ya uhaulishaji wa ardhi, hiyo si kazi ya waziri, isipokuwa ni kazi ambayo inafanywa moja kwa moja na Katibu wa Uhaulishaji. *(Makofi)*

Vile vile suala la Mwenyekiti katika Bodi hii. Mhe. Spika, suala hilo liko kwenye *pipeline Inshaallah*, na si muda mrefu Mwenyekiti atapatikana na wala hakuna wasi wasi wowote. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub, yeye alizungumzia wasi wasi wake juu ya Mamlaka ya Mji Mkongwe kuhodhi madaraka yote ndani ya mji huu, ingawa hali ya mji wenyewe bado hairidhishi. Vile vile anataka kujua faida ya Mji

Mkongwe kama Urithi wa Kimataifa zaidi ya kutiliwa vigae kwenye njia za mji huo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Mji Mkongwe unaongozwa na sheria na mamlaka hiyo. Kila kinachofanyika Mji Mkongwe ni kwa mujibu wa sheria hiyo iliyopitishwa na Baraza hili. Kwa kweli Mji Mkongwe una changamoto nyingi, lakini changamoto hizo ziko kwenye maeneo yote ya mji, isipokuwa Mji Mkongwe unaonekana zaidi, kwa sababu ndiko kwenye mrundikano mkubwa zaidi wa shughuli mbali mbali kama vile biashara, utalii na utamaduni.

Suala hili linachangia zaidi na Hadhi ya kuwa Urithi wa Dunia, faida ambayo inawachochea wawekezaji wengi akiwemo Mhe. Jaku Hashim Ayoub mwenyewe kufikiria kwanza kuwekeza Mji Mkongwe kuliko kwengineko, licha ya changamoto zote alizozitaja.

Miongoni mwa masharti yake katika Mji Mkongwe ni *control* ule mji kwa baadhi ya mambo kidogo yawe hayafanyiki kule. Mhe. Spika, moja katika hilo ni kupanga utaratibu wa kuingia magari kule, maana ule Mji Mkongwe unahifadhiwa. Sasa kwa sababu unahifadhiwa ukiacha gari kubwa ziingie kule na kwa kuwa zile nyumba ni za muda mrefu sana tena ni za udongo na mawe na wala si za matofali, basi baadhi ya nyumba huonesha athari za kupasuka.

Kutokana na sababu hiyo, ndio maana Mji Mkongwe ikaamuliwa kwa makusudi kabisa baadhi ya maeneo gari zisipite kabisa, na maeneo mengine zipite gari, lakini ni *one way* na zisirudie tena na zipite gari za kiasi na wala zisipite gari kubwa.

Mhe. Spika, ndio maana Mhe. Jaku Hashim Ayoub akaona kule njia zinafungwa kwa mujibu wa sheria, Mji Mkongwe unapata hadhi kwa jambo hilo, kwamba ule mji unalindwa. Mimi nimeondoka ofisini pale wakati nilipokuwa nakuja huku, basi ule mji Mhe. Spika utafikiri si mji wa Zanzibar hivi sasa, yaani umejaa watalii wengi ajabu, na wala humuoni Mswahili hata mmoja kama vile sehemu za Posta mpaka unakuja Mahakamani kumejaa watalii wengi.

Kwa hivyo, ili watalii waendelee kukaa pale, ndio maana hizi *traffic* zinapokuja kwa ajili ya kuwa-*controlled* kule, yaani ndio sababu ya *conrol traffic* kule katika Mji Mkongwe, hilo ndilo suala lenyewe. *Unless* kama tutasema tunabadilisha uamuzi kwamba hatutaki uwe Mji Mkongwe, lakini uwe mji wetu tu, na watu wafanye wanavyotaka na hilo litakuwa suala jengine Mhe. Spika.

Kwa kweli Mhe. Jaku Hashim Ayoub amezungumza mambo mengi na wala asifikiri kwamba sikuyachukua na nilisema niseme na kwangu, na nitalazimika kuyafanyia kazi, tena ninayo kwenye buku langu, maana buku karibu lijae kwa kuandika mambo mbali mbali, Mhe. Hamad Masoud Hamad alinitania pale kwamba naandika kama Jaji au unandika kama Daktari kutokana na alivyoniona nikiandika pale. Kwa hivyo, ninayo yote.

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali, alihoja kuhusu safari nyingi za nje ambazo zinapunguza uwezo wa kuwahudumia wananchi mahitaji ya msingi na ya dharura, na alisema ziara hizo zisitishwe.

Mhe. Spika, serikali kupitia wizara yangu inatafakari kwa makini aina ya safari zinazoendwa na watendaji na viongozi wake. Kwa maana hiyo, ni zile zinazoonekana kuwa na tija tu ndio hufanyika, na sio kila safari inalipiwa moja kwa moja na serikali, baadhi hugharamiwa na waandaaji, nyengine wahisani na pia kuna zile ambazo watendaji kwa namna moja au nyengine hujigharamia. Kwa kweli safari nyengine ni sehemu muhimu ya mchakato wa miradi kamili kama vile ya *Africa Development*, *JICA*, *MCC* na kadhalika. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ifahamike pia kwamba Zanzibar ina haki ya kushirikishwa katika Vikao vya Ushirikiano vya Kikanda, kama vile Jumuia ya Afrika ya Mashariki, *SADC*, ambapo mara nyengine huhitaji tujigharamie, mbali ya Ujumbe wa Watanzania, ambao kwa masuala mahsusi unaweza usikidhi haja ya kutetea maslahi mahsusi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Vile vile Mhe. Mjumbe alihoji kwamba walikuwa wapi viongozi wa wizara hata Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kutembelea vituo vya mafuta wakati wa uhaba wa bidhaa hiyo na Ikulu kutoa tamko kuhusu uhaba huo. Mhe. Spika, Idara yangu ya Nishati nashukuru sana tangu siku ile nimewaambia, kwamba wao wana jukumu la kuhakikisha mafuta katika nchi hii yanakuwemo.

Kwa kweli waliniuliza kwamba Mhe. Waziri unatuambia hivi kwa sheria gain? Niliwaambia sheria itafuata baadae, lakini hivi sasa nataka muone kwamba mafuta katika nchi hii yanakuwepo kwa wakati wote, na muwe munaweka data zenu vizuri, ili kuhakikisha upungufu gani upo kwa lengo la kuhimiza na hiyo sheria ambayo mnasema inatayarishwa basi itayarishwe na itakuja, lakini hili ni jukumu letu tufuatilie. Mhe. Spika, nawashukuru sana wanafuatilia kwa karibu kabisa, na wala si vibaya akatokea kiongozi wa kitaifa akatuunga mkono ni vizuri kabisa na huwa tunafurahi sana.

Mhe. Spika, kama kuna msikiti unasalisha na katika msikiti ule unatoa mawaidha, basi babu yangu mmoja aliniambia kama unataka uwe shekhe

mzuri, siku anayokuja shekhe unayemuamini mwambie yale mawaidha unayotoa wewe basi atoe yeye.

Sasa atakaposimama yeye yule na kupita mule unamopita wewe, basi wale ndio watasema ehe! Kumbe shekhe wetu anatuambia maneno yale yale anayotuambia shekhe huyu, kumbe anatuambia ndivyo na wewe unapata nguvu. Kwa hivyo, sisi tukipita tukawahimiza watu wa mafuta na halafu akatokea Mhe. Makamo wa Pili wa Rais akenda naye na kuzungumza yale yale, basi wewe unasema aa! Kumbe sasa serikali iko *serious* katika suala hili, ndio maana yake. *(Makofi)*

Kwa hivyo, namshukuru sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais katika kufuatilia upungufu huu unapotekea. Kwa kweli kama tusipokuwa karibu na wenzetu hawa Mhe. Spika, tutapata tatizo kubwa sana la mafuta katika nchi hii. Maana hawa kama hukuwafuata kwa karibu wakisikia mafuta yamepanda bei basi wanasita kuuza, wanasubiri na wao waambiwe wapandishe bei na yao. *(Makofi)*

Lakini kwa bahati mbaya kama alivyosema Mhe. Mjumbe mmoja kwamba wakisikia yameshuka bei hawakubali kuteremsha. Mhe. Spika, naahidi kwamba suala hili tutalifuatilia kwa karibu na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atatusaidia.

Mhe. Spika, yapo mengine ambayo amezungumza Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali sikuyaacha, isipokuwa ninayo katika maandishi yangu, lakini nimejibu hili ambalo lina umuhimu wake.

Vile vile Mhe. Ismail Jussa Ladhu, amehoji kuhusu uhalali wa Bara kuendelea na uchimbaji na utafutaji wa petroli na gesi asilia wakati Zanzibar imesitishwa. Mhe. Spika, pia Mhe. Mjumbe amehoji ukimya wa Zanzibar kuhusu Mkataba wa *Block No*. 8 alilolitaja kuwa ni la Zanzibar kutiwa saini na Waziri wa Nishati na Madini wa Serikali ya Muungano.

Mhe. Spika, hapa tunaweza tukawa labda tulipitikiwa, kwa sababu *Block No*. 9, 10, 11 na 12 ni *Block* zilizoko sehemu ya Zanzibar moja kwa moja tena wazi wazi, na hizi tumezizuia hazina ruhusa ya kufanyiwa utafiti wa aina yoyote.

Mpaka leo hazijafanyiwa utafiti kwa sababu tumezizuia. Kwa bahati mbaya *block* nam. 8 iko kule ipo na huku. Wakati ule ilipotajwa kuzuia hii haikutajwa kwa sababu ilionekana imegusa huku na huku. Labda ilibidi tuchore mpaka mwengine katikati sasa hivi kwamba *block* nambari 8 muingie mpaka hapa msizidi hapa, labda ingebidi tufanye hivyo.

Lakini *block* nambari 9, *block* nambari 10, *block* nambari11 and 12, hizi ziko *intent* kabisa mpaka sasa hivi. Na hazitofanyiwa uchunguzi wa aina yoyote mpaka tujue kimeeleweka. Hivi ndivyo tutakavyofanya na huo ndio msimamo wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, si msimamo mwengine kabisa hiyo hakuna wasi wasi.Tunaambiwa kwamba wakati tunangojea basi ufanywe angalau utafiti, aaa! Watu huagana pwani bwana, hawaagani kati kati ya bahari.

Mkifanya utafiti mwanzo maana yake kwamba mnakwenda kuagana kati kati ya bahari. Katikati ya bahari hakuna maagano tena. Lakini mkiagana pwani kabla hamjaingia baharini inakuwa uzuri zaidi, maana anayekwenda atakwenda atakaerudi atarudi, maana anakuwa yupo juu nchi kavu, lakini mkiingia bandarini hakuna tena maagano tena. Kwa hivyo watu huagana pwani, Waswahili ndivyo wanavyosema. Kuagana pwani ni kwamba tuseme hili tulililoliamua katika Baraza la Wawakilishi litekeleze kwanza halafu ndio twende kwenye mambo ya utafiti na mambo mengineyo.

Mhe. Omar Ali Shehe alihoji limbikizo kubwa la madeni ya kodi za nyumba na akatishia kutoipitisha bajeti iwapo hayatakusanywa. Naomba kumuhakikishia Mhe. Omar Ali, kama alivyobaini akiwa Mwenyekiti, wa Kamati ya PAC. Ukusanyaji umeongezeka sana katika na hivyo madeni hayo kupugua sana. Mkakati wa Wizara ni kuwa ifikapo mwaka 2013, madeni yasipindukie kodi ya mwezi mmoja ya nyumba zote za Serikali yaani kila nyumba, moja ya mkakati huo ni huu wa kuundwa shirika la nyumba.

Kwa kweli suala la kuunda Shirika la Nyuma tuka *serious* kabisa, sio maneno matupu. Moja ya mikakati huo ni kuunda Shirika la Nyumba. Ni vyema ikaeleweka kwa taasisi za ukodishaji nyumba haiyumkiniki kudai wapangaji muda wowote. Kuna wanaolipa kila baada ya miezi fulani ndani ya mwaka na hivyo kabla ya muda huo kutoonekana kulipa kodi kuna wanaochelewa kwa sababu ya taratibu za kibenki, kuna wengine ni wadaiwa sugu na kadhalika. Unapopita madeni ya Idara hiyo hadi sasa ni vyema tumezingatia na kanuni hii ya msingi. Mhe. Omar Ali Shehe, amezungumza mengi na yeye, masuala ya mafuta ameligusa vile vile, nitatoa maelezo yake baadaye.

Mhe. Mshimba Makame Mbarouk anahoji sababu za kukatiwa umeme wadaiwa wadogo wadogo tu na kuachwa wenye madeni makubwa. Mhe. Spika, kila mteja hulipa na kudaiwa kwa mujibu wa kiwango cha matumizi yake. Inawezekana bili ya mteja mkubwa ikawa ni shilingi milioni moja kila mwezi na ya mdogo ni sh 10,000/- tu kwa mwezi, mteja mkubwa akidaiwa milioni mbili maana yake ni kwamba hajalipa kodi ya miezi miwili. Lakini mteja mdogo anapodaiwa sh 12,000 anakuwa hajalipa kodi kwa miezi kumi na mbili huyu anakuwa ni mteja sugu zaidi licha ya udogo wa bili yake

anahitaji kukatiwa mwanzo kuliko asiyelipa kwa miezi miwili tu licha ya ukubwa wake, kwa sababu ya vile viwango vyao ambayo wameviweka.

Mhe. Spika, wajumbe naomba wanisamehe sitowataja kama vile walivyochangia, nitawataja kwa kupita katika zile hoja. Kama nilivyosema mwanzo sitojibu hoja zote, si rahisi kuweza kuzijibu kwa wakati wetu tulionao. Mhe. Mbarouk Mtando alitaka kujua safari zinazowendwa na Katibu Mkuu wa Wizara hii na faida yake. Kwanza kabisa Mhe. Spika, naomba kutoa ufafanuzi kwamba watendaji wakiwemo Makatibu Wakuu, hawana maamuzi ya mwisho juu ya safari wanazokwenda. Wanapaswa kupata idhini ya Serikali inayohitaji kwanza baraka za Mawaziri wao.

Madhumuni kuhakikisha kwamba safari inayoadhimiwa ina umuhimu, ulazima na manufaa kwa nchi ikalinganishwa na gharama zake. Ili kuondoa wasi wasi kama Mhe. Mtando baadhi ya safari hizo huwa pia ni maagizo ya Serikali yenyewe lakini pia kwa safari zinazohusisha ujumbe wa Wizara moja ama tofauti anapaswa kuongoza ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Serikali husika. Kwa maumbile ya Wizara yenye majukumu, sekta tofauti, safari za namna hiyo ni jambo la kutegemewa sana.

Mhe. Spika, Wizara yangu ina wafadhili wengi sana wanayoisaidia Wizara hii katika mambo mbali mbali na wakati mwengine unalazimika kuwafatilia. Safari za hivi karibu za Katibu Mkuu wa Wizara yangu ni ile ya *Saint Petersburg* Urusi ya tarehe 22/ Juni hadi tarehe 6 Julai mwaka 2012 alikoongoza wataalamu wa Wizara kwenye kikao cha Mkutano wa Urithi wa Dunia, Mji Mkongwe uliwasilishwa. Utekelezaji wa maelekezo yaliyotolewa na vikao vya miaka ya nyuma kuhusiana na miradi mbali mbali ukiwemo wa Bandari, Mambo Msige, Ukingo wa Mizingani, Matengenezo ya *Beit el Ajaib* na kadhalika.

Mahudhurio hayo ndiyo yanayohakikishia Mji Mkongwe kubaki kwenye orodha ya urithi wa dunia, gharama zimelipwa na SMZ yenyewe. Tarehe 3 hadi 10 Juni aliongoza ujumbe wa Zanzibar uliokwenda Botswana kwa ziara ya mafunzo juu ya matumizi bora ya ardhi, yakiwa ni maandalizi ya mapitio ya sera ya ardhi yanayoendelea. Na mabadilishano ya uzoefu na utaalamu yamesaidia kutoa viingizo muhimu kutoka sera hiyo. Ada za safari zimelipwa na mradi wa SMOLE. Mradi huu unazingatia masuala ya matumizi bora ya ardhi.

Tarehe 1 hadi 7 April aliongozo ujumbe wa ZAWA uliokwenda nchini Uturuki kwa mualiko wa gharama pamoja na baina na ZAWA na Shirika la Usambazaji Vifaa vya maji ili kuweza kuona teknolojia ya kisasa, utengenezaji wa zana mbali mbali za miundombinu ya maji kama pampu na

mita. Uelewa huo umetoa mwanga juu ya vigezo vinavyopaswa kutumika katika uingizaji na ununuzi wa vifaa hivyo ili kuepuka hasara ya vifaa hivyo kuharibika mara kwa mara na hivyo kuhakikisha fedha inayotumika inatoa thamani inayokusudiwa.

Tarehe 5 na tarehe 9 Disemba 2011, aliongoza ujumbe wa Wataalamu wa SMZ uliokwenda *Amsterdam* Uholanzi kwa ziara ya mafunzo kuhusu ushirikiano sanifu wa sekta za umma na binafsi katika miji ya majengo asilia. Ujumbe umejifunza jinsi ya sekta hizo zinavyoweza kushirikina kuendeleza majengo yaliyokosa wawekezaji ili kuyanusuru kama urithi wa taifa ndani ya mji ulio urithi wa dunia, gharama zililipwa na SMZ.

Kushirikiana na Kampuni iliyotoa mwaliko huo unaelekea kwenye mradi mkubwa unaogharimiwa na EU na UNESCO kuhusu kuinua uchumi wa wananchi kupitia Urithi wa Utamaduni. Ujumbe wa UNESCO utakuwa nchini wiki ijayo kwa mazungumzo zaidi.

Tarehe 22 hadi 30 Novemba 2011 alihudhuria mkutano wa Umoja wa Miji ya Urithi ya Dunia huko Ureno akiwa ni mratibu mmoja wapo wa Umoja huo, gharama za safari hiyo zimelipwa na Umoja huo. Wadhifa huo unasaidia sana kuupa Mji Mkongwe na Zanzibar heshima na ushawishi kwenye umoja huo.

Tarehe 1 hadi 10 Novemba aliongoza ujumbe wa wataalamu wa SMZ waliodhuru *Seychelles* kujifunza na upatikanaji nyumba kwa umma kwa gharama nafuu. Ziara hii iliratibiwa na Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais kufatia ziara yake ya awali nchini humo. Kwa upande wa Wizara yangu uzoefu wa ziara hiyo unasaidia sana katika uwandaaji unaondelea wa Sheria ya kuanzisha Shirika la Nyumba. Yapo masuala mengine mengi Mhe. Mtando ameyauliza lakini nasema kwa sababu ya wakati sitoweza kuyajibu.

Mhe. Salum Abdalla Hamadi alihoji kuhusu kuendelea kufanya kazi kwa Bodi ya Wahandisi na Wataalamu wa Ujenzi licha ya kumalizika muda wake. Mhe. Spika, naomba kumuhakikishia Mhe. Salum kwamba hakuna shughuli za bodi zinazoendelea tangu zimalize muda wake. Kama kuna mtu alimwambia bodi inafanya kazi, bodi haifanyi kazi. Bodi hatujaiteuwa nasubiri kuteuliwa kwa mwenyekiti ili niweze kuteuwa wajumbe.

Kinachoendelea ni shughuli za kawaida za utawala wa bodi hizo zinazoendeshwa na sekretariet ya bodi hizo ambazo katika kipindi hichi cha uchanga wake ni sekretarieti zinazoendeshwa na wafanyakazi wa Idara ya Ujenzi. Mapendekezo ya Mwenyekiti, wa bodi yameshawasilishwa na mara tutakapoidhinisha bodi mpya zitatangazwa. Ameuliza maswali mengine Mhe. Salum Abdalla Hamadi nnayo kwenye maandiko yangu.

Mhe. Hija Hassan Hija, alihisi picha muafaka zaidi ya kupamba kitabu cha hotuba ya bajeti ya Wizara yangu ingekuwa na Rais akifungua mfereji unaotoa maji badala ya iliyopo inayomuwezesha akikagua mitambo ya maji.
Mhe. Spika, napenda kumkumbusha kwamba Mhe. Rais ndani ya mwaka uliomalizika wa fedha alifanya kazi kama hizo alizozitaka Mhe. Hija ili Wizara yangu iliona kwamba pia iliyoweka ni muafaka zaidi. Watu wanachotaka ni maji hilo nalijua miye na lazima tuhakikishe kwamba watu tunawapatia maji, hilo nalijua miye. Suala la kuweka mfereji unaotoka maji bado si maji. Maana mfereji unaweza ukautoa ndani ya tangi na ukatoa maji, ukaufunga na mpira fulani ndani ya tangi, maji ni kitu muhimu kwa hivyo tengeneza mitambo ya maji ndio muhimu kabisa.

Hata tunataka kumsihi kidogo Mhe. Hija katika uwamuzi anaotaka kuufanya kusema kwamba anataka kuendelea na ujenzi kijiji kwake Mwambe, licha ya kuwa sitaki kulitumia neno hili lakini itanibidi niseme kwamba hakupewa kisheria. Kwa nafasi yake yeye namuomba ni bora aje ofisini tuzungumze, tukubaliane tunafanya nini kuliko kufanya hivyo. Maana akianza yeye na wengine watafanya na itakuwa sasa sheria inakorogeka.

Mhe. Spika, ni vizuri aje tupange tuzungumze, tukubaliane. Maana pengine hapo unapotaka kwenda kupajenga sasa hivi, huenda pakawa peshakuwa *located* mtu hapo. Itakuwa yeye sasa hazozani na mimi anazozana na huyo aliyepewa hapa mahala. Ni vizuri aje, tutakutana, tutazungumza, tutapanga, tutatizama uwezekano wa kumpatia mahala. Namshihi Mhe. Hija asifanye hivyo na afuate sheria, kwa sababu funzo unalotaka kulitoa linasura nyengine iliyotofauti. Kufanya hivyo kutawafanya wananchi wote wa maeneo mengine kususia maeneo hayo kugaiwa kwa Wazanzibari wengine. Naomba tuwasiliane tulimalize suala hilo kwa njia ya kistaarabu zaidi.

Mhe. Spika, nataka kuzungumzia kidogo kuhusiana mchango wa Mhe. Panya Ali Abdalla amezungumzia juu wafanyakazi walioajiriwa wanavyo vigezo na wanawake wangapi. Hoja imetolewa na Mhe. Panya Ali Abdalla. Jumla ya wafanyakazi wote walioajiriwa ni 66 na wanavyovigezo vilivyowekwa na kati ya hao wanawake ni 21 na wanaume ni 45.

Namuhakikishia Mhe. Panya kwamba wafanyakazi waliokufa wameshatolewa katika *pay role* na hakuna mshahara wao tena. Kwa sababu tunaogopa kuwalipa watu mishahara ambao wameshafariki PAC itakuja kutukamata baadaye. Wafanyakazi wote waliokwisha fariki washatolewa katika vocha za malipo kwani mara tu mtu anapofariki na kupata ithibati ya maandishi, taarifa hutolewa, hutangazwa rasmi katika gazeti la Serikali na kuondolewa katika orodha ya malipo ya mshahara.

Wizara imewapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi 84 na wafanyakazi 91 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi. Mchanganuo wa wafanyakazi hao wangapi wanawake hoja hii imetolewa na Mhe. Mgeni Hassan. Wizara imepata wafanyakazi 84 mafunzo ya muda mrefu na kati ya hao 51 ni wanaume na 33 ni wanawake. Aidha mafunzo mafupi jumla ya wafanyakazi 91 wamepata mafunzo hayo ambayo wanawake 65 na wanaume 26. Hili nawaomba akina mama kama watakamata kamba waliyonayo sasa kwa wanafunzi wanaoendelea madarasani basi nafasi za masomo kwa wanawake sitakuwa nyingi zaidi kuliko kwa wanaume.

Mhe. Spika, wanawake wanasoma bwana, ukipita katika hizo Sekondari Skuli ukizitizama utakuta wanaofanya vizuri wengi ni wanawake kuliko wanaume. Maana hawa watoto wakiume sijui wanamawazo gani kusema kweli. Miye wamenishangaza sana miye Wallahi, wao wapo kwenye mayoo tu basi wakati wote. Hawashughuliki kusoma, wavae suruwali wavifunge kabla hazijafika juu kiunoni, hayo ndio matatizo ambayo tunayapata katika wanafunzi wetu. Lakini watoto wanawake ukenda kuwatizama wanapasi, utakuta darasa zima wanawake kama wamo 25 wanaume utawakuta sio wengi utawakuta wa 25, wanaume utawakuta kama hivyo wako 15 au 20, lakini katika kupasi utakuta wanawake waliopasi pale katika 25 unakuta mpaka wanawake 18 wamepasi, lakini wanaume utakuta wamepasi saba au wanane. Hiyo ndio hali halisi, kwa hivyo hii watapata nafasi wengi zaidi bado.

Kuna haja ya kuwepo kwa chombo cha kusimamia ubora wa mafuta yanayoingizwa nchini na kuwepo utaratibu wa hali za bei za umeme. Ushauri huo umetolewa na Mhe. Rashid Seif. Kwa vile chombo hiki ni muhimu kinapaswa kuanzishwa kwa mujibu wa Sheria. Wizara imechukua juhudi kubwa ya uundaji wa sheria ya udhibiti wa huduma ya nishati na maji Zanzibar itakayosimamia biashara inayotokana na rasilimali ya nishati ya maji.

Rasimu ya Sheria hiyo imekamilika na kwa sasa inasubiri kuidhinishwa na Kamati ya Uongozi ya Wizara. Kwa hivyo Mhe. Rashid Seif hilo suala kamati imelipendekeza na tunalifanyia kazi *Inshalla* tutaileta sheria hapa. Wizara kuhakikisha nia yake ya kuwa Sheria ya Tathmini ya Ardhi na Majengo. Ushauri huu umetolewa na Mhe. Rashid Seif vile vile, nasema sheria hii tayari imeshatayarishwa.

Tathmini gani inayofanywa na Idara ya Mipango na Sera kwa miradi yake. Upatikanaji wa maji kwa maeneo mengi bado ni tatizo, Mhe. Fatma Mbarouk. Idara ya Mipango na Sera na Utafiti inasimamia miradi yote ya maendeleo ndani ya Wizara hii na kufatilia utekelezaji wake kwa kupitia kitengo chake

cha ufatiliaji wa tathmini. Ufatiliaji huu utasaidia kuona mwenendo wa utekelezaji wa kazi tulizojipangia ndani ya kipindi husika.

Vile vile tathmini ya utekelezaji kutuwezesha kubainisha mafanikio na mapungufu yaliyojitokeza katika utekelezaji wetu wa malengo na kuweka mikakati mipya ya utekelezaji ili tukawezesha kufika malengo hayo. Hapa mpaka Mhe. Ali Salum na Mhe. Fatma Mbarouk wakatufahamisha, nimekubali kwamba kweli, wakati wa mkutano wa hadhara pale Kibanda Maiti lile tengi hujaa maji. Lakini hilo tumelifatilia na tumegundua kwamba tatizo mchana mbali ya kuwa umeme unatupa shida. Maana kwanza tulipata habari kwamba kisima kile hakina maji. Lakini katika kufatilia tukagundua kwamba kisima kina maji lakini umeme unatupa shida. Tukafanya utafiti ni kitu gani tunapata shida kwenye umeme. Kumbe vile kuna bwana mmoja pale anafanya kazi ya *welding* sasa anapowasha *welding* umeme wote anachukua yeye kwa hivyo pale pampu inakuwa haifanyi kazi. Tunakusudia sasa hivi tupige maji usiku kujaza lile tangi ili asubuhi watu watumie yale maji.

Mhe. Spika, hapa kuna ushauri kutokana na kauli nam. 56 ya utumishi na utawala bora kwenye kukaimu nafasi ya anayetakiwa atakaimu nafasi hiyo kwa kipindi kisichozidi miezi 12. Kwa kuwa Kaimbu Mkurugenzi Idara ya Upimaji na Ramani ameshapitia kipindi hicho basi anaomba athibitishwe kwa Mkurugenzi kamili. Ushauri ulitolewa na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk. Mwakilishi wa Kitope na Mhe. Hamza Hassan Juma mwakilishi wa Kwamtipura.

Nakubaliana na Waheshimiwa Wawakilishi kwa ukomo wa muda wa dhamana haitakuwa kuzidi miezi 12 kwa mujibu wa kanuni za utumishi wa utawala bora. Napenda kumwambia Mhe. Mwakilishi kwa uteuzi wa Nafasi ya ukurugenzi unafanywa na Mhe. Rais wa Zanzibar. Hoja yake ni ya msingi na naamini kuwa kwa kuwa washauri wa wakuu wa waheshimiwa Rais tupo basi hoja hiyo itafanyiwa kazi.

Mhe. Makame Mshimba amesema hivi karibuni wapimaji wamepima kiwanja katika maeneo ya Kiwengwa kwa madhumuni ya kumpa mtu fulani na kumnyang'anya mwananchi aliyekuwa akimiliki eneo hilo. Unajua mimi katika mambo haya nimejifunza ni bora mtu ataje hakutaka kumpa mtu fulani, litajwe jina lake hasa. Sasa mimi mtu fulani simjui ndio tatizo hilo.

Mhe. Spika, kabla ya kuja suala hili napenda kueleza histori fupi ya maeneo ya ukanda wa Kiwengwa, Pwani Mchangani, mpaka Matemwe. Ukanda huu ni ukanda wa maweni ambao baada ya kukua kwa sekta ya utalii umekuwa ni maarufu kwa uwekezaji na ujenzi wa mahoteli ya kitalii. Katika ukanda huu takriban asilimia 98 ya maeneo ya ufukwe yameshauzwa kwa wawekezaji na

kujengwa Mahoteli. Kimsingi wewekezaji wote waliouziwa maeneo yaliyoekeza kutoka kwa wenyeji wa maeneo haya ambayo vijiji vyao vya asili na mashamba yao yaliyokuwa pembezoni mwa fuke hiyo.

Ili kusaidia maeneo hayo muhimu kwa utalii serikali iliona ni vyema kuimarisha miundombinu ya barabara iliyotoka Pongwe na kupitia Kiwengwa hadi Matemwe. Mapendekezo ya kitaalamu ya ujenzi wa barabara hiyo yalipangwa kuweka barabara hiyo kiasi cha mita 500 kutoka ufukweni. Eneo hili la mita 500 kutoka ufukweni ni msitu wa asili wa serikali na haujawahi kumilikiwa na watu binafsi kabla ya mpango huo.

Hii inathibitika wazi kwani mpaka barabara hiyo imakamilika hakutokea mwananchi hata mmoja kudai fidia ya eneo lake liloathirika kwa upasuaji wa njia na ujengaji wa barabara iliyotokea Pongwe mpaka Matemwe. Kilichotokea mara baada ya ujenzi wa barabara ya Pongwe/Kiwengwa/Matemwe kukamilika katika mwaka 1997/98 mwananchi mmoja mmoja walianza kusafisha maeneo kando ya barabara upande wa pili kwa kupanda mivinje na vilimo vya chakula kama miboga, mipapai na hata migomba sambamba na kuanzisha makaazi holela kidogo kidogo. Wananchi hao wengi wao baadaye walianza kuyanadi maeneo waliyojitwalia na kuyauza kwa watu wengine wenyeji na wageni.

Hali hiyo iliendelea na kuanza kushamiri kwa kasi kubwa Serikali ya Awamu ya Sita ilipogundua hali hiyo watu hawa walichukua hatua ya kutoa matangazo katika vyombo vya habari na kuwataka watu hao kuwacha kujitwalia maeneo hayo kiholela kwa kuyauza ovyo. Pamoja na hatua hiyo Serikali iliamua kulipanga eneo lote la ukanda huo lililo pembezoni mwa njia kuu ya Kiwengwa mpaka Matemwe kwa kulihami dhidi ya uvamizi huo na kuandaa mazingira bora ya kimaendeleo.

Eneo hilo lilipangwa kwa ajili ya makaazi, huduma ya kijamii na maeneo ya taasisi za Serikali na NGO, maeneo hayo yalipangwa na kutolewa hati za matumizi ya ardhi kabla ya kuwekwa mipaka ya ardhini. Mtindo huo wa kitaalamu unajulikana. kama *Pre-competition* yaani walichora kabisa kwenye karatasi ile sura ya lile eneo kabisa. Kwa hivyo watu wa taasisi mbali mbali waliopewa hati ya Serikali wakifika Idara ya Upimaji kwa kutaka kujua maeneo walipangiwa. Hata hivyo wapimaji wetu wamekuwa wakipita vikazo vingi na hata kutishiwa maisha yao na wananchi wa maeneo hayo wakiongozwa na baadhi ya wenzetu kwa madai kwamba hayo ni maeneo yao ya asili na wako tayari kufa kwa kuyatetea ili yasichukuliwe na Serikali na kugaiwa watu wanaotoka nje ya vijiji. Mambo haya yalishuhudiwa hata na vyombo vyetu vya habari vya Serikali, TV na redio.

Mhe. Spika, mimi nawaomba waheshimiwa wa sehemu ile wakae kitako walitafakuri suala hili sana. Tunapanga miji, tukijenga kiholela kuna matatizo yake, kwa hivyo watoe ushirikiano kwetu uili tupange miji vizuri iwe ni mahala ambapo mtu akenda kutembea anapapenda. Tusijenge vibanda vidogo vidogo na vyengine vya makuti, halafu wanakuwa watu wengine wanakaa pale inakuwa mtatizo moja kwa moja, tupangeni miji. Kwa hivyo nawaomba watu wa maeneo haya wakubali kwamba miji katika maeneo yale ipangwe, kuliko hivi tunavyokwenda sasa hivi.

Kuna hatari moja kama ikiwa ardhi ile ilikuwa si mali ya mtu, Serikali inataka kuipanga watu wanazuia na watu wa upande mwengine wakipata habari ile watakwambia na huku kwetu msije kupanga vile vile na upande mwengine nao watasema hivyo hivyo. Matokeo yake hakuna mahala hata ambapo Serikali wataweza kupanga. Kwa sababu watu wa sehemu zile wanakuwa wanazuia hili tulitafakuri vizuri sana kama kweli tunataka kuijenga nchi yetu iwe nzuri na iliyopendeza kwa mipango mizuri ya ramani hili tulifikiri vizuri sana suala hili.

Mhe. Spika, kuna baadhi ya Wajumbe wa Baraza hili waliwahi kupewa na wao shahada za kumiliki viwanja vile ambao kwa sababu hazijawekwa ramani pale chini ya ardhi mpaka leo hawajapata viwanja hivyo. Tumekwamba hapao Mhe. Spika, kwa hivyo sisi tunaendelea kuwasihi watu wa sehemu zile wakubali tufanye utaratibu. Waheshimiwa Wajumbe nakuombeni anayetaka kuendelea kusubiri asubiri tutakapokubaliana, tunawaomba Waheshimiwa Mshimba na wenzao watusaidie kwenye maeneo yale. Anayeona bora pesa zake arejeshewe basi naaje achukue. Kwa wale ambao wamekwisha kulipa. Hatuna njia nyengine lakini bado tunasema ni vizuri tufike mahala tukubaliane kwamba lile eneo tulipange vizuri na wao watapata humo humo humo humo viwanja vyao.

Mimi nashukuru sasa hivi sehemu zote zilizopita barabara watu wanajenga majumba ya maana kweli kweli sasa hivi. Ukenda Uroa kuna mabadiliko makubwa sasa hivi, wamejenga nyumba wametoka kule pwani wamekuja juu huku wamejenga nyumba nyuri nzuri kabisa kunavutiwa ukenda Marumbi sasa hivi kunavutia, lakini ndio wamejenga kiholela, ikipita njia hii unatokea uwani, ukipita njia hii unatokea jikoni, ukipita njia hii unatokea wapi. Sasa huo ndio ujenzi gani, jamani tupangeni hili ni suala muhimu.

Mhe. Spika, kuna hoja ya Mhe. Mtando hapa aliyozungumza juu ya suala la mpaka baina ya Potoa na Muwange. Mipaka ya shehia ni mipaka ya kiutawala na kuwekwa na kuondolwa kwake kunaratibiwa na Afisi ya Rais na Mwenyekiti, wa Baraza la Mapinduzi. Bahati mbaya sana mipaka hii haijawahi kuwekwa ardhi ingawa inajulikana kimantiki ya utawala.

Mhe. Spika, zipo sheria nyingi za zamani ambazo zimekatwa na kugaiwa kwa shehia mbili tofauti. Bahati mbaya katika ukataji huo Wizara yangu haihusishwi wala kupewa habari ya azma ya ukatwaji na hata matokeo yake. Lakini pia hakuna vielelezo vinavyoongoza ukataji wa mipaka wa shehia unakuwaje. Wizara husika pamoja na masheha wao wanakubaliana wapi waweke mipaka yao mipya.

Kwa kuwa wizara yangu haihusiki na maamuzi ya mipaka ya shehia na wala hakuna ramani inayoonesha wapi mpaka wa shehia mpya umepita inakuwa ni vigumu kwa idara ya upimaji kwenda kuonesha mpaka usio na vielelezo lakini pia ukati wa ugomvi baina ya shehia jirani. Idara ya Upimaji ina uwezo wa kurudisha mpaka kwa usahihi katika sentimita tano ikiwa mpaka ule upo mwanzo ilishiriki kuupima, yaani ile mipaka ya zamani iliyopimwa wanaweza kuirejesha.

Napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Mkwajuni kuwa mpaka wa Shehia ya Potoa na Muwange haukuwekwa na Idara ya Upimaji na wala hakuna taarifa za kiramani za mpaka huo. Kwa maelezo ya idara yangu haitoweza kutatua tatizo lililojitokeza la mpaka huo. Namuomba Mhe. Mwakilishi kwanza atafute suluhu na makubaliano ya pamoja baina ya masheha wa shehia hizo na baadae washukuru kupewa mpaka utakaokubalika.

Mhe. Spika, zamani tatizo kama hili likitokea Wazee wa ile nchi wanakubaliana mara moja na mpaka unapatikana mara moja. Wazee wenyewe sasa ndio sisi, wale wazee wa zamani kina Mzee Duni hawapo tena. Sasa sisi ndio wakurudi nyuma tukasema jamani hebu tukubaliane mpaka uwe wapi hapa katika hii Shehia yetu mpya, tukikubaliana tatizo haliji. Lakini tukijiengemeza katika upande mmoja tutakuwa tunasababisha matatizo kila siku. Mhe. Spika, hukuwa na nywele hizo, lakini sasa unazo, ndio uzee huo tena ushapiga hodi huo upo.

Mhe. Hamza Hasan Juma, amezungumzia suala la taasisi zake kupatiwa hati. Mhe. Spika, taasisi kuzipatia hati ni jambo la muhimu kabisa na nnatoa, hata juzi nimesaini baadhi ya hati ya baadhi ya taasisi za kijamii kama hospitali, skuli, wakati Bajeti inaendelea. Kwa hivyo nafikiri Mhe. Hamza hilo sio tatizo kubwa kusema kweli, hati unaweza ukaipata wakati wowote. Nakuomba nipe nafasi niifanye hiyo kazi, nimeshazipa skuli chungunzima nimesha-*sign*, nishawapa kabisa isipokuwa kuna kanuni zake. Kwa skuli maadam si *private* yako mwenyewe, basi nitaiandika Wizara ya Elimu. Na kwa hospitali maadam si *private*, si yako mwenyewe, nitaiandika Wizara ya Afya katika hati maana hivyo ndio vitu vya kudumu. Hizi kamati za maendeleo zinakuwepo zinaondoka, lakini Wizara ya Elimu ipo, kiongozi yeyote keshajengesha skuli mahala akubali sasa hivi ile skuli iwe mali ya

Wizara ya Elimu, hiyo hiyo ni benki yake keshatanguliza mbele ya safari asiwe na wasiwasi, atakapokwenda zake huko basi atakuja kila siku ile hesabu yake inatuna tu, inatuna tu, kwani inatoka wapi hii, ile skuli ya Kwamtipura ndio inakuja hii. Unatolewa kwenye mazonge unatiwa kwenye raha, ndio kwa sababu ume-*gain* pale ndio umetanguliza basi, ukitanguliza basi mambo yanakuwa mazuri tu weye.

Kwa sababu kila siku inakuja hujui duniani itaendelea kubakia siku ngapi hii Mhe. Spika, kwa hivyo kila siku inaingia tu. Tena inaingia *interest* ya halali sio *interest* unayoipata kwenye FBME na kwenye PBZ, *interest* ya kweli kweli inakuwa inaingia pale, basi ushatanguliza usione tabu tena, wewe ukishafanya jambo zuri toa tena *sadakatul jaria* itadumu hiyo, maana binaadamu anaishi kwa hizo *sadakatul jaria* ndio anaendelea kuishi huko. Yaliyobakia yote hapa yote unaacha, ukiacha shamba watu wananyan'ganyiana, ukiacha nyumba watu wanauza wanagawana watu wanakuja kukaa bure mwenyewe hupo huna habari hupo. Kwa hivyo hilo Mhe. Spika, tutalifanya kwa zile skuli ambazo tutaziandikisha ambazo mtu kazitoa ni skuli kwa ajili ya kijiji kile pale tumeiandika Wizara ya Elimu, na kwa hospitali tunaandika Wizara ya Afya ndio tunaowakabidhi eneo lile. Basi Mwalimu Mkuu atatunza pale na itatunzwa pale basi hakuna tatizo lolote.

Mhe. Jaku amezungumzia suala la mgogoro wa ardhi kwamba kesi zimerundikana kwenye mahkama ya ardhi. Lakini Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria suala hili ameshalizungumza vizuri kabisa, na mimi ninamshukuru sana Waziri wa Katiba na Sheria kwa utaratibu alioufanya. Na aliposema kwamba pale Chaani, Gamba karibu watafungua mimi nimepata faraja sana, lakini ninampa habari vile vile kwamba na Mkoa wa Kusini, Koani nyumba aliyokuwa akitumia Mkuu wa Mkoa ile tayari inafaa kwa mahkama ya ardhi pale, na pale tufungue vile vile tuweze kuzisambaza hizi mahkama mimi nakubaliana naye kabisa.

Tatizo la ujenzi holela unaoendelea nchini na wingi wa mipango ya miji isiyoonekana matunda yake. Hili amelizungumza Mhe. Ismail Jussa, Mhe. Ali Salim Haji, Mhe. Suleiman Hemed na Mhe. Mgeni Hassan Juma. Wote wametoa hoja kuhusu hali mbaya ya ujenzi holela wa miji yetu, na wametaka kujua Wizara yangu italitatua vipi tatizo hili. Kama nilivyosema katika bajeti yangu ukurasa wa 19 asilimia 70 ya miji inajengwa bila ya mpangilio.

Ni kweli kama alivyosema Mhe. Jussa kwa maeneo ya miji yaliyojengwa miaka ya karibuni mfano Nyerere, Tomondo na kadhalika hayana mipangilio mizuri ukilinganisha na yale maeneo ya zamani kama vile Kwahani, Kidongochekundu, yaani ukikaa juu huku Kwahani unamuona mtu aliyekuwepo Kariakoo nyumba zimepangwa vizuri kabisa. Sasa ni kweli na

ndio maana tukaleta utaratibu huu wa mipango miji hivi sasa hivi. Lakini hili Mhe. Spika, nataka tukubaliane. Maana Mhe. Spika, mtu ukimpa kiwanja ukamwambia kiwanja chako hichi hapa ninakupa na mipaka yako hii hapa, anapatizama hapo patupu anasema aaa hapo si panaingia kioski hapo anatia kioski keshaiziba njia zamani, au anajenga ghala keshapaziba zamani, matokeo yake inapanguka tena ile miji hili ni suala la kukubaliana Mhe. Spika.

Suala la ujenzi holela una sababu nyingi ikiwemo sababu ya kukosa mipango mizuri na kuwa na usimamizi mdogo wa mipango miji tuliyonayo. Kwanza niungane na Mwakilishi ninafikiri kuwa tatizo hilo lipo, lakini niwahakikishie serikali kuwa imeliona hilo ndio maana serikali ya awamu ya saba ikaanzisha taasisi maalum ya mipango miji na vijiji ili kutafuta ufumbuzi wa kudumu na endelevu wa suala hili.

Aidha Wizara yangu kupitia Idara hii imeshaweka mikakati ya kulitatua tatizo hili. Wizara inajua ujenzi holela unasababishwa na kukosa mipango miji, mipango miji na matumizi ya ardhi au kuwa na mipango iliyopitwa na wakati. Ujenzi holela vile vile husababishwa na usimamizi mdogo wa mipango iliyoko. Kuziba mapengo hayo katika mwaka huu Wizara kupitia Idara ya Mipango miji imekusudia kufanya yafuatayo.

Kutengeneza mipango minne ya matumizi bora endelevu ya ardhi katika miji na vijiji mpango huu utatumika nchi nzima. Mpango huu utatumika nchi nzima vile vile na *master plan* ya mji wa Zanzibar na mji wa Chake Chake mipango hii ni kwa ajili ya miji hii mikubwa na matumizi ya ardhi, mipango hii ni kwa ajili ya vijiji vyote vya Unguja na Pemba, kwa sasa tunaanza kwa kijiji cha Nungwi Unguja na Mgelema kwa Pemba kama nilivyosema katika Wizara yangu. Kwa hivyo Waheshimiwa mstahamili tupate kidogo *pilot project* ionekane mahala pale sasa hivi pako katika sura gani namna patakavyoweza kubadilika.

Hapa naomba kujibu hoja nyingi ya Mhe. Mgeni kwa Idara hii ina mipango mingi, lakini haionekani matunda yake. Ukweli kuwa mpango pekee uliopo wa mji ni *master plan* wa mji wa Zanzibar mwaka 1982, hivyo mipango hiyo iliyotajwa katika ukurasa wa 23 wa bajeti yangu ni mipya kabisa au nimepitia mipango ya zamani sana.

Hebu tuutizame kidogo mpango wa 1982 aliouleta Mzee Aboud Jumbe, huu ndio uliosababisha pale Gulioni kusimama jengo la BOT, halafu pale mbele kusimama jengo la ZSTC ni mpango huu, na pale ilipojengwa ofisi ya umeme Gulioni vile vile ni mpango huu. Na zilikuwa nyumba zile zinyooke kutoka pale ziende kusini moja kwa moja mpaka Kariakoo zijipange pale, ndio

maana kuna nyumba nyengine pale sasa hivi zinajengwa na watu wengine. Sasa ilikuwa tupate mji wa namna kama ile, hivi sasa kutawanyika si barabara sasa hivi twendeni juu. Mzee Karume aliona mbali tena aliona mbali sana kwa kujenga nyumba zile pale. Nyumba moja inachukua fleti mia moja na inapunguza matumizi ya ardhi mtapata nafasi ya kufanya kazi nyengine za kilimo.

Hivi sasa hivi kama hatuna mipango tutashindwa hata pa kulima, tutakata minazi yote, mtu ukimwambia kama Magomeni palikuwa pana miembe pale sisi tulikuwa tunakwenda Magomeni kula embe pale, na mitofaa mingi ajabu leo imebakia miembe mingapi Magomeni pale, hakuna muembe hata mmoja yote imeshakatwa pale. Begamoja pamoja na kuwa iko Begamoja lakini ilikuwa nayo na miembe mingi kweli kweli sasa hivi haina yote tumeshaijenga, yote tumeshaikata pale. Kwa Mhe. Salum Ali palikuwa pakiitwa Muembebeni, wakati wa ujana wetu tunakwenda kukesha pale. Beni inapigwa Kisimamajongoo hapo ikifika saa sita watu wanabeba beni wanakwenda Muembebeni, Begamoja tunamalizikia huko wakati wa *ujaahil* Mheshimiwa.

Mhe. Fatma Mbarouk vile vile Wizara imjulishe lini njia iliyopangwa kuunganisha njia ya Amani na ile ya Magomeni itajengwa? Mhe. Spika, Wizara iko katika hatua za mwisho za kustawisha *master plan* ya mji wa Zanzibar, mpango huu utawekwa sawa na masuala yote ya matumizi ya ardhi ndani ya mji huu, ikiwemo suala la njia zote za miji. Aidha Wizara yangu inafahamu kwamba Wizara ya Mawasiliano na Miundombinu ina mpango mkubwa wa kujenga njia zote za mjini, kufanya hivi kutauokoa mji wa Zanzibar na tatizo kubwa na sugu la msongamano wa magari yenye kuhangaisha sana wakazi wa miji.

Mfano mzuri na hai uliopo sasa katika mji wa Dar es Salaam, kujiepusha na tatizo hili Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Miundombinu itahakikisha kwamba njia zote zinabakia na zinatengenezwa ili zitoe huduma nzuri. Na hii *operation* Wizara ya Mawasiliano imeshaianza hivi sasa, hivi wapo kwenye njia ya Begamoja pale wanaitia lami nayo kwa sababu ukikuta *traffic* imekuzidi Muembenjugu unachepuka unaingia pale. Na pale kwa Kassim Ali pale nayo tukiijenga ile, vile vile ukitoka pale foleni unachepuka unaingia njia ile pale zinasaidia sana njia hizi.

Suala la kituo chako cha Polisi Mhe. Fatma sisi tuko tayari kwa pale penye waya wetu tumsogeze kwa pembeni naomba azungumze na Kamati yake wakubali kituo kijengwe, lakini sio pale juu ya ule waya, ni hatari kujenga kwenye ule waya Mhe. Spika. Halafu ni hatari pia kuna mita fulani baina ya ule waya na unapotaka kuanza kujenga jengo jengine ni hatari vile vile. Hii

barabara inayotoka Makunduchi hewani mpaka ikaanguka pale,m hiyo ni joki ambayo uliipata kwa mtu mmoja aliizungumza siku moja mahala. Lakini kwa kweli tuko tayari kukusaidia kujenga kituo kwa kusogea upande pale karibu na *branch* unaweza kujenga kituo chako pale, lakini hakitakuwa kikubwa pengine kama vile ulivyokwisha kujipanga mwenyewe.

Mhe. Spika, Mhe. Mohammed Raza amezungumzia juu ya kiwanja cha mfalme wa UAE kupatiwa muwekezaji, hoja hii ilitolewa na Mhe. Mohammed Raza, kiwanja hicho kilitolewa kama masharti ya kawaida ya ukodishwaji wa ardhi. Kwani utumiaji wa ardhi kwa mgeni ni lazima uwe kwa mkataba wa ukodishaji ardhi na sio kwa zawadi. Hivyo kinachosemwa hapa ni *land lease agreement* iliyopewa *Sheikh Zeid Al Nahyan* hapo Pwani mchangani kwa mujibu wa sheria za haki za matumizi ya Ardhi namba 12 ya mwaka 1992. Mkataba huu ulifutwa baada ya muda wa masharti ya uendelezaji kupita na kulipia kodi ya ardhi eneo hilo kwa sasa limekodishwa muwekezaji mwengine.

Mhe. Spika, tunataka kuleta sheria katika Baraza la Wawakilishi tufanye *amendment* ya sheria ya ruhusa ya matumizi ardhi. Unajua kuna watu wengine wanachukua ardhi wanakaa nayo kwa muda mrefu bila ya kuitumia. Sasa watu wengine wanatafuta yeye amekaa muda mrefu, kwa hivyo mimi ninafikiri sheria tuifanyie marekebisho ili tujue kama kiwanja kimetumika basi kiwe katika hali gani, hilo ndio suala muhimu kusema kweli.

Halafu Sheikh Ali Salum alizungumza suala la kiwanda cha Maruhubi eneo la Maruhubi, la ali muradhi kufutiwa na kupewa mkataba wa ukodishaji wa ardhi wa *Zanzibar Dar Product* hoja hii imetolewa na Mhe. Ali Salum Haji wa Kwahani. Suala hili ufumbuzi wake umeshapatikana na ali muradhi ameshapatiwa eneo jengine na pale pataendelea na mradi mwengine.

Mhe. Mgeni Hassan Juma alitoa maoni yake kwamba kuna ukosefu wa uratibu, *coordination* ndani ya taasisi za serikali kunakowezesha baadhi ya wananchi kukiuka taratibu na sheria zilizopo. Mhe. Spika, wazo hili tunalichukua na sisi watendaji itabidi tuelezane juu ya suala hili kwamba ni kweli tuwe tunaelewana baina ya taasisi na taasisi, na mtu akifanya umjue kwamba huyu kafanya makusudi huyu kafanya vipi.

Ukodishaji wa ardhi kwa mujibu wa sheria, haki ya matumizi ya ardhi *rent act* namba 12 Waziri amehusika kukodisha ardhi na pia kufuta ukodishaji huo. Aidha ufutaji wa mikataba hauzingatii matakwa ya utawala bali huzingatia kukubalika kwa sheria husika. Kifungu cha 48 (1) ndicho kinachompa mamlaka Waziri kufuta mikataba ya uondoshaji wa ardhi ikiwa mkodishaji kashindwa kuendeleza ardhi hiyo kwa kipindi cha miezi 30

kuanzia tarehe iliyopatiwa hati kama analipa kodi ya ardhi. Na inasema *for fail by the holder of such lease to complete development of lease land within a period of thirty month from the date of granted the lease.*

Kushindwa kuendeleza ardhi hiyo kwa mujibu ya masharti ya uwekezaji yaliyokubaliwa na ZIPA au taasisi nyengine zilizowasilishwa Waziri wakati wa kuomba mkataba huo wa ardhi. Kushindwa kulipia ada kwenye *shadow* ardhi kila mwaka baada ya muda wake kwa msamaha kumalizika. Kushindwa michoro yake kwa zaidi ya miezi sita, michoro hii ikiwemo *site layer out, typographic the map, water suppy, plant sections and elevence of the all proposed structure*. Muwekezaji akivunja masharti ya mkataba au sheria ya nchi.

Mhe. Spika, hili lilitolewa na Mhe. Hamza Hassan Juma ambalo nimeona nilisome kidogo na Mhe. Mshimba Mbarouk na Mhe. Hija kwamba ukodishwaji kwa kweli una muda wake. Na mimi ninawasihi wakubali kwamba tufate ule muda wa ukodishwaji kama mtu hajapatumia basi uzuri bora apewe mtu mwengine tufate hivyo.

Mhe. Spika, kufutwa mkataba wa ardhi ya muwekezaji anayelipa dola za Kimarekani 11,565 na kupewa kwa muwekezaji mwengine anayelipa dola za kimarekani 5,000 na dola za kimarekani 13365 na kupewa muwekezaji mwengine aliyelipa dola za kimarekani 3000 hoja hii imetolewa na Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Makame Mshimba, na Mhe. Hija Hassan.

Mhe. Spika, mnamo tarehe 7 Novemba, 2006 kampuni inayoitwa *Saco Pandri Resort* na *Severing Sandry Resort* zilizokodishwa ardhi hapo Kizimkazi kwa mkataba wa ukodishaji ardhi wenye nambari ya usajili DP No. 781 2006 na DP 78 2006 kwa muda wa miaka 33, maeneo hayo yana wastani wa ukubwa wa ekta 2.57 na hekta 2.97 zilizokodishwa kwa ajili ya ujenzi wa *hotel complex*. Hata hivyo mnamo tarehe 1/2/2012 mikataba hiyo ilifutwa rasmi na barua yenye kumbukumbu namba MUNA 29/3/C Vol. MUNA 23/3/C/100/Vol zinahusika. Baadae Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilikodisha eneo hilo kampuni ya *Coconut Resort* mnamo tarehe 28 Februari eneo lenye ukubwa wa hekta 2.5 kwa malipo ya ardhi ya dola ya kimarekani elfu tano.

Aidha kampuni ya *Saco Pams Resort* zilishindwa kuyaendeleza maeneo hayo kwa zaidi ya miaka 4, kitendo hicho ni kinyume ya kifungu cha 48(1) a.b.c. Aidha muwekezaji wa sasa yaani *Coconut Resort and villars Ltd* ametakiwa kulipa deni la 5,000 kila mwaka kwa viwango vya uwekezaji wazalendo. Kuna masharti ya wawekezaji wazalendo wanapunguziwa bei wao hawapewi ile ile ambayo muwekezaji mgeni. Kudaiwa kupaswa kulipa dola 500 kwa kila hekta moja kwa mwaka. Kwa vile kwa muwekekezaji wa sasa kampuni

ya *The address* amepewa dola za kimarekani kila mwaka kwa viwango vya wawekezaji wazalendo *local investors,* yaani hupaswa kulipa dola 500 kwa kila hekta moja kwa mwaka.

Hata hivyo kwa kuwa muwekezaji wa kampuni ya *saco pams* wamefungua kesi namba 71ya tarehe 28 Mei, katika mahkama ya ardhi dhidi ya kampuni ya *coconut resort and villars* inayomiliki eneo hilo, kwa sasa Wizara yangu haipaswi kulitolea uamuzi, hili suala liko mahkamani Mhe. Hamza kwa hivyo tungojee mahakama wamalize.

Kwa ufupi kigezo kikubwa cha viwango vya kodi au kupangwa kwa kuangalia aina ya wawekezaji, kwani kuna wawekezaji wageni na wenyeji. Hivyo vyombo vya wawekezaji wazalendo ni kidogo ukilinganisha na vyombo vya wawekezaji wageni kuwa ni vikubwa.

Kufutwa kwa mradi wa *leisure coup* Muyuni. Mhe. Spika, mnamo tarehe 17 Mei 2007 kampuni inayoitwa leisure *Coup LS Dubai World Al Nakhil* ilikodishwa ardhi hapo Matemwe Muyuni kwa mkataba wa ukodishaji ardhi wenye DP namba 804 kwa muda wa miaka 49. Eneo hili lina wastani wa ukubwa wa hekta 76 na lilikodishwa kwa ajili ya wa *hotel complex*. Eneo hili lilitakiwa kulipa kodi ya ardhi ya dola za Kimarekani 19,000 kwa mwaka. Hata hivyo mnamo tarehe machi, 2001 mkataba huu ulifutwa rasmi. Kwa mujibu wa sheria ya ardhi ya mwaka 1992 muwekezaji hupewa kipindi cha msamaha wa kodi cha miaka miwili na nusu tangu kusainiwa kwa mkataba wake. Hivyo Mhe. Waziri aliona iko haja kuufuta mkataba huo kutokana na kushindwa kuliendeleza eneo hilo kwa muda wa kipindi cha miaka 4.

Baada ya kufutwa kwa eneo hilo serikali ya mapinduzi ya Zanzibar ilizikodisha kampuni tatu tofauti nazo ni kama zifuatazo:

Peneral limited Ilikodisha ardhi mnamo tarehe 20 Disemba, eneo lenye ukubwa hekta 47.49 kwa malipo ya kodi ya ardhi dola za kimarekani 95,000 kwa mwaka.

Eucas limited ilikodisha ardhi mnamo tarehe 16 Novemba eneo lenye ukubwa wa hekta 18.28 kwa malipo ya kodi 45,600 kwa mwaka.

Ald Resort limited ilikodishwa ardhi mnamo tarehe 2 januari, eneo lenye ukubwa wa hekta 8.1 kwa malipo ya ardhi ya dola za kimarekani 24,500 kwa mwaka. Aidha eneo hilo halikukodishwa kwa kampuni nane ambazo ni hewa, bali yalikodishwa kwa kampuni tatu kama nilivyozitaja hapo juu, ambao ukijumlisha huko kuna dola 95 kwa mwaka, kuna dola 45 kwa mwaka na

kuna dola 24 kwa mwaka hicho ndicho kipato chetu sasa hivi katika kiwanja hiki.

Kuhusu kufutwa kwa ukodishwaji ardhi kwa kampuni ya *Sunset Paradise* hapo Kama, mkataba wa ukodishaji ardhi ulitayarishwa tarehe 4 katika eneo la Kama lenye ukubwa wa hekta 6.2 kwa ajili ya ujenzi wa hoteli ya kitalii. Muwekezaji ni mgeni hivyo alipaswa kulipa dola za kimarekani 39,000. Hata hivyo tarehe 7/3 mkataba huu ulifutwa rasmi kwa barua yenye kumbukumbu nambari hiyo hapo, kwa sababu muwekezaji huyo alishindwa kuliendeleza eneo hilo kwa muda wa miaka miwili na nusu kama ilivyooneshwa katika mkataba wake wa eneo hilo, na amekodishwa muwekezaji ambaye amepangiwa kulipa dola za kimarekani 2500 kwa mwaka. Huyu ni mzanzibari.

Utayarishaji wa utoaji wa hati miliki ya matumizi ya ardhi hoja hii ilitolewa na Mhe. Mgeni, utayarishaji wa utoaji wa hati za haki na matumizi ya ardhi baada ya kubaini kuwa wananchi wengi hawaelewi uwepo Afisi ya Mrajis wa Ardhi. Wizara imechukua hatua ya kuonana na Mrajis wa nyaraka na kuelezana mipaka, majukumu ya kila taasisi *register of document*. Vikao hivyo vimeanza kuzaa matunda na kwa sasa matatizo hayo yameanza kupungua, wananchi wengi sasa wanakuja kwa Mrajis kwa ajili ya kupata hati za usajili.

Mashamba ya Selemu na Kijichi wamepewa viongozi, hoja ilitolewa Mhe. Mwanaidi na Mhe. Shawana. Mhe. Spika, malalamiko ya Selem ni ya muda mrefu sana na wananchi pale wanapata tabu sana kwenye masuala haya. Mheshimiwa tunaamua sisi Serikali sasa hivi, Wizara yangu inaamua kwamba nadhani ni vizuri waliopata ardhi katika sehemu hii waturejeshee ardhi yetu na wabakie na eka tatu tatu. Kwa hivyo ni vizuri wakachague eneo ambalo wanalipenda wachukue eka tatu, zilizobakia tuendelee kuwagaia watu wengine pale. Hilo ndio suala muhimu kusema kweli juu ya uamuzi huu. Tupunguze migogoro ya ardhi sisi wenyewe hakuna mtu atakaekuja kutupunguzia migogoro ya ardhi hapa, ni sisi wenyewe.

Baada ya agizo la Mhe. Rais kuagiza utatuzi wa migogoro ya ardhi, ni migogoro gani imepata ufumbuzi, hoja hii imetolewa na Mhe. Shawana Bukheti Hassan Jimbo la Dole. Eneo liko jirani ya hoteli ya *Resident* Kizimkazi Mkoa wa Kusini Unguja, mzozo ulikuwa baina ya wananchi na Kamati ya maendeleo ya Jimbo kwa kushirikiana na uongozi wa Mkoa. Pande zinazohusika tulizikutanisha na kuwapa taaluma na kuwa ardhi waliyokuwa wakigombea ni mali ya serikali. Tuliwaongoza kuwa anayehitaji ardhi hiyo alete ombi lake Wizarani kwa mazingatio, na kwa sasa tatizo la mgogoro huo umeshamalizika.

Kuhusu bodi mbali mbali za Wizara hii kumalizika muda wake hoja hii ilitolewa Mhe. Salum Abdalla naomba niwajibu Wajumbe katika wizara hii, ni kweli kwamba bodi nyingi zimemalizika muda wake, nimekuta karibu bodi zote hapa zimemalizika muda wake na sasa hivi ndio naziunda upya.

Mhe. Mwenyekiti nikitizama saa pale naona muda umekwenda sana, na tunaweza tukashindwa kupitisha mafungu, maana nadhani kuna mabuti mengi hapa. Sasa nawaomba radhi wale ambao kwa bahati sijagusa hoja zao, nawaahidi kwamba hizo hoja nimezichukua na nitazifanyia kazi. Lakini nataka nizungumze mambo mawili makubwa.

Jambo la kwanza ninalotaka kulizungumza hapa Mhe. Spika, juu ya suala la uundaji wa kamati teule. Mhe. Spika, Wizara yangu hata haina tatizo kuundwa kamati teule kabisa. Ofisi yako Mhe. Spika, ninakubali kabisa iunde kamati teule ya kuchunguza migogoro hii ya ardhi, lakini ipatikane hadidu rejea zitazoondoa muingiliano baina ya kazi inayofanya mahkama na kazi itakayofanywa na kamati yako. Baadhi ya migogoro Mhe. Spika, iko mahakamani, si vizuri kuchukua mgogoro uliofika mahakamani ukauleta huku. Kwa hivyo panahitaji kufanywa utafiti, Ofisi yako ifanye utafiti kabisa una Wajumbe wengi tu hapa juu ya mambo gani yashughulikiwe katika kamati teule hii juu ya suala la migogoro ya ardhi tusiingiliane na taratibu za kimahkama ambazo zinaendelea kufanywa. Hilo wizara yangu haina tatizo kabisa.

Kuna suala ambalo nimeombwa sana mimi hapa kwamba nilete sheria juu ya suala la mafuta (*petrol)*, uchimbaji na utafutaji mafuta na gesi asilia. Mhe. Spika, mimi wala si mkaidi hata kidogo. Wasiwasi wangu nina katiba mbili mkononi mwangu hizi hapa, na mimi katika kufanya kazi hii nimeapishwa na nikapewa katiba hizi.Mimi Mhe. Spika, sio ninayekuja kuapa huja na udhu hapa mimi, baadhi ya kinamama wananitania leo nadhani hutaki kupewa mkono na tukiondoka pale je, ushaapa sasa hivi tukusalimie basi. Siku nyengine hata siku kama hizi hakuna kiapo hunambia leo vipi mkono unautaka, kwa sababu siku ile Mhe. Spika, huwezi kucheza na kitabu takatifu cha *qur-an* kuja kula kiapo bila ya kuwa na udhu, ukikichezea kitabu kile kwa nini? Ile maana yake unataka kukubali kwa kula kiapo kwa kutekeleza vyombo hivi ambavyo vimetengenezwa, vikirekebishwa maana yake nimeshapata mwanya wa kwamba nitatumia hivyo vilivyorekebishwa sasa hivi. Lakini kama havijarekebishwa hivi si rahisi kufanya kitu kwa mujibu wa katiba wakati umeapa kwamba utailinda, ikawa ndio umefanya jambo la maana hujafanya la maana bado.

Mhe. Spika, katiba ya Muungano kifungu cha nne kinasema, ‘shughuli zote za mamlaka ya nchi katika jamhuri ya muungano zitatekelezwa na kudhibitiwa

na vyombo viwili vyenye mamlaka ya utendaji, vyombo viwili vyenye mamlaka ya utoaji wa haki na pia vyombo viwili vyenye mamlaka ya kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma. Hicho 4 kifungu kidogo cha kwanza. Kinasomeka hivi, vyombo vyenye mamlaka ya utendaji vitakuwa ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Vyombo vyenye mamlaka ya utoaji haki ni mahakama ya serikali ya jamhuri ya muungano na mahakama ya serikali ya mapinduzi ya Zanzibar. Na vyombo vyenye mamlaka ya kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma vitakuwa ni Bunge na Baraza la Wawakilishi, chombo chetu hiki hapa. Ukiisoma katiba hii kwenye kifungu cha 64 Mhe. Spika, ninakwambia juu ya sheria juu ya mambo mengine yoyote kuhusu Tanzania Bara itakuwa miongoni mwa Bunge sawa. Kifungu cha pili kinasema mamlaka yote kwenye sheria katika Tanzania Zanzibar juu ya mambo yote yasiyokuwa ya Muungano yatakuwa mikononi mwa Baraza la Wawakilishi, sawa sawa. Endapo sheria yoyote iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi inahusu jambo lolote katika Tanzania Zanzaibar ambalo liko chini ya mamlaka ya Bunge, sheria hii itakuwa batili na itatenguka, na endapo sheria yoyote iliyotungwa na Bunge inahusu jambo lote ambalo liko chini ya mamlaka ya Baraza la Wawakilishi sheria hii itakuwa batili na itatenguka. Hiki ndio kifungu ninachokizingatia mimi katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano.

Lakini ukija katika katiba ya Zanzibar toleo la 2010 kifungu cha 32 nacho kimesema kuwa hakuna sheria yoyote itakayopitishwa na bunge la muungano ambayo itatumika Zanzibar mpaka sheria hiyo iwe ni kwa ajili ya mambo ya muungano tu na ipitishwe kulingana na maelezo yaliyo chini ya vifungu vya katiba ya jamhuri ya muungano wa Tanzania. Kwa hivyo sisi tumezuia sheria inayohusu Zanzibar isitungwe kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano, na huku imesema imezuia kwamba isiwe inahusu mambo ya muungano isitungwe kwenye baraza la Wawakilishi na ikatungwa inakuwa batili.

Ninawaomba wenzangu, ninawasihi sana wenzangu, tena sana tuzingatie vyombo vyetu hivi ambavyo tumekula kiapo wakati tulipoingizwa katika chombo hiki, ninawaomba sana. Kuna *development* Mhe. Spika, nimeipata mimi baada ya kufatilia masuala haya kwamba ile miezi 4 tuliyoahidiwa kwamba *cabinet* ijayo kwamba suala letu hili ambalo limeshaazimia hapa linapelekwa katika *cabinet* ya Jamhuri ya Muungano. Tungojee majibu baada ya kipindi kifupi kutoka *cabinet* ya Jamhuri ya Muungano. Ninawasihi wenzangu sana tusikoroge vyombo vyetu hivi ambavyo vimetungwa na sisi wenyewe na zimepitishwa na sisi wenyewe, na tuvilinde kama tunavyosema kwamba tutavilinda wakati tunapokula kiapo.

Mhe. Spika, haya ni mambo ambayo nimeyazungumza, nawasihi wale wenzangu wote ambao walikuwa wametoa hoja zao lakini sikuzijibu ni kwa sababu ya wakati, nakimbilia ili tuwahi angalau kupitisha mafungu kidogo hapa, na nawaomba tena kwa mara nyengine tena mimi ni mgeni. Hii kazi yenyewe sijaianza mnanihukumu jamani *nyee*! Maana angalau ingekuwa nimeianza mkasema aa wewe tumekuona bwana, mimi ndio kwanza ninaanza hebu nipeni nafasi niifanye hii kazi jamani. *(Kicheko)*

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Waziri ametoa hoja, kwa maana hiyo tufanye uamuzi na ili kupata uamuzi basi sasa Waheshimiwa Wajumbe niwahoji wale wanaowafiki hoja hii ya Mhe. Waziri ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa mwaka 2012/2013 wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kukubali hotuba ya bajeti ya wizara yangu, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kupitisha vifungu vya matumizi vya wizara yangu.

KAMATI YA MATUMIZI

Fungu 25 Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati

Kifungu 0301 – Ofisi Kuu Pemba Shs156,000,000

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nahitaji muongozo wako, katika Fungu hili la 25 ambalo ni mapato, haya nilihoji juu ya Mamlaka ya Maji wanavyodaiwa sana na *ZECO*. Sasa nilitaka hapa nitafute kifungu kinachohusiana na hiyo ili nihoji, lakini bahati mbaya katika mtiririko wa mafungu katika fungu hili *ZECO* haikuainishwa ili nipate pahala niweke hilo swali langu. Sasa nahitaji muongozo wako hili hasa niende pahala gani.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Omar Ali Shehe anataka muongozo kwa sababu anataka kuhoji kuhusiana na madeni ya Mamlaka ya Maji sawa, ambayo Mamlaka hiyo inadaiwa na *ZECO* ambayo hapa vitu hivyo havipo. Kwa kawaida inapotokea suala aina hiyo tunakwenda kwenye utawala tunajenga

hiyo hoja, sasa kama utawala wenyewe ni Ofisi Kuu Pemba basi itakuwa ndio hapa hapa, laa utawala wenyewe ni Zanzibar, kwa maana itakuwa ni kwa upande wa Unguja. Sasa huo ndio muongozo ambao ningeweza kuutoa, kwa sababu vyombo vya mamlaka kimsingi ni kama mashirika, mambo yake yanakwenda kwa mujibu wa bodi zao, utaratibu wa kudaiana huwa hauonekani hapa na kwa kawaida hata matumizi yao yanapitishwa na bodi zao, lakini kama unataka kuuliza kitu basi ni kwenda kwenye utawala.

Mhe. Omar Ali Shehe: Sawa Mhe. Mwenyekiti, nitakwenda kwenye Utawala tuendelee.

Kifungu 0301 – Ofisi Kuu Pemba	Sh.156,000,000
Kifungu 0501 – Idara ya Ujenzi	Sh.7,000,000
Kifungu 0701 – Hifadhi ya Mji Mkongwe	Sh.24,000,000
Kifungu 0901 – Idara ya Ardhi na Usajili	Sh.3,505,000,000
Kifungu 1001 – Idara ya Upimaji na Ramani	

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, wakati nachangia nilihoji namna ambavyo nyumba zetu za maendeleo zinavyoendelea kuchakaa bila ya matengenezo, na nikasema kwamba Ripoti ya Mdhibiti na Makaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2008/2009 ilionesha kwamba kuna deni kubwa sana lililorundikana kwa wateja, ambalo hadi sasa kwa kweli Idara ya Nyumba imeshindwa kudai.

Hapa naomba niseme Mhe. Mwenyekiti, kwamba jumla ya fedha zote ambazo zilikuwa zinadaiwa asilimia 56 bado ziko mikononi mwa wateja. Katika asilimia hizo 56 asilimia 23 hazijalipwa kabisa, na asilimia 76 ziko katika hali ambayo haijulikani kwa sababu kuna watu wanasema kwamba nyumba zile wamepewa na Mzee Karume ambao wao hawastahiki kulipa. Sasa nikahoji kwamba Waziri aliunda Tume Maalum, tume hiyo imechukua muda mrefu mno zaidi ya miaka saba haijatoa ripoti. Nilimuuliza Mhe. Waziri atakapokuja atupe ufafanuzi je, ripoti ya tume hiyo itatolewa lini, ili tufike pahala tufanye uchambuzi kati ya wale wadeni ambao ni halali yao walipewa nyumba na Mzee Karume, na wale ambao wanatumia visingizio. Sasa nilimuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa kwanza haturidhiki kuwa tangu mwaka 2008/2009 hadi sasa kuwa kuna zaidi ya shilingi 36 milioni hazijalipwa, ni miaka mingi kuanzia mwaka 2008 mpaka leo mwaka 2012 ni miaka mingi. Sasa hizi 36 milioni zitalipwa vipi?

Kwa sababu humu humu katika ripoti Baraza hili limeombwa liidhinishe fedha kwa ajili ya matengenezo, sasa hatuwezi kuidhinisha fedha wakati fedha zipo, lakini wanashindwa kudai. Kwa hivyo, nilijenga hoja kwamba hizi shilingi 36 milioni zitalipwa vipi.

Lakini vile vile shilingi 118 milioni ambazo ziko katika mabano hazijulikani uhalali wake, ambazo hizi zitatokana na ile ripoti ya tume ya Mhe. Waziri, lini tume hii italeta ripoti yake, ili tufike pahala tuangalie ule uhalali wake wanaopaswa kulipa walipe na wanaopaswa waendelee kukaa kwa heshima ya Mzee wetu waendelee kukaa. Kwa hivyo nahitaji maelezo hapo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Nafikiri Mhe. Omar hilo tulizungumzie kwenye Idara ya Nyumba na Makaazi, nafikiri hapo ndipo penyewe, hii ni Idara ya Upimaji. Sijui kama ulikusudia hapo.

Mhe. Omar Ali Shehe: Ndio tuko hapo. Ah! Nilifikiri tuko kwenye kifungu 1101.

Mhe. Mwenyekiti: Bado kidogo tu, nitajitahidi nisisahau nikwite.

Kifungu 1001 – Idara ya Upimaji na Ramani Sh.250,000,000
Kifungu 1101 – Idara ya Nyumba na Makaazi

Mhe. Omar Ali Shehe: Sasa Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo yangu yarudiwe ili Mhe. Waziri anijibu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri maelezo ndio yale aliyoyatoa mwanzo tumpatie maelezo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, hoja yake nimeikamata vizuri sana na ni hoja ya maana sana, kusema kweli na tunaihitaji kuifanyia kazi. Zile *data* ambazo ananipa yeye mimi sina, lakini nachukua kwake kama ndo taarifa na ninamuhakikishia kwamba hii kazi nitaifanya mimi *Inshaallah* Mwenyezi Mungu akipenda.

Kuhusu ripoti ya wale ambao hawalipi kwa sababu wanasema wamepewa nyumba na Marehemu Mzee Karume, hiyo ripoti Mheshimiwa tayari imeshafika ofisini na ilikuwa nataka tupate nafasi kidogo tuijadili kwenye Kamati ya Uongozi, ili kuipeleka katika vyombo vya juu kwa ajili ya kufanyiwa kazi. Kwa hivyo, iko tayari keshaikabidhi Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi ambaye ndiye Mwenyekiti. Kwa hiyo tutaipata hiyo ripoti tutaifanyia kazi halafu baadae tutaipeleka panapohusika, asubiri kidogo anipe muda.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri aliyepita naye aliniahidi hivyo hivyo kwamba ripoti iko tayari na naomba niseme kwamba

tangu mwezi Julai tuliambiwa ripoti itakuwa tayari na itatolewa, lakini hadi sasa bado. Hebu Mhe. Waziri kwa sababu ripoti tayari, na kwa sababu hoja hii ni ya Kamati ya *PAC,* hebu naomba unipe muda kama lini wizara yako au wewe mwenyewe utakaa pamoja na kamati katika kukabidhiwa ili tuone kwamba sasa tunakwenda pamoja.

Kwa sababu narudia kusema kwamba suala hili ni la zamani, na tulipokwenda Idarani tuliambiwa Julai, Julai ikapita, Agosti ikapita, Septemba, Disemba ikaja nyengine, sasa hapa naomba hasa, kwa sababu Mhe. Waziri ni mpya nakubaliana naye, lakini naomba tu katika hili tuliunganishe basi na Kamati ya *PAC* ili tukae pamoja mimi na yeye hapo atakapokabidhiwa, tuone kwamba sasa ishakabidhiwa ili twende pamoja.

Lakini lile suala la takwimu nasikitika kwa kweli, kwamba ikiwa jana nilizungumza hivi na Mhe. Waziri ndio kwanza anapata *data* hapa, nilitegemea baada ya kuzungumza vile wataalamu wake watampa hizi *figure*, kwa sababu hizi *figure* ndio nilizitayarisha hapa. Sasa ikiwa Mhe. Waziri ndio kwanza unazipata uone kwamba watendaji wako jana hawakukusaidia. Kwa hivyo, chukua *data* hizi mimi nakubali na uzifanyie kazi. Kwa maana hiyo baada ya kukubaliana hivyo naona Mhe. Waziri anijibu hilo halafu tuendelee.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, kama atakubaliana na mimi kwa kuwa sasa niko kwenye bajeti hapa, na si vizuri wenzangu wanaendelea na bajeti zao mimi nikajitenga nikawa sipo, kwa hivyo hii kazi niifanye mwezi wa nane. Kumi la kwanza mwezi wa nane nikae na Kamati yangu ya Uongozi tuipitie hii ripoti, sijui kama Baraza litakuwa bado lipo wakati huo au limeshaondoka, lakini baadae ndio niilete panapohusika. Nakubali kabisa kwamba kumi la kwanza mwezi wa nane nitaishughulikia ripoti hii Mungu akipenda kabla hatujaingia kwenye vuguvugu la sensa.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, kwa uzee wa Mzee wetu yule na kwa upya wake mimi nakubali tuendelee.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na wakati sina nia ya kuzuia kifungu, lakini katika kuchangia kwangu yale yangu mimi mwenyewe niliyoyaeleza aniachie, lakini nilimwambia Mhe. Waziri kwamba nitahitaji orodha ya nyumba zote alizozijenga Marehemu Karume za Mijini na Vijijini, na nyumba hizo zilizokodishwa ngapi, zilizokuwa hazikaliwi ngapi, mbovu ngapi na hali yake halisi ilivyo. Lakini sikujibiwa katika mchango wangu neno hata moja, naomba basi hili Mhe. Waziri anipe taarifa kwa sababu na huko nyuma niliuliza swali mimi.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, kweli Mhe. Bi Asha alizungumza suala hilo lakini mimi nililikamata nusu, nilikamata zaidi nyumba ambazo bado ziko mikononi kwa viongozi ambao wameshastaafu na hawako kwenye shughuli za uwaziri tena, ambayo hiyo nilipozitafuta nikapata ni nyumba 14. Hizo ndizo nilizozipata na watu hao wote nimeshawaandikia barua ili watupishe katika nyumba hizo tufanye matengenezo ili tuweze kuwaweka Waheshimiwa wengine. Hili la nyumba za vijijini zote Unguja na Pemba sikuwahi kuifanya hesabu hiyo Mhe. Mwenyekiti,

Nakubaliana naye kabisa, lakini ni hesabu ambayo inahitaji muda na ndio nikasema katika mambo haya kuna mambo lazima uyafanyie utafiti kwa kweli, lakini najua kwamba Nyumba za Maendeleo nyingi za vijijini haziko katika hali nzuri. Mimi nimekubali wito wake kwamba zile Nyumba za Maendeleo zinataka kufanyiwa mkakati maalum wa kufanyiwa matengenezo, kwa sababu nikipita naziona kwamba haziko katika hali nzuri.

Kwa hivyo, nakubali matamshi yake kuwa zile nyumba haziko katika hali nzuri kusema kweli. Sasa kweli zimo nyumba mle zimeuzwa kihalali, kuna nyumba zimeuzwa kwa vilemba, watu wametoa vilemba wameziuza zile nyumba, kuna nyumba wameuza kwa sababu ilikuwa ni mali yao. Sasa hii inahitaji utafiti wa muda sio kwa ghafla. Kwa sababu kuna watu Mhe, Mwenyekiti, katika nyumba zile alilipwa kwa nyumba yake iliyovunjwa Vikokotoni lakini ni yake kaiuza, lakini ndani ya *block* lile kuna nyumba katika nyumba zile alipewa mtu akae akaichukulia kilemba.

Katika nyumba zile zile kuna nyumba mtu alikuwa ameazimwa kama Afisa wa Serikali akae pale, lakini mpaka leo huna hakika kama kainunua au bado, ni masuala ambayo yanahitaji kufanyiwa utafiti Mhe. Mwenyekiti. Kwa hivyo, mimi nimeona kwa hili anipe nafasi.

Kwa hilo la viongozi ambalo aliliuliza zamani hizi najua kwamba zipo nyumba ambazo bado ziko mikononi, ambazo hizo tunataka hawa wenzetu wakisikia masuala haya wazirejeshe hizo nyumba ili tuweze kuweka viongozi wetu.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, kwa imani kabisa na mimi niseme kwamba Mhe. Waziri na ninavyomjua mfuatiliaji, mtendaji nampa muda au anambie ni miezi mingapi basi mimi nitakubali mpaka kikao kinachokuja. Kwa sababu hizi nyumba ni nyingi na ni sehemu mbali mbali zinataka utafiti wa hali ya juu. Kwa hivyo, mimi namstahamilia mpaka kikao kijacho penye uhai na uzima, tutakuwa tumeshafunga Ramadhani hatuna matatizo aje kwa sababu nimetaka katika kikao hiki asinipe peke yangu

tuweze kujua kwenye Baraza hili, ni nyumba ngapi ambazo zimo katika hali nzuri. Kama alivyoeleza ameeleza vizuri sana, baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa sina nia lakini nilitaka angalau nifafanuliwe kidogo. Tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri maombi hayo kwamba jambo hili tulete taarifa kikao kinachokuja.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Nakubali Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu 1101 – Idara ya Nyumba na Makaazi	Sh.150,000,000
Jumla ya Fungu:	Sh. **4,092,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizibila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 25 Wizara ya Maji, Makaazi, Maji na Nishati

Kifungu 0301 – Ofisi Kuu Pemba	Sh. 995,000,000
Kifungu 0302 – Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba	

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru Mhe. Waziri kwa kujitahidi kutupa ufafanuzi wa hoja zetu mbali mbali ambazo tulizitoa hapa. Mhe. Mwenyekiti, bila ya kupoteza wakati katika mchango wangu kama alivyosema mwenyewe niligusia maeneo mengi, kuna maeneo ya mafungu utanisamehe Mhe. Mwenyekiti, yatapofika nilisema kwa jumla kwa sababu ukisema kimoja kimoja hukimalizi, lakini hapa sipo ninapotaka kwenda tukifika huko nitamwambia.

Hapa nililokuwa nimelizungumza *specifically* nilisema hizi hesabu alizotuletea hapa wizara watendaji wake ama wanakusudia kutudanganya au wanakusudia tuidhinishe matumizi yasiyokuwa halali.

Mhe. Mwenyekiti, fungu 0302 ni Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba na maelezo yake katika *vote* 263100 Ruzuku (*Transfers to other general government units, programs and..,* haikumalizika. Kwenye maelezo ya ziada ruzuku kwenye uendeshaji, *salvation for other charges* wameombewa shilingi milioni saba.

Lakini Mhe. Mwenyekiti ukifungua ukurasa wa 406 wa buku hili hili, kuna *vote* 1102 nambari tofauti Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba, kwa Kiingereza vile vile, *house rent control board,* maelezo ya fungu 263100

nambari zinafanana, ruzuku (*Transfers to other general government units, programs and..,*. Kwa Kiswahili kuna maelezo ya ziada pale 263102 Ruzuku ya uendeshaji *salvation for other charges* ni shilingi 30 milioni zinaombwa. Sasa Mhe. Mwenyekiti, huu sio utaratibu, idara moja ina *vote* mbili tofauti au *sub vote* mbili tofauti katika wizara, huku inaombewa shilingi milioni saba na huku inaombewa shilingi 30 milioni tukisema hapa kama kuna wizi tutakuwa tunakosea Waheshimiwa Wawakilishi na Mhe. Mwenyekiti.

Sasa nilimwambia jana Mhe. Waziri kwamba katika mafungu ambayo ninataka maelezo ni hili, kuna hatari nikayazuia yote mawili kwa sababu kukawa kote kuna wizi manake siwezi kujua hapa lipi lililokuwa sahihi la shilingi milioni saba au 30 milioni. Kwa hivyo, nilikuwa naomba kwanza anipe maelezo, kwa sababu hili hakuligusa kabisa katika majumuisho yake kabla ya kuendelea mbele. Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza nampongeza sana Mhe. Jussa kwa sababu hii kazi anayoifanya ndio kazi hasa inayotakiwa kufanywa katika masuala ya kulinda pesa za wananchi. Ni kazi nzuri sana kusema kweli. Kwa hivyo, namtanabahisha tu kwamba hii ya kwanza nataka nimfahamishe kwamba Bodi ya Kudhibiti Kodi ina sehemu mbili, Mwenyekiti ni mmoja lakini anaongoza watu wa sehemu mbili kuna Pemba na Unguja. Kwa hivyo, zile shilingi milioni saba ni za Pemba posho za wale watu wa Pemba, kuna na askari na watu wengineo wanaosimamia wakati anapoendesha Mahkama yake kule. Hii ya pili ni ya Unguja Mhe. Mwenyekiti, Mwenyekiti anaposimamia mambo ya Unguja ndio anatumia hii ya pili.

Kwa hivyo, mimi nampongeza sana kutanabahi katika masuala haya ni kazi nzuri sana anayoifanya Mheshimiwa Mjumbe.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, unajua labda niseme kitu kimoja pengine sijaenda katika hoja ya Mhe. Waziri. Mhe. Mwenyekiti nadhani unazo taarifa Baraza hili limeandikiwa tahariri mara mbili kipindi hiki kusifiwa kwa kazi nzuri inayofanywa, na hata kutakiwa Bunge la Jamhuri ya Muungano lijifunze vipi Baraza la Wawakilishi linafanya kazi ya kusimamia fedha za wananchi wa Zanzibar. Lakini hata Bunge limeambiwa lijifunze utaratibu anaotumia Mhe. Spika wa Baraza la Wawakilishi anapokuwa Mwenyekiti wa Kamati kuongoza utaratibu wa kupitisha vifungu.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nimesema hayo kwa sababu sisi tunapopitisha mafungu yanayotuongoza hapa ni haya, na utaratibu tuliouzowea ni ule aliosema. Kwanza hili nataka kulikemea na serikali ijirekebishe kuanzia mwakani. Inaonekana hakuna muongozo mmoja katika serikali unaoeleweka

au wizara haziheshimu muongozo mmoja unaotolewa na Wizara ya Fedha katika hili.

Mhe. Mwenyekiti, kuna wizara utakuta idara yake imejigawa Unguja na Pemba wakati muundo wa serikali yetu ule ule mmoja, sawa sawa na ofisi kila wizara ina ofisi Pemba lakini kuna wizara idara zake utakuta kuna fungu la Unguja mbali na la Pemba mbali, kuna wizara haifanyi hivyo. Sasa hii itatupa shida, halafu utakuja kukuta katika wizara moja kuna idara zimegawika Unguja na Pemba kuna idara zimewekwa pamoja tu. Sasa hili Mhe. Mwenyekiti, nalikubali kwa kumheshimu Mhe. Waziri tu, kwa sababu najua kauli yake ni kauli thabiti na namjua katika mawazidi ambao wanaweza ata nikiamshwa usingizini nikiambiwa kuwa nimlie kiapo kwamba hana tabia ya ufisadi na wizi mmoja Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban. Ni mtu ambaye katumikia muda mrefu katika serikali hii, na ana utumishi uliotukuka kabisa, sijawahi kusikia neno lolote dhidi yake, inaweza kuwa ni mengine kila mmoja na udhaifu wake hata mimi nina wangu Mhe. Mwenyekiti.

Kwa hivyo, nalikubali lakini nasema haya mambo yarekebishwe Mhe. Mwenyekiti, hatuwezi kuwa katika mabuku haya hakuna maelezo hayo halafu tunapokuja tunapewa maelezo ya mdomo kama hayo. Nalikubali tuendelee Mhe. Mwenyekiti, lakini nasema mwakani tukijaaliwa katika mambo mengi yajipange, vyenginevyo kuna hatari ya kuja kurejesha buku zima hili Mheshimiwa arudi tukasema tutakuja kukutana bajeti hapa mwezi wa Septemba ili tuwape miezi mitatu wakalisawazishe buku hili Mhe. Mwenyekiti. Baada ya hayo nasema Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 0302 – Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba Sh.7,000,000
Kifungu 0401 – Idara ya Mipango, Sera na Utafiti

Mhe. Hamza Hassan Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza Mhe. Mwenyekiti, nataka nimshukuru sana, sana, sana Mhe. Waziri na vile vile nataka nimshukuru sana, sana Mwanasheria Mkuu kwa kukubali kwamba sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuweze kusimamia yale mambo ambayo tumehisi kidogo yako kinyume kinyume. Sasa Mhe. Mwenyekiti, naamini baadae utatoa muongozo wako.

Baada ya shukurani hizo Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia lile suala la kwenye ardhi, siligusi tena kwa sababu Mhe. Waziri kashakiri na Mhe. Mwanasheria Mkuu kashatoa muongozo, lililobakia itakuwa ni kazi yako wewe Mwenyekiti. Hoja yangu inakuja katika Mamlaka ya Maji (ZAWA), nilieleza *concern* yangu kwamba Serikali inajitahidi sana, vingozi wetu wanahangaika sana, wakubwa wetu, Maraisi wetu kila wanapkwenda wnaomba misaada kwa ajili ya kuondoa shida ya wananchi juu suala la maji,

lakini ukija katika utekelezaji fedha nyingi zimeshatumika na bado tatizo la maji linaendelea kuwepo. Mhe. Spika mimi nilisema kwmba nataka tukachungulie na nafikiri ingawa Mhe Waziri suala hili hakulitolea kauli lakini tutakapokwenda kutafuta katika maeneo ya migogoro ya ardhi ambayo tunahisi kuwa haiko Mahakamani nadhani nahuku tukachungulie na sababu zangu ni hizi:

Mhe. Mwenyekiti naomba kw sababu kwanza Mhe. Waziri kutokana na muda kibanda kilichojengwa Kijitoupele nilipata taarifa kwamba kilijengwa kwa milioni karibu arobaini na hakunijibu, sasa kile atakuja kunitolea ufafanuzi lakini zaidi naomba nisome taarifa niliyonayo mkononi, sitaki nisome maelezo lakini nataka nisome ile taarifa yenyewe fupi ili tueleweke “kwa hivyo naomba kutuma ombi la maposho kama hivi ifuatavyo, na hapa wanaotakiwa kulipwa wala siwataji tunasitiri lakini nitataja *figure* pamoja na vyeo vyao na hapa ndio tutapata kulinganisha.

1. Meneja	600,000/= posho la kikao na haikuandikwa siku ngapi humu
2. Mhandisi wa mradi	450,000/=
3. Mhasibu	450,000/=
4. Manunuzi	450,000/=
5. Afisa elimu wa mradi	250,000/=
6. Afisa elimu ya jamii	250,000/=
7. Afisa mwengine	250,000/=
8. Afisa wa Afya	250,000/=
9. Msaidizi Mhasibu	250,000/=
10. Msaidizi Meneja	400,000/=
11. Mhandisi	400,000/=
12. Afisa kutoka sehemu nyengine	200,000/=
13. Afisa wa Elimu	200,000/=
14. Afisa wa Afya	200,000/=
15. Sekretari	150,000/=
16. Dereva	150,000/=
17. Dereva	150,000/=
18. Mhudumu	40,000/=
19. Mhudumu	40,000/=

Sasa maposho haya hii sio bodi. Matumizi haya ya fedha Mhe. Spika, ndio kidogo ambayo tunayo wasi wasi nayo, lakini na jengine katika hii miradi ambayo imejengwa nitaomba nisome baadhi ya maeneo ambayo utafiti unaonesha hatukufanikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, anasema kwamba miongoni mwa mambo ya kuanzia kufanya utafiti ni matangi ya maji, plastic yaani GRP kwa upande wa Unguja inaonekana yanatusumbua kwani matangi hayo yote yaliyojengwa yanavuja kupindukia, hadi kufikia kuacha kuyatumia, kwani yanaelekea kushinda kufanyiwa matengenezo ikiwa bado ni mapya kulingana na *life time* ya matangi hayo.

Mfano tangi la maji la Makunduchi, Bumbwisudi, Bwejuu, Ukongoroni na mengineyo. Lakini vile vile hivi karibuni tumefikia kulivunja kabisa tangi la GRP la Dundua na kujenga tangi jipya la zege.

Jambo jengine ambalo linalosumbua ni *pump* za kusukumia maji kwa upande wa Unguja zinaungua bila ya mpangilio, hali hiyo inaleta kurudisha nyuma kwenye maendeleo ya kazi nyengine. Kwani gharama za kununua ni kubwa hadi kufikia sasa mafundi wetu wa Mamlaka ya Maji Unguja wanatoa sababu ambazo hazifahamiki. Kwani kila siku wanabadilisha sababu za kuungua *pump* mara kwa mara.

Hali ni tofauti kwa upande wa Pemba. Kwa upande wa Pemba hali ni nzuri sitaki kwenda huko lakini nina-*quote* kifungu cha mwisho kinasema, "Mafanikio ya miradi ya maji inayofanywa na Mamlaka ya Maji bado haioneshi mafanikio kama vile serikali na wananchi wanavyoweka matumaini kabla na wakati wa utekelezaji wa mradi huo, hii ni kasoro ambayo inahitaji kufanyiwa utafiti wa kujua sababu za kina. Kwani baadhi ya makosa yanayofanywa hayastahiki kufanywa hata na watoto wadogo, kwani ni wazi hayahitaji kuyatafuta na yanaiweka Mamlaka kwenye sura isiyokuwa nzuri".

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nimejaribu kusoma taarifa hii fupi, ili kuona ni namna gani Mamlaka hii bado haijajipanga. Mimi ninahisi twende tukapate taarifa kwenye wenyewe wahusika ili tupate kujua nini tatizo, kwa sababu kwanza tunahisi kuna matumizi mabaya ya fedha, lakini vile vile na katika eneo la *procurement* bado inaonesha tunanunua vitu ambavyo vipo *under quality*.

Mhe. Mwenyekiti, kuna siku nilizungumza hapa tunapokwenda katika ukaguzi wa kuangalia *value for money*, lakini tatizo letu hatufanyi ile *technical auditing*. Mhe. Mwenyekiti, hapa ndipo tunapofeli.

Hata huu mradi wa Japan siku ambayo ulizinduliwa pale kuna *engineer* mmoja alisema mradi huu hatutegemei kwamba utafanikiwa. Kwa sababu wakati tunazindua bado kuna *linkage* nyingi.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, hapa kitu ambacho ninachotaka kukisema kwamba Mhe. Waziri kama nilivyosema bado ni mpya na amesema tumemsaidia sana semina, na tunakuahidi tutakupa semina za ziada ili ujue huko afisini kuna.

Mhe. Mawaziri tunakupenda lakini na hili utalishughulikia. Mhe. Mwenyekiti, naomba maelekezo.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa Mjumbe hoja yako ni nini katika maelezo haya.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu kama alivyokubali Mhe. Waziri kwamba hana tatizo na ile tume kwenda kuangalia masuala ya ardhi, lakini na hili vile vile tupate nafasi twende tukahoji, tuchunguze na tuwaulize wenyewe wataalamu, kwa sababu hata aliyeandika ripoti hii yupo tutapata nafasi ya kumuuliza vizuri kwa sababu ameshafanya utafiti wa kutosha.

Maana tume imezungumzia juu ya masuala ya ardhi. Hebu kama kuna maelezo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba tume waliyoiomba hasa wakati walipokuwa wakichangia Waheshimiwa Wajumbe ni Tume ya Kufuatilia Migogoro ya Ardhi, nayo nimesema kwamba wizara yangu katika hilo haina matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, afisi yako iunde tume hiyo na iipe hadidu rejea. Sasa hili ni jipya ambalo sikuligusa mimi katika mazungumzo yangu. Naona ni vizuri, maana yake kuna mambo katika aliyoyasema yanajibika, kuna mambo hayawezi kujibika ghafla.

Kwa mfano tatizo la maji. Mhe. Mwenyekiti, tatizo hili linasababishwa na mambo mengi sio *procurement* peke yake. Mhe. Mwenyekiti, uvamizi wa maeneo katika vyanzo vya maji unapunguza kiwango cha maji katika hali kubwa sana.

Juzi niliwachukua Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi, nikawatembeza katika vyanzo vya maji. Ni chanzo kimoja tu ndio tulichokuta kipo katika hali nzuri. Hiki cha Dimani.

Lakini vyanzo tulivyokwenda kaskazi huku, tumekwenda Kiwengwa kule, tumeingia chini kule kwenye maji, maji hivi sasa yameshageuka maji ya chumvi, mtihani unaanza huo. Tumekuja zetu hapo Mwanyanya tumetizama, maji badala ya kuwa yamefika kwenye ile level ya juu kabisa kwenye chumba

ambapo mlango ulikuwa huwezi kufungua, leo uyachungulie yapo chini kule yanachemka kwa taabu.

Tumekuja zetu Mtoni, hapo ndio ghasi. Sijui kama leo hayajakauka. Hiyo ndio hali halisi. Kwa hivyo vyanzo vya maji vina matatizo yake. Hivyo upungufuu wa maji pia unasababishwa pia na haya maeneo ya vyanzo vya maji kuvamiwa na kujenga katika maeneo yao yanapunguza uwezo wa visima vile kutoa maji. Hilo ni tatizo moja.

Pili kazungumza suala la matangi. Kuna matangi kusema kweli ni ya muda mrefu lazima yaanze kuvuja. Kuna matangi yaliyojengwa na mradi wa China. Ni matangi ambayo kwa kweli yanaachana mara moja yakipata hali ya hewa yetu. Hali ya hewa ya China na hapa ni tofauti. Yakipata jua zinapindana zile sandarusi zinaachana na maji huvuja.

Ndio tatizo la Makunduchi lipo hivyo, Mgenihaji lipo tatizo hilo hilo, likipigwa na jua tu huwa yanavuja. Ndio maana ZAWA hivi sasa wanapendekeza sana kujenga tangi kama liliopo pale SEMUSO ambalo lile ndilo linalodumu.

Lakini hata hivyo pamoja na masuala ya posho aliyoyagusa, ni masuala ambayo kusema kweli wizara yangu haiamui masuala ya posho, pale kuna bodi katika ZAWA ndio inayofanya kazi. Labda hivi sasa ana *draw intention* yangu ni kwamba yale yawe yanaletwa kwangu niyaone niyaidhinishe. Ninakubali hilo nitachukua hatua kusema kweli.

Hili suala la kibanda ninachokisikia hapo. Mimi ninadhani Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ipo, ni vizuri ifanye hiyo kazi. Ningemshauri ikanya kazi hiyo Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi na huku tukaendelea na bodi, tutatizama hali halisi, ukipatikana ule ukweli Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu itachukua hatua tu. Hapana tatizo.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa ninacheka cheka ndio maana na wengine wanacheka.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri mimi ninataka nimsaidie zaidi ili huu mtihani aliokuwa nao afaulu. Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikieleza ninafikiri baadae ukiangalia katika *hansard* nilitoa angalizo vile vile, na huku pia kunahitaji kukachunguzwe, kwa sababu kuna matumizi ambayo tunahisi hayapo vizuri.

Ndio maana nikasema hivi sasa ipo haja tufanye na *technical auditing*, hatutokwenda peke yetu. Wapo watu tutawatafuta watakwenda kumsaidia Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, wafadhili ndio wanaotusaidia pesa hizi kila siku, na ikiwa mambo hayaendi kidogo inakuwa ni matatizo. Sasa Mhe. Waziri hapa kaeleza kwamba matangi yamekaa muda mrefu lakini ripoti hii alikuwa anapelekewa Mkurugenzi alikuwa anasema vipi, "Kufikia kuyatumia kwani kunaelekea kushindwa kufanyiwa matengenezo yakiwa bado ni mapya kulingana na *life time.*

Ina maana unaposema bado ni mapya kulingana na *life time*, ina maana hayajafikia kuwa makongwe. Sasa Mhe. Mwenyekiti, naomba labda baadae tutakapokuja kutoa muongozo, mimi nitaomba na vile vile labda nisibishane kwa sababu Mhe. Waziri ni mwalimu wangu sana.

Naomba sawa hili tusiliingize katika kamati teule lakini tunawaomba sana watu wa Mamlaka ya Maji, wajue kwamba wanayoyafanya tunayajua. Sasa hivi tena basi lakini Kamati ya Mawasiliano na Miundombinu. Mhe. Mwenyekiti, kumejaa madudu huyaoni tusaidie Mhe. Mshimba (*Makofi*).

Naomba hili tuliachie lakini kamati naomba ifanye kazi yake.

Mhe. Mwenyekiti: Ninakushukuru sana Mhe. Hamza na ninamshukuru vile vile Mhe. Waziri. Ninafikiri hapa Mhe. Waziri anakubali kwamba asaidiwe sana kama unavyosaidia, na kama ulivyoiomba kamati pale Mwenyekiti ananitazama, basi na yeye hiyo kazi ataifanya kumsaidia Mhe. Waziri.

Nia na madhumuni ni kuona kwamba masuala haya yanafanikiwa kwa faida ya wananchi. Kwa hivyo ninashukuru kwa mashauriano na maelekezo hayo na Mhe. Waziri yupo tayari kufanya kazi pamoja na kamati.

Unajua hizi hoja zilikuja kama radi. Kwa hivyo walikuwa ni wengi sana. Sasa hebu nimsikilize Mhe. Mtando.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Ninashukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kuniona. Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa ninachangia nilizungumzia suala la …

Mhe. Mwenyekiti: Hebu samahani kidogo. Labda nitoe taarifa tu kidogo kwamba wale wasikilizaji waliopo juu ambao walikuja kwa madhumuni ya hotuba ya Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria kwa leo haitokuwepo mpaka siku ya Jumatatu.

Sasa kama wapo basi na wanapenda kusikiliza waendelee lakini itakuwa walikuja kwa ajili ya hiyo, wanaweza kwenda mpaka siku ya Jumatatu.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Ninakushukuru Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa ninachangia hotuba hii ya Mhe. Waziri nilizungumzia suala la upandishwaji ule wa umeme katika kipindi hiki cha karibuni ambapo Mhe. Naibu Waziri alipokuwa anakuja kutoa majumuisho hapa alilizungumzia hili.

Ulianza kwenye tarehe 5 akasema umeishia kwenye tarehe 10, yaani matumizi yale yalikuwa kwa kawaida units ilikuwa ni 168 lakini ilipanda 322. Amelizungumza kwamba limetokana na maharibiko katika mitambo yao.

Lakini mimi niliuliza swali kwamba kwa wale waliouziwa kwa bei ile ambayo sio halali, zile fedha ambazo wametumia kwa wakati huu zitarudi vipi. Nilikuwa ninataka kujua zitarejeshwa kwa njia ipi. Jee watarejeshewa kwa kupewa umeme mwengine au watarejeshewa fedha zao au utaratibu gani utakaotumika ili fedha zile zirudi kwa wale wananchi ambao wamekatwa pesa zile pasi na matumizi.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwamba hilo suala kweli alilizungumza na kweli hiyo *technicality* tuliyokuwa nayo katika kompyuta zetu, na kwa kweli limeshajirekebisha na ni kweli wapo watu walioathirika baina ya tarehe 5 na tarehe 9, kwa sababu tarehe 10 mashine zimeanza kwenda kama kawaida.

Tumesema kwamba kwa wale ambao walioathirika katika wakati ule. Kama wanataka uhakika wa kujua kwamba wamerejeshewa umeme wao ni vizuri waandike malalamiko kwenye shirika pale, watajulishwa kwamba wamesharejeshewa *units* zao au hawarejeshewa *units* zao.

Kama hawajarejeshewa basi watarejeshewa *units* zao. Shirika limekubali kabisa kuchukua hiyo dhamana, imekubali kabisa kwamba itachukua pindi wakidai. Hilo halina matatizo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri lakini mimi kidogo nilikuwa kidogo ninataka atusaidie ufafanuzi.

Kwa sababu kosa hili lilifanywa na shirika, sasa tukianza kuwaambia wananchi ndio waanze kuandika maombi au malalamiko, hilo kosa lilifanywa na shirika. Mimi ninafikiri shirika lilikuwa liandike barua kwa hao wananchi

waliowakosa kuwaomba radhi kwa hilo tukio ambalo wamelifanya na kuwaonesha kwamba kila mtu kumuandikia barua kuwa deni hili ambalo tumelikata silo, labda ilikuwa ni hivyo kuliko wananchi ndio waliombe shirika.

Naona Mhe. Mwenyekiti, kama itakuwa ni kinyumenyume. Ninafikiri Mhe. Waziri hebu utusaidie busara zaidi, hizi fedha ndio mimi penye utata wangu ulipo zitarudi vipi. Maana umesema wengine wamerejeshewa na waliokuwa hawajarejeshewa aandike barua. Lakini hapa kuna fedha, hii unit ilikuwa inauzwa 168 lakini siku ile kwa tarehe 5 mpaka hiyo tarehe 9 ambayo aliyoisema Mhe. Waziri iliuzwa kwa shilingi 322, ni ongezeko kubwa sana hilo.

Ndio nilikuwa ninataka kujua, zitarudi vipi ili wale walionunua umeme kwa bei ambayo siyo, kwa sababu malalamiko haya ni mengi. Kama kuandika barua basi mimi nilikuwa naomba kwa Mhe. Waziri bora shirika lako liwaandikie barua hao waliowafanyia makosa na sio wananchi waliofanyiwa makosa ndio waandike barua ya malalamiko, wao walikwenda kununua umeme kwa ile bei ya kawaida ndio wanayoifahamu, na ndio maana wakawa wanalalamika. Hebu tusaidie ufafanuzi Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu sana Mhe. Mtando. Lakini ninamwambia kwamba walioathirika katika matatizo ya kompyuta zetu kwenye tarehe hizi nilizozitaja, shirika inawajua kwa sababu wapo kwenye mitandao yao na wanajua huyu ameathirika.

Shirika wameniahidi kwamba watawarejeshea *units* zao wale walioathirika. Lakini binadamu anaweza akajenga hofu akasema nitajuaje kama mimi nitarejeshewa *units*, basi ni vizuri aende atarejeshewa *units*, hatorejeshewa pesa, atarejeshewa *units* zake zilizopungua.

Kama Mhe. Salmin Awadh *units* 45 zimepungua atarejeshewa na risiti zake zimethibitisha pale kwamba yeye zimepunguzwa *units* 45 kwenye kipindi kile. Kwa hivyo atarejeshewa *units* kama kawaida. Hiyo imekubali kuwa atarejeshewa *units*.

Sasa suala la kuwaandikia barua, sio wazo baya lakini kawaida Mhe. Mwenyekiti, haki hudaiwa, si vibaya mtu kudai haki yake.

Mhe. Mwenyekiti: Nadhani muongozo upo wazi.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu kwa kiasi Mhe. Waziri lakini hebu atupe uhakikia basi wa kule kurejeshewa kwao kutachukua muda gani.

Maana ili itakapofika hicho kiwango ambacho wao wamepanga kuzirejesha zile *units* kwa wale *units* kwa sababu wanao kwenye mitandao yao, kwamba mpaka tarehe labda mtu atakuwa hajarejeshewa sasa huyo aka-*claim* pale.

Kwa sababu anavyoonesha kuwa kuna utaratibu mzuri tu wameuandaa wa kurejesha zile *units*. Sasa hebu atusaidie kwamba mpaka tarehe gani kama mtu atakuwa zile *units* hazijarejeshwa kwake basi huyu ndio aende akalalamike kule.

Mimi ninafikiri huu utaratibu ndio utakaotusaidia kuweza kujua kwamba muda utakaotolewa tutakuwa tunajua kuwa labda baada ya wiki mbili watakuwa wamesharejeshewa wote. Kwa hivyo mtu atajikuta hayumo kwenye kurejeshewa, sasa huyu ndio akalalamike. Labda atusaidie hilo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ninafikiri katika kurahisisha tatizo hili ni vizuri hao walioathirika wakapeleka malalamiko yao. Kwa sababu gani.

Anaweza Mhe. Waziri akaahidi wakarejeshewa waliorejeshewa, tuseme muda wa wiki mbili lakini wengine ikawa wamesahaulika wakaja wakasema mbona wengine hawajalipwa. Ni vizuri basi wangepeleka malalamiko ili kudai baada ya hapo sasa, hii inawezekana sana kuweza kuweka lakini bila ya kuwa na malalamiko kwa sababu watu wenyewe ni wengi, si mmoja, si wawili ni wengi kuna uwezekano kabisa wengine wakaja wakaachwa kama hakuna malalamiko ya wale walioathirika yaliyofika pale ili wakachukua hatua.

Mimi ninadhani ushauri huu aliotoa Mhe. Waziri ni sahihi kabisa.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Ninakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa busara zako na hivi ndio ninavyokupenda, una hekma na busara katika kuongoza. Ninakushukuru Mhe. Mwenyekiti, na tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Nina hofu ya kuja kuambiwa ninampa Mhe. Jussa tu na wakati mwengine na si wakati mwengine ni wakati wote anakuwa na hoja za msingi sana. Lakini nadhani Mhe. Ali Salum nadhani tumpe nafasi.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa busara zako, kuangalia zile buti ndogo ndogo angalau na sisi tupewe nafasi.

Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikimuuliza mzee wangu, maalim, Alhaji katika suala la migogoro ya ardhi Maruhubi, nilitoa mfano ndugu zetu wa mkorogo wale, miguu mswahili, nywele mwarabu.

Sasa ameniambia kwamba amelipatia ufumbuzi. Ninataka anisaidie kwa sababu sikutosheka na majibu yake. Huo ufumbuzi uliopatikana ni upi, yaani yule aliomba *lease* mwanzo, ikaja akafutiwa pasipo na utaratibu na akaanza na utaratibu wa kuanza kujenga ndio aliyerejeshewa au yule ambaye alipewa *lease* mara ya pili ndiye kapatiwa.

Ninataka huu ufafanuzi ni yupi hivi sasa anayemiliki lile eneo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, mimi ninataka kumfahamisha Mhe. Ali Salum kwamba tulichokifanya sisi ni usuluhishi, kuondoa ule mgogoro. Yule aliyepewa hati na huyu alipewa hati. Kwa hivyo tumewatafutia mwahala, wewe utaondoka hapa utakwenda hapa na wewe utabaki hapa.

Tume-s*olve* limemalizika. Tumefanya usuluhishi na wenyewe wameridhika.

Mhe. Ali Salum Haji: Nimeridhika Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Naona Mhe. Jussa mnyonge kweli. Tunaendelea.

Jumla ya Kifungu Idara ya Mipango, Sera na Utafiti shs.166, 000,000/=

Kifungu 0402 Mamlaka ya Maji Zanzibar

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, katika jumla ya michango yangu niliyotoa kuhusiana na suala la maji Mhe. Waziri atakumbuka nilimwambia kwamba mtangulizi wake, aliyekuwa Waziri wa wizara hiyo Mhe. Ali Juma Shamuhuna tulikuwa tukizungumza, na kama alivyosema kwamba sikuwahi kuliibua hapa, tulikuwa tunazungumza nikifuatia kama ni Mwakilishi tu juu ya suala la haja ya kuongezea nguvu katika huduma ya maji inayokuja katika Mji Mkongwe hasa ukizingatiwa hii ni *capital* ya Zanzibar.

Lakini vile vile kwamba ndio eneo ambalo lenye vitega uchumi vingi, na linachangia pakubwa katika uchumi wa nchi yetu, utalii na maeneo mengi mengi Mhe. Mwenyekiti, maofisi ya serikali yote yapo pale.

Sasa katika mchango wangu nilitaka kujua hatua iliyofikiwa hivi sasa katika kile kisima ambacho tuliahidiwa kwamba kitachimbwa, ili kuongezea nguvu

kile kisima kinachotoa maji kwa Mji Mkongwe hivi sasa, ili vipatikane visima viwili visukume maji kwa nguvu zaidi katika eneo la Mji Mkongwe na kumaliza, ninafikiri halitomalizika angalau kupunguza kwa kiasi kikubwa tatizo la Mji Mkongwe ambalo lipo katika mji mkuu wa nchi ya Zanzibar.

Naomba maelezo kutoka kwa Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, huu mradi wa hivyo visima 30 bado haujaanza lakini karibu utaanza. Kwa hivyo hilo suala lipo katika mpango wa kuhakikisha kuwa tunaongeza visima kwa ajili ya maji ya Mji Mkongwe. Hiyo tunajitahidi sana kwamba tutalishughulikia sana suala hilo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Ramadhani ni mzee wangu kama nilivyosema na kwa sababu kasema kuwa yeye ni mpya, ninamkubalia lakini wala sitaki kuwambia anipe muda kama wengine, mimi ninampa mwaka mzima wa fedha huu lakini namuomba tukijaaliwa mwakani tutakapokuja kwenye bajeti nione kwamba tayari kisima hiki kimechimbwa na kimeanza kazi na Mji Mkongwe unapata kuhudumiwa kama mji mkuu wa nchi ya Zanzibar.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jussa huyo atakuja na *hansard* baadae. Tunaendelea.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nilizungumza usambazaji wa maji vijijini na nikasema kuwa taarifa iliyokuwemo kwenye kitabu cha bajeti iliyopita ya Wachina kuchangia Dola za Kimarekani milioni moja na nusu, pamoja na sehemu ambazo maji yalikuwa yapelekwe takribani ndivyo yalivyoelezwa vile vile katika kitabu cha bajeti hiki cha mwaka 2012/13.

Kwanza nilitaka kujua kuwa hizi Dola za Kimarekani ambazo milioni moja na nusu, ambazo zilikuwemo katika kitabu kilichopita na zinaingizwa tena humu, ni nyengine au ni zile zile hazikulipwa. Hilo ni moja.

Pili kulikuwa na sehemu ilielekezwa kuwa tutasaidiwa kwa maji na moja ilikuwa ni Mtambwe Kaskazini. Katika kitabu kilichopita hili halikutokea vijiji vimebakia vile vile na humu imetiwa tena isipokuwa Kisiwani kwa humu imepunguzwa. Kwa hivyo ilikuwa naomba maelezo.

Halafu kuna vijiji havikutiwa lakini kitabu hivi kinasema vyote vitashughulikiwa, kwa hivyo naomba Mhe. Waziri atueleze hali halisi ilivyo,

maana haya maelezo yaliomo mwaka huu ndio yale yale ya mwaka jana katika kifungu hiki.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, katika kitabu nilikuwa ninazungumza mambo mawili. Ninazungumza utekelezaji wa mwaka uliopita na nitakayoyafanya katika mwaka ujao.

Kwa hivyo ile aliyoikuta katika utekelezaji wa mwaka uliopita, niliyozungumza leo ni katika utekelezaji kwenye kipindi kijacho. Ni kweli kabisa kutokana na hali halisi ya upatikanaji wa maji unaweza mradi ukauanzisha lakini usiweze kuukamilisha.

Kwa hivyo itabidi lazima uendelee. Kwa hivyo ninakubali kwamba anayo matatizo Mhe. Mwakilishi katika jimbo lake, na haki yake kupigania watu wa jimbo lake ili na wao wapate maji kama wanavyopata sehemu nyengine, lakini na sisi tunajitahidi kuona kwamba tunamfikishia maji katika maeneo yake.

Wakumuomba hapo ni Mwenyezi Mungu atujaalie tufanikiwe katika miradi yetu hii, ili kila mtu katika kijiji chake aweze kupata maji. Lakini huko ardhini Mhe. Mwenyekiti, kuna tatizo la maji, tena ni kubwa. Unachimba kisima unakipiga *pump* wiki moja, wiki ya pili hamna kitu. Kwa hivyo tatizo hili ndilo linalotokezea.

Hivyo utakuta kuna mwahala miundombinu ya maji, mabomba ya maji tumekwenda na kuyafikisha mpaka huko, lakini bahati mbaya unapiga maji siku mbili, unafungua kwa sherehe na kila kitu, kisima kinakauka kinakuwa hakina maji.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, mimi ninamuomba tu awe msatahamilivu na sisi tunajitahidi kumuona. Nia yetu hasa hasa malalamiko kama maji hayapatikanaji hapa Unguja hatutaki yawepo ndani ya Baraza, yasiwepo hasa, tunataka watu wote wanapata maji kwa uhakika lakini sasa unachokitaka sicho utakachokipata, utakipata utakachojaaliwa.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri sikumfahamu, lakini kwa hili ninalolizungumza nimemsikia kama akisema kuwa maji yamekauka. Sisi kisima chetu maji hayajakauka na mashine iliomo ni ya milioni kumi na nane. Hivi sasa inafanya kazi chini ya uwezo wake kutokana na kuwa hayo mabomba hayajasambazwa. Hiyo ni taarifa.

Lakini nilisema vipi Mhe. Mwenyekiti, katika kitabu kilichopita hiki ulisema kwamba Wachina watachangia Dola za Kimarekani milioni moja na nusu, na

katika kitabu hiki tunachokizungumza imetiwa hivyo hivyo. Ndio ninasema zile pesa hazikuchangiwa ndio zimeingizwa huku au vipi. Naona hili hajanijibu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, nilisema kwamba huo mradi haujaanza wa China tunautaka. Unaweza ukaahidiwa miradi ukaambiwa utaanza kesho kutwa lakini ikawa bado haujaanza.

Lakini maji Pemba juzi tumesaini mradi hapa tarehe 30 mwezi wa Mei ulikuwa ule, tumesaini maji kwa ajili ya Pemba na Wilaya ya Wete imo katika mradi huo. Kwa hivyo tusubiri namna watakavyoendelea Wachina, juu una ADB huu, si Wachina.

Mhe Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, na la mwisho nalo hakulijibu ni kuwa safari ile Kisiwani ilitiwa kwamba itapelekewa maji lakini safari hii kaikata haimo. Ndio ninasema kule nako vipi, hajajibu kule Kisiwani, kajibu ni Mtambwe ya Kaskazini.

Mhe. Mwenyekiti: Ninafikiri umemfahamu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Nimemfahamu Mhe. Mwenyekiti, ninasema kama haimo ninaahidi nitairejesha.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Naam.

Mhe. Mwenyekiti: Anasema kama haimo atairejesha.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Kama itarejeshwa basi Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Spika: Nilikwenda kuivaa hii nguo ili kuomba muda kwa sababu shughuli yetu hii inaonekana kama haitomaliza hivi punde. Kwa hivyo Mhe. Mwanasheria Mkuu.

KUONGEZWA MUDA WA BARAZA

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, kwa vile muda uliobaki kwa ajili ya shughuli iliopo mbele yetu hautoshi, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu likubali kutengua Kanuni ya Muda na tuendelee mpaka hoja hii

iliyoletwa na Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati itakapomalizika.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.
Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, naafiki**.**

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

KAMATI YA MATUMIZI

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilisema ni lini Mamlaka ya Maji itamiliki gari yake yenye mkonga wa krini baada ya kutegemea gari ya Wizara ya Kilimo tu ikawa wananchi wa maeneo ya vijijini wanapata shida.

Vile vile wananchi wa eneo la Mbweni wakiwemo viongozi wetu mashuhuri kukosa huduma ya maji, kuwa kushindwa kununua *pump* ya shilingi milioni tano tu, akiwemo Makamo wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Jaku anaitakia mema Mamlaka ya Maji (ZAWA) kwa sababu hivi sasa gari moja ipo, lakini anatilia mkazo kwamba itafutwe na nyengine. Wazo ni zuri inshaallah, uwezo tukiwa nao tutafuta hiyo gari nyengine.

Lakini hivi sasa ipo na inafanya kazi vizuri. Ni kweli baadhi ya wakati ikipata *short down* tunaazima huko tunakoazima lakini gari ipo Mamlaka ya Maji.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe Mwenyekiti, hiyo gari imekuja lini.

Mhe. Mwenyekiti: Umeipata hoja Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, mimi nimekuja nimeikuta kwa hivyo sasa sijui imekuja lini.

Kwa sababu hili suala umekuwa ukiliuliza zamani nikalazimika niwaulize wale, wakaniambia kwamba gari tunayo, mimi nimekuja nimeikuta lakini gari ndio gari, mara inakwenda gereji, ndio gari ilivyo desturi yake sio kama kila siku ndio itafanya kazi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, mimi ninajua kwamba hakuna gari. Gari iliyokuwepo ni ya Wizara ya Kilimo na mimi ni mmoja wa

wadau wakubwa inayokodi gari hiyo kutoka kampuni za *private* kwa shilingi laki mbili na nusu kwenda Unguja Ukuu, Mfumbwi – Jambiani na kwengineko kwa jimbo langu mimi.

Sasa kama kuna gari imekuja jana au leo jioni sijui.

Mhe. Mwenyekiti: Sijakufahamu Mhe. Jaku, hebu elezea kwa urefu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, hiyo gari kama imekuja leo sawa ninaweza kukubali lakini kwa jana na juzi gari haipo, gari ninayoijua mimi ni ya Wizara ya Kilimo, na wakati mwengine inakuwa haipatikani gari hiyo, tunataabika kwenda kukodi nje kwa thamani ya shilingi laki mbili na nusu Mhe. Mwenyekiti.

Sasa mimi ninavyojua hiyo gari haipo Mhe. Mwenyekiti, gari iliopo ni ya Wizara ya Kilimo na ukiupinda usukani ukitaka kwenda kushoto basi unakwenda kulia. Kwa maana gari yenyewe imechoka sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Jaku lazima akubali kuchukua *credit* yake juu ya ufuatiliaji wa mambo. Kama yeye alichukua gari kupeleka Unguja Ukuu, alikuwa akifanya kazi nzuri sana ambayo sisi imetuvutia kuhakikisha yanafika Pete na maji yamefika Pete.

Lakini gari ipo na juzi ilikuwa Nungwi kwenye kisima cha Kigunda inafanya kazi. Kwa hivyo mimi nimelikuta, hiyo ndio hali halisi. Lakini yeye kwamba jitihada kwamba kuchukua Wizara ya Kilimo akakosa akenda kuazima kwengine, hiyo ndio *spirit* ambayo Mhe. Mwakilishi anataka kuonekana kwamba anawatumikia watu wake, akiona huku munakawia basi yeye anatafuta gari mwenyewe anapeleka, ni nzuri kabisa hiyo na imemsaidia sana kwa sababu hivi sasa matatizo ya maji yamepungua kabisa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, suala la pili sijapata jawabu, hili mimi nitaridhia lakini gari ninajua haipo Mhe. Waziri, gari iliyokuwepo ni moja tu ya Wizara ya Kilimo lakini ni mkubwa wangu na bosi wangu katika chama, nitaridhia hilo. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Tunashukuru sana Mhe. Jaku kwa kushirikana na wizara hii. Ninasema tunashukuru kwa kushirikiana na wizara hii. Nadhani hivi sasa tuendelee.

Kifungu 0402 Mamlaka ya Maji Zanzibar Sh.2,005,000,000

Kifungu 0501 Idara ya Ujenzi Sh. 622,000,000

Kifungu 0701 Hifadhi ya Mji Mkongwe

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kumpa kipaumbele Mwakilishi wa Mji Mkongwe, kusimamia fungu la Hifadhi ya Mji Mkongwe. Mhe. Mwenyekiti, moja katika bahati za Mji Mkongwe ina Wawakilishi wengi sana katika Baraza hili, nawashukuru sana akiwemo Mhe. Omar Yussuf mkaazi wa Mji Mkongwe na mpiga kura, tunaheshimu kwamba tunao watetezi wengi.

Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu niliipongeza mamlaka katika maeneo ambayo inafanya kazi vizuri, lakini kuna maeneo kadhaa ambayo nilitaka maelezo ya Mhe. Waziri. Lakini najuakwa wingi wa hoja, kama alivyosema mwenyewe hakuweza kujibu zote, kwa sababu anasema alipokea hoja zaidi ya 100. Kwa hivyo, mimi zile nyengine namuachia akazifanyie kazi, kwa sababu anasema zote kazinukuu. Lakini kuna moja, hii haigusi wakaazi wa Mji Mkongwe tu, hii inagusa nchi kwa ujumla wake kwa ile nafasi ya Mji Mkongwe kama ndio makao makuu ya nchi. Hili Mhe. Mwenyekiti, lilikuwa linahusu kuendelea kuvamiwa na kujengwa maeneo ya wazi katika Mji Mkongwe.

Mhe. Mwenyekiti, sote ni mashahidi kama tutalilia ardhi, basi katika Mji Mkongwe hakuna hata ile nafasi ya ardhi tena, tangu hivyo tulivyoikuta. Sasa bado kumejitokeza wajanja wachache wanapenya huku na kule, wanatafuta kila uhalali wanajenga hata kwenye vichochoro Mhe. Mwenyekiti. Kama Mhe. Waziri katika maelezo yake alivyokuwa kaligusa. Kwa hivyo, mimi sina tatizo kama palikuwa na nyumba, halafu ikavunjwa ikajengwa nyengine. Lakini kama Mwakilishi wa wananchi wa Mji Mkongwe, wananchi wanasikitika sana kuona maeneo ya wazi ambayo tanguapo ni machache katika Mji Mkongwe na ambayo ndio pekee yanaweza kutumiwa na watoto wa Mji Mkongwe kucheza nayo yakiwa yanavamiwa na kupewa ruhusa watu kujenga.

Kwa hivyo, nilikuwa nataka leo Waziri atumie fursa hii anipe kauli ya Serikali, kwamba kwa Mji Mkongwe ukiondoa yale maeneo ambayo yalikuwa na majengo yakaruhusiwa kujengwa tena, na kama kuna vichochoro kwa ndani ya mtu hatuingilii, lakini kwa hayo maeneo ya wazi, sasa nataka atowe kauli kwa maeneo hayo kwa Mji Mkongwe itakuwa basi. Tuna maeneo mengi, kuna uwanda mkubwa wa kuelekea kwetu Makunduchi Mhe. Mwenyekiti, kwetu mimi na kwenu wewe Mhe. Mwenyekiti, tunaweza tukapeleka watu wakajenga, lakini maeneo ya Mji Mkongwe kwa yale maeneo ya wazi, tupate kauli ya Waziri kwamba sasa yale maeneo yale

yataachiwa, ili angalau ule mji ubakie na haiba yake kama ulivyokusudiwa, chini ya ile sheria ya hifadhi ya Miji ya Kale katika Dunia. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri anipe kauli.

Mhe. Waziri Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Ismail Jussal Ladhu sikuwahi kumjibu hilo swali, kwa sababu ya kuwahi wakati. Lakini ni kweli nimefahamishwa kwamba sasa hivi, maeneo ya wazi yote Mhe. Mwenyekiti, yamekuwa-*registered* katika Mji Mkongwe, na kuingizwa katika hifadhi ya mji ambayo na sheria ya Mji Mkongwe ifanye kazi mpaka katika yale maeneo ya wazi. Kwa hivyo, namuahidi kwa sababu sasa hivi yanalindwa rasmi kisheria, basi hayatoendelea kujengwa maeneo ya wazi Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mhe. Waziri kwa kauli yake hiyo ambayo nimeitaka. Namuhakikishia kama Mwakilishi wa wananchi wa Mji Mkongwe, nitashirikiana naye kuona kama ikiwa patakuwa na eneo lolote la wazi la Mji Mkongwe ambalo litajengwa kuanzia sasa, basi nitakiuka idara zote nitakwenda moja kwa moja kwenda kumripotia, ili aweze kuzuwia ujenzi kama huo. Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, ahsate sana tuendelee.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa, kwa huzuni kubwa na kwa unyonge mkubwa, nilikuwa nauliza swali karibu mara tatu katika Baraza la Wawakilishi hili Mhe. Mwenyekiti na wakati mwengine hata Mawaziri hili swali wanalipiga chenga. Mhe. Mwenyekiti, bado nina kilio kikubwa kuhusu barabara ya Msikiti wa Ijumaa kuelekea Forodhani katika jumba la kulelea watoto.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri alipokuwa akijibu, alisema kuna nyumba za udongo, lakini washauri wake wanataka kumpoteza, namwambia hivi hivi wazi kabisa, kama kuna kilio kikubwa, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kuna njia ndio iko katikati ya mji na kuna nyumba nyingi, pale alipojibu Mhe. Waziri hapana nyumba. Kwa hapa Mhe. Waziri nakuheshimu, unaweza kunizaa na vile vile pamoja na kuwa ni bosi wangu lakini hapa hapatoshi, ninataka maelezo ya kina, vyenginevyo nitataka maelezo ya kina, lakini hili halipiti.

Mhe. Waziri Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema katika majumuisho yangu pale, ni kwamba Mji Mkongwe ni lazima uwe na utaratibu kutokana na kuuhifadhi ule mji. Zamani tulipoanza kuzifunga zile njia, zilikuwa zinamalizikia pale Malindi, tukazisogeza mpaka pale bandarini. Sasa ukiondoka pale bandarini kuelekea kule mbele mpaka kuelekea kwenye nyumba ya watoto, kule *traffic* inazuilika, kwa sababu

traffic kule inatokea Mnazi Mmoja inazunguma nyuma *Africa House*, ndio inatokea kule. Ile tumezuwia makusudia, sasa hatuna *guarantee* kwamba magari yatakayoruhusiwa kutoka huku kupita mpaka kwenye nyumba ya watoto kupenya pale, kwamba halitaweza kumaliza safari yake ya kwenda pale, hatuna uhakika ya hiyo, ndio maana pale panazuiliwa. Hata kama akitokea mfanyakazi wa manispaa, atakuambia kwa pale nenda mara moja utafika, kwa sababu tatizo lililokuwepo pale ni ile bandari ya Forodha Mchanga ni kwamba pale yanakuja magari mengi tena yenye uwezo mkubwa wa kuchukua mizigo.

Lakini tatizo tunalopata ni hilo, yakifika pale hatuna hakika, kwa sababu dereva ni dereva, dereva anahesabu *trip* zake. Akiona mimi nikipenya hapa nimefika kule basi hana habari ya jambo jengine, ndio maana tumezuwia wasifike pale, vyenginevyo tukae kitako tuamuwe vyengine, tusipoamua vyengine itakuwa ule mji hatuuhifadhi. Ndio maana Mhe. Jabu Hashim Ayoub anaona tabu hiyo kwamba hayapati kupita magari ya mizigo pale kuteremka mpaka kule tunazuwia kweli Mhe. Mwenyekiti, na nyumba zinapata athari kwa hivyo na ule mji nataka uendelee kuwepo. Anayetaka kuuendeleza mji ule aje kuujenga kwa mujibu wa vile ulivyo sasa hivi, hiyo ndio hali halisi. Kwa hivyo, mimi namuomba asiwe mnyonge sana, wala asisikitike sana. Kama ana mawazo zaidi namuomba ayalete Wizarani tuyafikirie zaidi sisi na yeye tufanye vipi, lakini ile bandari inatupa shida kwa magari makubwa, hiyo ndio hali halisi. *(Makofi).*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, hili suala bado kwangu mimi ni zito na mimi kama nilivyosema mwanzo, mimi ni mwekezaji wa Mji Mkongwe. Mimi Mji Mkongwe naujua. Yeye alikuwa akitoka huko alikua akiishia Mazizini ndipo kwenye ofisi yake, sasa siri ya kaburi anaijua maiti. Mimi bado kabisa, mpaka ifunguliwe njia ile ndio niridhike, vyenginevyo tupige kura kabisa, lakini hili sikubali katu. Sisi tumekuba kwa niaba ya wananchi kuja kuwatetea na pia kuja kuikosoa Serikali hatujafanya makosa ni wajibu wetu.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri mimi kama mwanao, nakuheshimu sana lakini washauri wako wa Mji Mkongwe wamekushauri sivyo Mhe. Waziri. Kama wanautaka Mji Mkongwe kweli basi wangeusafisha, Mji Mkongwe wote unanuka na kama pana shimo, ile nyumba ya kulea watoto pana magari yalikua yanapita chini ya nyumba wala hakujafanya ufa na hayo magari yalikuwa yakipita tokea enzi za wazee wetu wanavaa tunguja ndio urembo wakati huo. Leo unakuja kutuambia nini Mhe. Waziri kuhusu suala hili. Mimi bado na ninakuheshimu Mhe. Waziri, mzee wangu, bosi wangu kwenye chama, lakini bado hapa pazito. *(Makofi).*

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, ukiona mpaka Mhe. Jaku Hashim ameiva namna hiyo, basi ujuwe kweli limemuuma hilo analolizungumza. Lakini hapa tunachuzunguza sio *position*, wala sio mawazo ya Mhe. Waziri. Hapa tunazungumza sheria yetu ilivyo na imeeleza wazi, kama Mhe. Jaku Hashim hana, basi mimi niko tayari nikae nae na nimuoneshe sheria inavyosema na kanuni zake kuhusiana na suala la *traffic* katika Mji Mkongwe. Sasa kama hilo linatatizo, mimi nadhani ingeanzia huko kuleta mawazo yake yeye ya kwamba aah! Sasa hiyo sheria tuifute haifai, lakini Mhe. Waziri akiahidi vyengine atakuwa anakwenda kinyume na sheria na atakuwa anakwenda kinyume na kanuni.

Mhe. Mwenyekiti, Waswahili wanasema 'ukipenda doriani upende na harufu yake'. Kwa hivyo, kama tunataka Mji Mkongwe uendelee kuwa ni hifadhi ya kimataifa na ni urithi wa kimataifa miongoni mwa masharti yake ni hayo, yana *inconvenience* yake. Wenzetu Lamu nadhani hata gari hawaruhusu mpaka leo pamoja na ustaarabu ulioko, kwa sababu wanataka hilo. Hivyo, hilo ni suala la sheria. Kwa hivyo, mimi ningemshauri Mhe. Jaku Hashim tungetizama labda hizo *alternative* zake za vipi turekebishe sheria bila ya kwenda kinyume na masharti ya hifadhi ya kimataifa ambapo ndio hadhi ambayo Mji Mkongwe inayo. Lakini kumtaka Mhe. Waziri, ni kumtaka avunje sheria na ni kumtaka autowe Mji Mkongwe wa Zanzibar upoteze sifa na sidhani kama hiyo ndio sera ya nchi yetu kwa sasa hivi. Kama tunataka kwenda huko, hiyo ni hoja nyengine, iletwe, izingatiwe na mpaka tufikie mwisho turekebishe na hayo mengine.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, mimi namshauri sana Mhe. Mwanasheria Mkuu kutokana na elimu yake aliyokuwa nayo, pamoja na hekima zake na busara zake. Mimi nimekufuata sio mara moja au mara mbili, ukaniambia kaa kaa, lala lala, inuka inuka, ukisema usiku unasema mchana. Lakini hili bado Mhe. Mwanasheria Mkuu hebu niambie kweli, hawa kukaa juu ya sheria ni Mji Mkongwe Mhe. Mwanasheria Mkuu, nina ushahidi sio mmoja, sio miwili wala sio mitatu. Sasa mkuki kwa nguruwe tu kwa binadamu unauma. Kama msongamano Mji Mkongwe wametoa kibali kuwa nyumba inajengwa pale tokea Mhe. Dk. Aman Karume aliyeleta Serikali ya Kitaifa hii, kuna nyumba imezungushwa mabati miaka minne sasa hivi, sizungumzi kwa kubahatisha. Kama msongamano wameuanza wao, sasa elimu ya sheria, sheria gani. Wanatoa vibali nyumba za chini zinavunjwa zinajengwa na kama kukiuka sheria ni Mji Mkongwe. Mhe. Mwanasheria mimi nakuheshimu hili suala ni zito, tupige kura tumalize basi hakuna njia nyengine.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, mimi nadhani tunakiri kama unavyokiri na wewe Mhe. Jaku Hashim kwamba suala hili ni zito. Ushauri wa

Mhe. Mwanasheria Mkuu na ushauri wa Mhe. Waziri ni kwamba ni vyema tukakaa pamoja na mamlaka yenyewe na kuiangalia hiyo sheria. Kama kuna jambo ambalo linaweza kurekebishika, ili mambo yawe mazuri zaidi kwa faida ya wananchi na uhifadhi uendelee kuwepo. Hilo ni jambo la kukaa, sio vyema chombo hiki tukaamua kitu kumbe kuna sheria inayoelekeza. Kama kuna sheria ambayo inahitaji marekebisho, utaratibu wa kurekebisha sheria upo.

Kwa hivyo, Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Ofisi ya Mhe. Waziri, Mhe. Mwanasheria Mkuu na mamlaka yenyewe ipo. Mimi nadhani ni jambo ambalo linawezekana sana, wanasiasa wanasema linazungumzika. Kwa hivyo, tuzungumzeni na mimi sitaki hili tuendelee na mjadala, tukaja tukafikia pahala tukaamua, kwa sababu hili siwezi hata kuruhusu kupiga kura. Hili halipigiki kura, unaweza ukapiga kura ukawa umehalifu sheria fulani. Sasa jambo ambalo lina maelekezo ya sheria huwezi ukalipigia kura, ukipiga kura unaweza kufikia pahala ukafuta sheria.

Kwa hivyo, tukaeni pamoja ili jambo hili tulizingatie na Mhe. Jaku Hashim Ayoub ashirikishwe katika suala hili. Hata mwenyewe mwakilishi wa jimbo lile kwa sababu ndiye anayewakilisha jimbo lile. Kwa hivyo, nafikiri tuendelee. *(Makofi).*

Kifungu 0701 Hifadhi ya Mji Mkongwe Sh.330,000,000

Kifungu 0801 Idara ya Nishati

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kutaka kupata maelezo. Mhe. Mwenyekiti, nilipochangia nilianza na kitabu kilichopita ambacho kilieleza kuwa wizara hii kwa kushirikiana na Shirika la Umeme, itahakikisha kwamba inakamilisha kusambaza umeme katika vijiji vyote vilivyosalia kutokana na kumalizika kwa awamu ya nne katika vijiji vyote vilivyosalia.

Mhe. Mwenyekiti, katika kitabu hiki ambacho tunakijadili kwenye ukurasa ule ule wa 59 kama huku, maelezo ni kuwa kazi ya usambazaji umeme vijijini inaendelea kutekelezwa kwenye Mfuko wa Shirika la Umeme pamoja na mchango wa wanavijiji.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nina maswali mawili. Swali la mwanzo, mwanzoni ilikuwa wizara yenyewe kwa kushirikiana na Shirika la Umeme watawasambazia wananchi umeme, lakini huku wanasema wameshirikiana na wananchi katika kuchangia.

Je, ule mpango wa Serikali wa kuwapelekea wanavijini umeme, ambapo nashukuru sana wanavijini wanajitahidi sana kulipia umeme huu na wanauhitaji kwa nguvu zote umeondoka?

Kama kuna kuchangia kuna fomula mpya, tunaomba tuambiwe ili tujuwe namna ya kuchangia. Kwa sababu ziko wizara, kama Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, wanasema jengeni jengo mpaka likimalizika juu na mkishaweka linta basi Serikali itaezeka, hawa uchangiaji wao uko katika fomula gani. Kama wameuondoa ule mpango wa mwanzo wa kuwapelekea umem wananchi moja kwa moja.

Mhe. Waziri Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, uchangiaji ni utamaduni wetu tangu mwaka 1964, tunachangia kihali na tunachangia kimali. Sasa linapotokea tatizo watu wanahitaji umeme na kuna sehemu ya kazi ya kuleta umeme wanaiweza wenyewe, ambapo zamani tulikuwa tukiwapa nafasi ya kutafuta nguzo wakati huo hatujapata athari kubwa kwenye masuala ya nguzo ambazo hazikuiva vizuri. Basi walikuwa wakitafuta nguzo, halafu sisi tunaendelea na kazi. Lakini kama kuna mwakilishi kagundua waya nusu safari na akituambaia kagundua waya nusu ya safari na sisi nguzo tunazo tunakwenda, sio kama tumeuondoa ule utaratibu hapana, huu ni utamaduni wetu kuchangia. Kwa kweli ipo haja hasa ya kurudi kuendelea kuchangia katika kuharakisha maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, majimbo ambayo watu wamesimamia suala la uchangiaji yamepiga hatua sana. Majimbo ambayo kidogo watu wanasubiri kutekelezewa na serikali kwa asilimia 100 yamesinzia kidogo. Kwa hivyo, Mhe. Mjumbe usifikirie huo utaratibu tumeuondoa, utaratibu bado upo, lakini pia na uchangiaji ni utamaduni wetu. Utamaduni mzuri Mhe. Mwenyekiti, tusiuache ni mzuri unatufaa na unatusaidia.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kule kwetu Uzini kulikua na tatizo kubwa sana la umeme. Tulichanga kila nyumba shilingi 20,000/- basi ilitusaidia kuharakisha kutufikishia umeme katika kijiji kile pale, kwa sababu Shirika la Umeme lilikuja likatuunga mkono na tukapata kufanya kazi vizuri. Mhe. Jaku Hashim ana mpango sasa hivi, ana matatizo ya umeme pale Jambiani katika sehemu moja ndogo na keshakuwa tayari kuchangia kwa kiasi fulani ili wananchi wake wapate umeme, ndio utamaduni wetu Mhe. Mwenyekiti, sio kama tumeuacha ule utaratibu wa kawaida.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, mimi nilisema kwa sababu kuna vijiji vingi sana ambavyo havina umeme na nilivitaja hapa, sitaki nipoteze tena muda. Watu wangu walikwenda katika shirika. Lakini kilichokuwa kikifanywa ni kupewa makisio na kazi ilikuwa inamalizikia

hapo, kwa makisio yale na kwa sababu vijiji vingi havina umeme, ndio nikasema nataka nipate ile fomula ni asilimia ngapi ya kuchangia, maana tufanye kitu ambacho kiko katika fomula, sio tu maelezo, hayo maelezo yatatufikisha mbali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano ikiwa umeme ni shilingi milioni 20,000 mfano, wananchi wachangie milioni 5, tujuwe hivyo ili tuweze kujipanga na tuendelee na hiyo shughuli, kwa sababu wananchi wetu wanapata tabu.

Mhe. Waziri Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, kama hilo ni tatizo kwamba kuna vijiji vingi vyake ambavyo havijapata umeme. Apange programu, kwa sababu kupanga ni kuchagua na awe karibu na wananchi wake wakubaliane, tunaanza na kijiji fulani kwa kipindi hiki. Kwa hivyo, wananchi watachanga na yeye atachanga kidogo, hatutaki kumpa asilimia. Atuoneshe ile nia tu kwamba yeye yuko tayari ambapo sisi tunaweza tukaimaliza ile sehemu iliyobakia pale, hatuwezi kumpa asilimia, kwa nini tumfunge kwenye asilimia wakati ile ni dhima yetu pia serikali. Sisi kidogo kidogo kwa uwezo wetu tutapeleka umeme katika vijiji, kazi hiyo tunaendelea. Kwa sasa hivi Pemba ni rahisi kupeleka umeme, kwa sababu umeme sasa hivi Pemba unafika, kwa hivyo tutapeleka. Lakini katika *speed* yetu kama inaonekana ndogo, basi apange programu kwamba naanza kijiji hiki, *Alhamdulillah* nimefanikiwa. Wenziwe wa kijiji cha pili wakiona aah wale wamefanikiwa, wamefanikiwa vipi. Aah! Wale walisaidia kidogo na wao wakikamatana kamatana wakichangia kidogo, utakuwa umeme umesogea ule na wengine wakichangia kidogo umeme utasogea mpaka watamalizika wote wale, baada ya muda mfupi tu.

Kwa hivyo, sipendelei kumpa asilimia, atuoneshe dalili ya kuwa yeye anataka umeme ufike pale. kwa hivyo, katika kuchangia akituletea shilingi laki moja kutaka umeme katika kijiji kizima. Tutasema huyu mtu kweli hayupo *serious.* Lakini akituletea hata vifaa, akisema mimi mita zangu hizi hapa 300, nanunua waya wa mita 150. Kwa hivyo, sisi tutamuunga mkono, kwa sababu tutajua mita 150 tutalazimika kumaliza sisi wenyewe, hakuna tatizo tunafanya hilo na vijiji vyengine vinafanya hivyo hatuna tatizo.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nimemsikia Mhe. Waziri, na hii kupanga ni kuchangua, labda ndio iliyosababisha jimbo langu ikawa hata kijiji kimoja hakikupata umeme. Lakini ikiwa mwenyewe Mhe. Waziri anasema kuwa tuchangie hivyo hivyo na shughuli itakwenda na kama akiniahidi Mwenyezi Mungu akitujaalia tukimaliza Baraza hili, kama zikionekana katika jimbo langu hizi shughuli zimefanywa na mimi nikichangia kidogo kidogo, akikubali hivyo basi tuendelee. Ikiwa atakubali hivyo.

Lakini ikiwa ni vile vile kwenda kule tukishapewa makisio basi. Naomba ufafanuzi zaidi nitasimama pale pale katika asilimia ya kuchangia. Ikiwa mwenyewe ataona atakwenda hivyo kidogo kidogo sawa. Lakini ikiwa ndio hivyo kupanga ni kuchagua. Naona hii mimi haijanikalia sawa kidogo.

Mhe. Waziri Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, sikumpata vizuri, lakini namshajihisha kwamba ajaribu huu utaratibu niliomwambia na atafanikiwa, asiwe na wasi wasi. Kwa mfano, umeme unatakiwa mita 300, basi yeye atupe mita 150 tutamuunga mkono, hakuna tatizo lolote, wala sikusudii mimi kule wasiwe na umeme. Umeme kule utakwenda kwa mujibu wa uwezo wa serikali. Tukipata mradi wa kupeleka umeme tutaupeleka. Umeme utakwenda tu maofisa wangu wako kule, wanayajua maeneo yote yaliyokuwa na matatizo ya umeme kule.

Lakini kama yeye anataka kuharakisha ni vizuri basi ashirikiane na wananchi. Wala simwambii yeye atowe mfukono mwake, ashirikiane na wananchi katika kuchanga. Utamaduni wetu tusiuache, tuwazoweshe wananchi wetu utamaduni warudi kule kwenye utamaduni, watu wamejenga mambo makubwa. Kwa mfano, maskuli mengi yamejengwa kwa utamaduni huo, hospitali zimejengwa mpaka sasa hivi Mhe. Waziri wa Afya anasema bora basi, maana zimeshakuwa nyingi mno, wamejenga wananchi. Kwa hivyo, Mhe. Mjumbe asiwe mnyonge akaona labda anafanyiwa yeye tu, hapana kabisa. Tutashirikiana na yeye bila shaka, mimi namuahidi kabisa.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, kwanza katika mtu aliyekuwa anachangia na mwenye mashirikiano sana ni mimi. Miradi yangu nimeisikia hapa chungu nzima ambayo serikali imeshindwa kunimalizia.

Kwa hivyo, ikiwa Mhe. Waziri anasema hivyo, naomba Mwenyezi Mungu ajaalie iwe hivyo, na Inshaallah tutamaliza na tutashirikiana na wale wananchi angalau waondokane na dhiki hiyo waliyonayo. Nashukuru tuendelee.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilimuomba Mhe. Waziri anieleze ni kampuni gani inayochunguza kiwango cha ubora wa mfuta. Lakini Mhe. Waziri nafikiri hilo kaghafilika hilo hakuwahi kunijibu na hii imetokana na magari mengi kuharibika katika kipindi cha miezi mitatu au minne kutokana na mafuta yote yaliyoletwa kisiwani Zanzibar kuwa hayaridhishi kwa kiwango chake, na magari yapo yaliyoharibika kwa sababu ya mafuta hayo, akitaka Mhe.Waziri nimpeleke akayaone ushahidi upo. Mhe. Waziri anieleze vizuri.

Mhe. Waziri Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Jaku Hashim, anazungumzia juu ya ubora wa mafuta. Mhe. Mwenyekiti, gari tunazozitumia sisi, matumizi yake ya mafuta yanatofauti na gari wanazotumia wenzetu Europe. Wenzetu kule siku hizi badala ya kuchukua mafuta *pure*, wanachukua mafuta ambayo ndani yake yana *alcohol* cha kiwango kama asilimia 20 hivi. Gari zao kule zinafanyakazi hazina matatizo yoyote. Lakini ukiyachukua mafuta yale ukiyaleta Zanzibar, yakitumika katika gari, basi gari zetu ndio zinapata hayo matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, mafuta nyalio zake ni maji, ukiwa una *pure petrol* ukiiweka kwenye maji, basi unapata *petrol* tupu ukipiga pampu ile. Lakini ikiwa *petrol* umeichanganya na ile *spirit* iliyokuwa kule, ukaichanganya na ile *petrol* ambayo kwa wenzetu gari zinafanyakazi, basi ukiiweka katika maji yanachanganyika maji na mafuta. Hili tatizo lilitokea katika haya masuala ya mabadiliko ya uagiziaji wa mafuta kutoka Dar es Salaam. Kuna mnunuzi mmoja alikwenda kununua mafuta yana hiyo asilimia ya *methanol* ilikuwemo mle. Sasa yale ndio yaliyokuja hapa, ukiyaweka juu ya maji yale yanachanganyika na mafuta yote, haikubali kukaa peke yake, hilo ndio tatizo tulilopata. Lakini sasa hivi wamejirekebisha, wameshajua. Kwa sababu sio gari za Unguja tu peke yake zilizoharibika, hata gari za Bara pia zilipata matatizo hivyo hivyo. Sasa hivi wanaagiza kama walivyokuwa wakiagiza zamani pure *petrol* haina ule mchanganyiko wa *methanol* kama ile iliyonunuliwa katika kipindi cha nyuma ambayo ilileta matatizo katika magari yetu.

Kwa hivyo, aliuliza ni kampuni gani inayofanya utafiti. Mafuta yote yanaangaliwa na *TBS*. Sasa *TBS* kuwekwa ile *methanol* kwa mafuta sio tatizo, lakini sasa hivi ukiwaambia kwamba mimi yangu usiyachanganye na hii kwa kwetu sisi, kwa gari zetu hizi zinakuwa hazileti matatizo. Tulipata athari sana gari zetu zilipata matatizo kwa sababu mafuta yale yalipokuja katika kipindi kile ambayo yalikuwa yamechanganywa na hii *alcohol* ambayo inaleta matatizo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kwa vile kaniahidi tutashirikiana katika suala la Mji Mkongwe, naomba tuendelee.

Kifungu 0801 Idara ya Nishati Sh.216, 000, 0000

Kifungu 0901

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa ya kutoa maelekezo yangu. Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia niliulizia suala la mzee wetu juu ya shamba lake. Mhe.

Mwanasheria Mkuu alitujibu hapa, lakini hoja yangu ilikuwa kwamba suala hili limekwisha kutafutiwa ufumbuzi na mahakama imeshatoa maelekezo kwamba hawa watu wapewe shamba lao. Je, kuna kitu gani kinachosababisha suala hili lisifikie katika maamuzi ambayo mahakama imekwisha kutoa. Nilikuwa nataka kupata maelezo kutoka kwa Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, hili suala Mhe. Mwanasheria Mkuu amelijibu vizuri, na kwa sababu hili suala tangu limeanza Mhe. Mwanasheria Mkuu yumo katika shughuli hizi. Mimi namuomba Mhe. Mwanasheria Mkuu anisaidie katika suala hili kumfahamisha.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kueleza wakati ninachangia. Kwanza nadhani Mhe. Mahmoud atakubaliana na mimi kwamba tatizo la shamba hili sio la Serikali kwamba imeichukua, au la serikali imezuwia asirejeshewe mwenyewe. Ni kweli kwamba mahakama ilifika pahala ikatoa maamuzi, sasa suala la utekelezaji linakuwa ni la Polisi. Polisi katika utekelezaji siku zote imekuwa ikikumbana na kikwazo. Kikwazo kikubwa ambacho imekumbana nacho ni ukweli. Maana walipokwenda mahakamani wahusika walipata sheria, lakini kilichoko unapotaka kwenda kutekeleza sasa ni suala la haki, wako watu wenye haki zao, ambapo hakuna mtu yeyote ambaye anaweza akakataa, kwamba umesema kweli umekwenda mahakanani na mahakama ikasema kwamba shamba hii ni shamba ya Mhe. Mahmoud, lakini ukenda ukweli wa mambo na ambao kila mtu hakatai, ni kuwa wewe unaambiwa shamba ya Mhe. Mahmoud kuna wenyewe ambao wana nyaraka za tokea mwaka 1925, kuna wenye nyaraka za tokea mwaka 1930 na kuna waliopewa eka katika eneo hilo hilo ambalo wewe mahakama imesema kwamba ni haki yako.

Kwa hivyo, tatizo linakuja hapo, kuwa mahakama si imeshakupa amri, sasa chukua na mimi mwenyewe niko hapa, ndio kikwazo ambacho kimetokea na tuliwahi kutoa wazo kwamba hili jambo limeharibika mikononi mwa mahakama. Kwa sababu na mahakama yenyewe iliunda tume vile vile, ilimpeleka Mhe. Zubeir na wataalamu wake, wakenda wakathibitisha kwamba kweli katika eneo hilo ambalo mahakama imesema wapewe hawa mabwana, muna haki za watu, mashamba ya watu wenye nyaraka, waliopewa eka na waliokaa *by presumption*.

Kwa hivyo, pendekezo lililokuja ni kwamba labda hili eneo basi lichukuliwe na serikali, labda ilipe fidia halafu iwarejeshee wale wenyewe. Hilo nalo likawa gumu, kwa sababu aliyependekezewa suala hilo akasema kwamba inakuaje mahakama yenyewe ilijua kuwa eneo hili lina haki za watu halafu ikatoa amri hii. Kwa hivyo, kama ni kulipa basi hawa watu wawe-*identify*

eneo lao na ilikwenda ikawekwa mpaka *beacon* katika hivyo vishamba vyao vinne. Lakini tatizo limekuja katika kutekeleza ile hukumu, ni kupewa haki juu ya haki ya mtu mwengine ambapo mahakama haikuliona, imetoa haki juu ya haki. Sasa tatizo ni katika utekelezaji wa hukumu, ndio maana nikasema mimi kama ni suala hili, basi ni suala ambalo kwa kweli hakuna mtu yeyote ambaye atakuwa na ufundi wa kuliweza. Kwa sababu utakapokwenda kulitekeleza pale, labda uende ukawauwe wale watu wote, halafu uwaambie kwamba haya sasa wewe chukua haki yako. Watu ndio walio chachamaa.

Mhe. Mwenyekiti, tumesikia mara nyingi kumekuwa kuna migogoro ya Shakani kwa sababu ya tatizo hili, kwa sababu huo ni ukweli ambao umethibitishwa kila pahala. Sasa kama kuna njia nadhani ni kushirikiana katika kuona njia gani sasa ya kusuluhisha katika hili. Huyu mmoja kapata haki mahakamani na huyu mmoja ana haki ya asili. Ndio tatizo lilipo kwa kweli. Kwa hivyo, isilaumiwe serikali katika hili kwamba labda Waziri kachukua au serikali imelichukua, tena baada ya mwenyewe kufariki. Mimi hilo tu ndio nimesema kwamba tatizo hili tulitafuatie ufumbuzi kwa njia ambayo ni muafaka.

Lakini hapa hatuwezi kupata ufumbuzi. Kwa sababu mimi tokea naanza kazi basi kesi hiyo nimeikuta, mpaka nimekwenda kusoma, nimerudi na mpaka nimekuja hapa Barazani na bado haijamalizika.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, mimi nimefarijika na maelekezo ambayo Mhe. Mwanasheria Mkuu ameendelea kuyatoa. Lakini hawa watu wanataka kujua nini wafanye katika suala hili? Naomba muongozo wako Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Dk. Mwinyihaji Makame, kama ingekuwa hii ni kesi basi angekuwa shahidi wangu mzuri kweli kweli, kwa ugumu wa suala hili. Mimi nasema kwamba tumejaribu mpaka kuna pahala tukafikia ukingoni. Kwa hivyo, mimi nasema tuchukuwe juhudi zile zile ambazo tumechukua. Kwa sababu tuliwahi kuchukua juhudi ya kulitafutia ufumbuzi hili suala pamoja na ugumu wake uliopo. Tulifika pahala, mimi nadhani pale tulipofika kwa kushirikiana hasa na Mwakilishi wa jimbo lile linalohusika tuziendeleze zile juhudi kwa sababu wote ni wake hawa wanaosema ya kwake ni wa kwake, na wale wanaosema haya ni ya kwao ni wa kwake na pia ni wa serikali.

Kwa hivyo, nadhani zile juhudi tulizokuwa tukiziendeleza tusiziache na tuziendeleze na labda tunaweza kupata muafaka, lakini si suala rahisi kama hivyo ambavyo wengine wangependa watu waamini kama ni jambo rahisi. *(Makofi)*

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, ahsante na mimi nimepokea maelekezo na naomba tuendelee, lakini bado nahitaji msaada katika suala hili. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, tunakushukuru kwamba suala hilo litafuatiliwa zaidi, basi ni vyema kila mwenye haki aipate ni vizuri sana kuzingatia hilo. Sasa utaratibu kama wa suluhu au ni *revision* ama jambo gani lolote linalowezekana, lakini ilivyo kila mwenye haki ni vyema akaipa. *(Makofi)*

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia hotuba hii kwenye Idara ya Ardhi nilikuwa na hoja tatu. Kwa kweli niungane na mwenzangu kwa kumpongeza Mhe. Waziri kwa jinsi hoja ya mwanzo alivyoimaliza kuhusu Kamati Teule, nampongeza.

Hoja ya pili niliizungumza nia yangu ya kujenga kule eneo la Mwambe ambalo limechukuliwa na mkubwa mmoja, Mhe. Waziri amenipa nasaha na nazikubali, lakini mwisho alinishauri kwamba tukae. Sasa naomba tuweke *Hansard* sawa kwa hapa kwamba nimuombe tusikae, kwa sababu tukikaa itaonekana kama ni tatizo langu na huyo mkubwa. Mhe. Mwenyekiti, naomba na hii aikubali ipelekwe kule kwenye Kamati Teule, ili iangaliwe kwa nini amepata ardhi ile.

Hoja ya tatu nilimuuliza Mhe. Waziri kwamba katika enzi za Mhe. Waziri Buruhani Saadati Haji kulikuwa na mtendaji ambaye alikuwa na dhana ya *lease*, na amesababisha matatizo mengi na kuondoshwa katika eneo hilo, lakini *GNU* ilipokuja imemchukua tena, sasa kasi ya matatizo ya *lease* imezidi.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri anisaidie na kwa nini wakamrudisha tena na matokeo haya kesi ya *lease* pamoja na migogoro ya ardhi imezidi, naomba anisaidie.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, madhumuni ya kukubali kwangu kuundwa kwa ile Kamati Teule juu ya suala hili ni hilo, kwa sababu watakapokwenda kule na kukuta kwamba huyo aliyepelekwa anasababisha matatizo, ndiye muhusika basi atahukumiwa. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Mjumbe tuiache Kamati Teule juu ya suala la ardhi ifanye kazi na atailinda pamoja na kupewa hadidu rejea yeye *Inshaallah*.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, haja yangu ilikuwa ni *Hansard* irekodi hilo kwamba hii kamati ikienda na hilo ilione. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee. *(Makofi)*

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa uamuzi wake wa kutukubalia lile suala letu kwamba tunaomba tuunde Kamati Teule, kwa sababu suala hili kama utakumbuka Mhe. Mwenyekiti nililianza tangu kwenye Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwenye hotuba yake, tuliomba na tukakubaliana kwamba tusubiri wizara husika na mimi nilikuwa ndiye mtoa hoja siku ile. Sasa leo imefika ile wizara husika na nimeona sana tutumie kile kifungu cha 120 kwa ajili ya kuunda Kamati Teule. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, juu ya jambo gani.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, juu ya migogoro ya ardhi, tulizungumzia migogoro ya ardhi, kwa hiyo tuunde Kamati Teule kwa suala la migogoro ya ardhi. Sasa wakati wa hotuba ya bajeti ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais tulikubaliana tuisubiri wizara husika, katika michango yetu Waheshimiwa Wajumbe wengi tulichangia suala hili, mpaka leo Mhe. Waziri amekiri kwamba tuunde tume hii. Mhe. Mwenyekiti, mimi ninavyojua kwa mujibu wa Kanuni ni lazima iletwe hoja. Kwa hivyo, mimi nilikuwa natoa hoja sasa tutumie ile Kanuni ya 120 kwa ajili ya kuunda Kamati Teule juu ya migogoro ya ardhi. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, sawa kimsingi suala hilo limeshakubalika, isipokuwa ugumu wake ni mmoja tu, kupembua yale masuala ambayo yako Mahakamani na yale ambayo hayako Mahakamani na huo ndio ugumu wake. *(Makofi)*

Lakini kwa upande wa serikali na upande wa Waheshimiwa Wajumbe tumepiga makofi mengi kwamba hilo linakubalika. Sasa kazi hiyo ameachiwa Spika aje aitafute hiyo Kamati Teule, ili wakakae huko na waseme Mwenyekiti ni yupi, lakini kimsingi limekubalika. Tunaendelea. *(Makofi)*

Kifungu 0901	–	Idara ya Ardhi na Usajili Sh.359,000,000/=
Kifungu 1001	–	Idara ya Upimaji na Ramani Sh.358,000,000/=
Kifungu 1101	–	Idara ya Nyumba na Makaazi

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia katika hotuba yake Mhe. Waziri nilichangia zaidi kwenye hii Idara ya Nyumba na Maakazi kuhusu zile nyumba 20 za watu wa Wafku sikupata jawabu lake. Sasa namuomba Mhe. Waziri kama kuna ufafanuzi

wowote juu ya zile nyumba 20 za watu wa Wakfu, naomba anipatie, ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana kwamba Mhe. Mjumbe amesubiri mpaka tumefika hapa na kuliuliza swali hili. Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu pamoja na Idara ya Nyumba haina tatizo ya kuzirejesha zile nyumba 20 kwenye Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, kwa sababu kule kuna Kamisheni na Mali ya Amana. *(Makofi)*

Lakini mimi nilivyoambiwa ni kwamba tatizo ni kodi ya zile nyumba, sasa kama tatizo ni kodi mimi naijua Sheria ya Wakfu na Mali ya Amana inao uwezo wa kuongeza kodi wakati wowote, na hilo wala sio tatizo kubwa kusema kweli. Kwa hivyo, nawaomba ni vizuri wakubali kuzipokea zile nyumba na ile dhima kwenye Idara yetu ya Nyumba iondoke, suala hilo tuko tayari kabisa na wala hatuna tatizo nalo hata kidogo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ninachotaka kutoa taarifa ni kwamba wakati wa kutafuta wale wanaodai katika nyumba zile, ambao wanadai hawajafidiwa kwa bahati walijichomoza wengine wanne wa ziada mbali ya wale waliochunguzwa na ile kamati na kamati ikathibitisha kwamba hawa wengine wa ziada wanadai. Kwa hivyo, sasa wale wakalipwa katika nyumba 20 na zikabakia 16.

Kwa maana hiyo, ziliopo hivi sasa ni 16, ambazo hizi wanaweza waka-*deal* nazo Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, lakini bado wanaidai Idara ya Nyumba nyumba nyengine nne kwa ajili ya kufidia pale, na hilo ni deni tutazungumza mimi na wao na Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria ananisikiliza tutakaa na kupanga.

Mhe. Mwenyekiti, mimi aliniita na alinieleza suala hilo na nilimwambia aniletee barua, kama angelikuwa ameniletea barua basi ningekuwa nimeshatekeleza hivi sasa. Kwa hivyo, niko tayari ziende kwenye Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana na wala hakuna tatizo lolote, kama kuna mawazo zaidi basi mimi na mwenzangu Mheshimiwa tutakaa pamoja, ili tukubaliane juu ya utekelezaji wa suala hili. *(Makofi)*

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, ahsante na ndio unaambiwa mtu mzima dawa, busara zinavyotumika na sisi tunapenda namna hii, maelezo yako wazi tena ya ufasaha kabisa. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee. *(Makofi)*

Kifungu 1101 – Idara ya Nyumba na Makaazi

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia kwenye bajeti hii lilikuja suala juu ya matengenezo ya Nyumba za Kikwajuni, Michenzani na Kilimani. Lakini nilimfahamisha Mhe. Waziri kwamba nyumba zile hazijawahi kufanyiwa matengenezo ya aina yoyote.

Sasa wakati alipokuja kujibu hoja Mhe. Waziri sikusikia maelekezo kuhusiana na suala lile, kwa sababu hivi sasa kuna baadhi ya nyumba nyengine zinataka kuua kutokana na uchakavu na kudondoka kwa matofali wenyewe. Kwa hivyo, naomba maelekezo ya Mhe. Waziri katika suala hili.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, maneno yake nayakubali ni sahihi na sasa ndio tunataka kuanzisha huo utaratibu wa kuweka Shirika la Nyumba na kuzifanyia matengenezo zile nyumba. Vile vile kwa yale matengenezo ambayo yanaharibika, ambayo Wajumbe wa Kamati wakati mwengine hutuletea sisi huwa tunachukua hali ya kuzihami.

Lakini tunalo tatizo moja ambalo nataka nilieleze. Mhe. Mwenyekiti, ni vizuri hivi sasa ile Sheria yetu ya Kondominia ianze kufanya kazi, kwa sababu ile itawezesha kuharakisha matengenezo ya nyumba zile, kwa sababu kuna baadhi ya nyumba katika nyumba zile zimeshamilikiwa na watu binafsi. Sasa ukichukua fedha ya serikali na kwenda kutengeneza nyumba ya mtu binfasi utakuja kuhojiwa tena hapa kwenye hili Baraza la Wawakilishi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tulichoweza kukihami sisi kama juu paa linaharibika na hiyo tunaweza kusaidia, kwa sababu ni jukumu letu kuwasaidia wananchi wetu katika kuhakikisha kwamba dari zile za juu tunaweza kuzifanyia matengenezo.

Nadhani suala hili litakuwa zuri na jepesi zaidi tutakapokuwa na Sheria yetu ile ya Kondominia, inawezesha kufanya matengenezo katika maeneo mbali mbali na sheria hiyo ilipitishwa hapa na Baraza la Wawakilishi na wale watakuwa wanaachia kupitia kwenye kondominia yao pamoja na kamati yao itakuwa inafanya kazi pale, na matengenezo yatakuwa yanakwenda vizuri na serikali itakuwa inaratibu na huo ndio utaratibu mzuri na kuliko kusema tunakwenda kutengeneza nyumba yote, wakati nyumba tayari mtu ameshamiliki.

Kwa hivyo, watu wanaweza kusema kwamba wameula pale nyumba wamenunua ni yao wenyewe na halafu wanatengenezewa na tutakuja kuulizwa maswali hapa hapa. Mhe. Mwenyekiti, nakubali suala hilo na ndio maana ya kupitisha ile Sheria ya Kondominia kwa sababu hiyo.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana labda niulize swali la nyongeza. Kwani nyumba hizi zimeshauzwa zote hamna za serikali? Mhe. Mwenyekiti, naomba jawabu katika hilo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, nyumba Mhe. Asha Bakari Makame ameuliza hapa kwamba ngapi zimeuzwa na ngapi zimebakia, nilieleza kwamba zile nyumba zinahitaji kufanyiwa kazi kwa karibu sana, kwa sababu kuna nyumba zimeuzwa hasa kihalali na serikali katika nyumba zile. *(Makofi)*

Vile vile kuna nyumba alipewa mtu pale ee bwana kaa hapa akatokea mmoja mwenye fedha zake akamwambia nitakupa kilemba, akatoa kilemba na kuichukua ile nyumba. Mhe. Mwenyekiti, kuna pia aliekwa mtu mfanyakazi na alikaa pale, baadaye akaondoka akamuweka mwanawe, akamuweka mjukuu. *(Makofi)*

Sasa bado zipo nyumba pale bado ni mali ya serikali, lakini zipo nyumba pale si mali ya serikali ambazo zimeuzwa kihalali, kuna nyumba amelipwa mtu fidia ya nyumba yake na huyu akiuza ameuza nyumba yake na zimo mule ndani. Kwa hivyo, ndipo pale niliposema kama nilivyomjibu Mhe. Asha Bakari Makame, kwamba linataka kufanyiwa kazi kwa ukaribu zaidi, na hii kazi tumeichukua kwa ajili ya kuifanya. *(Makofi)*

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee na huku tukisubiri taarifa kutoka kwa Mhe. Asha Bakari Makame pamoja na mambo mengine. Ahsante.

Kifungu 1101 –Idara ya Nyumba na Makaazi Sh. 239, 000,000/=
Kifungu 1102 – Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba Sh.30,000,000/=
Kifungu 1201 –Mahakama ya Ardhi

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. Wakati nilipokuwa nikichangia katika Mahakama hii ya Ardhi niliulizia kuhusu malipo ya wale *Assessors* ambao wanashirikiana. Vile vile niliulizia kuhusu Mahakama ya pale Gamba, ambayo ingeweza kusaidia migogoro katika Wilaya, ni lini itafunguliwa ili tuweze kuitumia?

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, naomba lile la mwanzo arejee kwa sababu ya lile zogo pale sikulisikia lile la mwanzo na lile la pili nimelisikia.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, nakuomba urudie lile swali la mwanzo.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, swali la mwanzo kuna *Assessors* katika Mahakama ya Ardhi, malipo yao inaweza kutimia miezi miwili mpaka mitatu hawajapata. Kwa hivyo, nataka kujua ni lini watapatiwa au kuna mkataba maalum ambao watawekewa, ili waweze kujua malipo yao wanayapata vipi? *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru naomba nimjibu Mhe. Mjumbe kwamba katika Wizara ya Katiba na Sheria kuna kifungu cha *Assessors*, ambapo kwa kweli kuna deni kubwa la *Assessors* na wala sio kwa Mahakama ya Ardhi tu, isipokuwa ni kwa Mahakama zote. Kwa hivyo, tayari tumeshaomba fedha na tumeshazipa na ikimaliza bajeti fedha zao watalipwa. *(Makofi)*

Vile vile kuhusu hii Mahakama ya Gamba, kama nilivyosema mwanzo iko katika hatua za mwisho kurekebishwa, kwa sababu ile nyumba tuliyoipata ni mfano wa nyumba, unajua Mahakama kuna utaratibu wake wa ujenzi. Kwa hivyo, hivi sasa tunakamilisha ule utaratibu wa ujenzi wa Mahakama na tukikamilisha hayo, basi Mahakama ya Ardhi ya Gamba itaanza na wala haitachukua muda mkubwa.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. Nashukuru kwa kupata majibu yenye kutia matumaini tuendelee. *(Makofi)*

Kifungu 1201	–	Mahakama ya Ardhi	Sh. 194,000,000/=
Kifungu 1301	–	Idara ya Uendeshaji na Utumishi	

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, ahsante na nimefurahi kupewa muda peke yangu, nadhani nitapata muda wa kutosha kujenga hoja yangu.

Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu nilizungumzia suala ambalo limekuwa ni mbio za sakafuni, lakini hizi hazina ukingo. Suala zima la Azimio la Baraza hili lililoitishwa mwezi wa Aprili mwaka 2009 la kuliondoa suala la mafuta na gesi asilia katika mambo ya Muungano. Vile vile katika mchango wangu nilisema wazi kwamba natambua kwamba mamlaka ya kuliondoa hili rasmi yako katika Bunge la Jamhuri ya Muungano kwa mujibu wa Katiba tuliyonayo sasa.
Lakini Mhe. Mwenyekiti, nilisema limechukua muda mrefu sana, pia nilisema uungwana, heshima, hekima, ustaarabu, busara za Wazanzibari zinatafsirika vibaya Mhe. Mwenyekiti, ndio maana hakujachukuliwa hatua mpaka hivi sasa.

Kwa hivyo, nilitoa pendekezo hapa na nilisema katika hili sitapitisha fungu hili ikiwa Mhe. Waziri hakuniambia lini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

itasimamia sasa azimio lile. Mhe. Mwenyekiti, mwaka jana wewe shahidi tulilileta hapa na tulibishana sana, tulimpatisha dhiki si ndogo Mhe. Waziri wa wakati ule Mhe. Ali Juma Shamuhuna, lakini hatimaye serikali ikatuambia tuiachie itakwenda kulifanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, nakumbuka aliyetoa *commitment* ya mwisho baada ya kuomba muda alikuwa Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwamba tuwape mwaka mmoja, katika mchango wangu Mhe. Mwenyekiti nimesema mwaka mmoja umemalizika.

Vile vile katika Kikao cha Mashauriano, ambacho Makamo wa Pili aliongoza Mawaziri kwa upande wa Zanzibar, wamekwenda na wakasema wapewe muda kule na walipewa miezi minne, umemalizika mwezi wa Mei hakuna hatua Mhe. Mwenyekiti.

Sasa nikasema Mhe. Mwenyekiti, wakati umefika serikali sasa itekeleze upande wake wa Zanzibar kwa kuleta sheria ambayo rasimu yake ya mswada iko tayari, Sheria ya Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta Zanzibar na Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Kusimamia Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta Zanzibar (*Zanzibar Petroleum Development Authority*).

Mhe. Mwenyekiti, nimemsikiliza Mhe. Waziri katika majibu yake, alichoniambia kwamba yeye ameapa kwa Katiba mbili na akazionesha. Lakini alisema kuna fununu kwamba suala hili litapelekwa katika kikao cha Baraza la Mawaziri la Jamhuri ya Muungano.

Mhe. Mwenyekiti, mimi bado nina wasi wasi na majibu haya na ndio maana nimesema nafurahi kwamba katika hili nimekuwa peke yangu Mhe. Mwenyekiti, ili nipate kutoa maelezo.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili ni muhimu sana kwa wananchi wa Zanzibar, na mimi naamini wakati tunazungumza wananchi wa Zanzibar wote walikuwa wanasubiri hatima ya suala hili katika bajeti hii.

Mhe. Mwenyekiti, ukinipa hoja kwamba kwa sababu tumeapa kwa Katiba mbili na mafuta na gesi asilia imetajwa humu katika nyongeza ya kwanza, kwa hivyo tusiende tuchukue hatua ya kuleta sheria hii hapa, Mhe. Mwenyekiti mimi nitakuwa siifahamu Serikali yangu ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwani naipenda sana.

Kwa kweli katika orodha hii Mhe. Mwenyekiti, ulinzi na usalama ni suala la Muungano, lakini Zanzibar ina Idara Maalum na Katiba yetu ya Zanzibar inazitambua hizo. Katika Katiba hii Mhe. Mwenyekiti, biashara nchi za nje ni

suala la Muungano, lakini tunaziendesha wenyewe Zanzibar na Baraza hili tunapitisha Sheria ya *ZSTC* na kuipa mamlaka ya kufanya biashara nchi za nje.

Mhe. Mwenyekiti, katika Katiba hii usafiri na usafirishaji wa anga ni suala la Muungano, lakini tumepitisha Sheria hapa ya Kuunda Mamlaka ya Viwanja vya Ndege na masuala mengine.

Mhe. Mwenyekiti, katika Katiba hii utafiti, takwimu yote ni masuala ya Muungano, lakini tumepitisha sheria mbali mbali zinazozitambua taasisi zetu ambazo zinasimamia na hata bandari ni suala la Muungano, lakini tumeunda Shirika la Bandari hapa na tumeweka sheria. Sasa nakumbuka hekima ya serikali ya mwaka jana, namalizia Mhe. Mwenyekiti na wala sitaki kuchukua muda wako.

Kwa kweli nakumbuka mwaka jana Mhe. Mwenyekiti na Mhe. Mwanasheria Mkuu alitupa hekima yake na mwaka jana tukaikubali hapa, kwamba hili kwa maumbile yake lilivyo ndio maana likatolewa Azimio katika Baraza, kwa sababu hizo kampuni zinazotaka kuchimba hazitakuja zile zinazoheshimika na wala sio zile zinazojipitisha, kwani kuna kampuni nyengine zinazojipitisha kwa Mawaziri na kujaribu ku-*lob* na tunazifuatilia kwa makini, lakini kampuni makini hazitakuja. *(Makofi)*

Sasa Mhe. Mwenyekiti, ninachosema mimi nilichotoa hoja katika mchango wangu ni kwamba najua, na ukienda katika *Hansard* nilisema hivyo, kwamba najua sheria tunaweza tukazipitisha hapa na zisiweze kuleta kampuni kuja hapa. Lakini mimi nataka tuchukue hatua hii, ili tupeleke ujumbe kuharakisha suala hili kuondolewa, na hizo hatua alizotuambia Mhe. Waziri kama zinachukuliwa basi ziharakize kuliondoa kwamba sasa Wazanzibari tumeamua.

Mhe. Mwenyekiti, nataka Mhe. Waziri anipe kauli katika hili, kwamba na tumepitisha utaratibu mpya katika Kanuni zetu kuna *first reading, second reading and third reading*.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri katika hili aniambie kwamba ndani ya Kikao cha Oktoba Mhe. Mwenyekiti, tutaletewa sheria hizi mbili kuja kusomewa kwa mara ya kwanza, ili Kikao cha Januari Baraza hili liheshimu na litekeleze maamuzi ya Baraza lako ambalo ulilionguza wewe mwenyewe Aprili, 2009 kuheshimu maamuzi yake. Mhe. Mwenyekiti naomba sana kauli ya Mhe. Waziri. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, mimi bado nina wasi wasi kupitisha sheria hapa na halafu ikawa batili, itakuwa tumejiridhisha mno.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, rudia majibu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, nasema nina wasi wasi kupitisha sheria hapa na halafu ikawa batili. Lakini kwa sababu wenzetu kule wameshatuambia kwamba wanapeleka *Cabinet* ijayo kesho kutwa, mimi naona tusubiri majibu ya *Cabinet* pale, kwa sababu viongozi wetu wa juu wameshasema kwamba suala hilo halina matatizo, kwa hiyo tuwasubiri watafanya uamuzi gani *Inshaallah*. Kwa hivyo, siwezi kumuahidi kwamba nitaleta kwenye Kikao cha Oktoba, isipokuwa itategemea hali.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, namuelewa sana na wala sitaki kumpa tabu Mhe. Waziri. Mhe. Mwenyekiti, mimi Baraza hili nimeingia mwaka 2010 mwezi wa Novemba.

Baraza ulilioliongoza wewe la Saba lililokuwa na viongozi waliolisimamia lile wakiongozwa na Waheshimiwa Mawaziri wetu wapo hapa, wengine waliokuwapo wakati ule, Wajumbe waliobobea akina Mhe. Ali Mzee Ali nimewataja wote waliopitisha maamuzi.

Vile vile katika Jarida ulilonigaia Mhe. Mwenyekiti katika ofisi yako Baraza lile lilisifiwa, kwa sababu ni muhimu sana lilisifiwa katika habari hii, Baraza la Saba la Wawakilishi Lavunjwa, Mhe. Mwenyekiti naomba kunukuu kidogo. “Baraza hilo litakumbukwa kihistoria kuwa ni Baraza lililoweka misingi ya kudumu ya umoja, mshikamano, utulivu na amani ya Zanzibar, limeweza kufanya maamuzi mazito kwa uadilifu na kujijengea heshima kubwa mbele ya jamii.

Pia limesimamia vyema madhumuni na malengo ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Januari 12 mwaka 1964, kulinda uhuru wa Zanzibar na watu wake, kulinda utu, umoja na heshima ya Wazanzibari kujiamulia mambo yao yanayohusu nchi na uchumi kwa jumla”. Hii ni heshima yako Mhe. Mwenyekiti ulipoliongoza Baraza la Saba na mpaka leo unaendelea kuliongoza. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimemuelewa Mhe. Waziri. Sasa ninachotaka, kwa sababu kama nilivyosema kwamba hii *danedane* imeshakuwa kubwa, imekuwa katika Muungano huu namna unavyoendeshwa Mhe. Mwenyekiti Zanzibar kama vile tumekufa dungu msokoni, tulizokula tuziteme na mchezoni hatumo. Sasa tumeshachoka Mhe. Mwenyekiti, nadhani tumecheza

dungu msokoni, unaambiwa uziteme na mchezoni humo utoke. Mhe. Mwenyekiti, Muungano wa namna hii hautusaidii.

Sasa ninachosema lilitoka hili na wakati fulani tulibishana humu ndani na tuliambiwa halipelekwi katika kero za Muungano. Vile vile siku moja. Tulim-*confront* hapa Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, kwamba umetujibia swali hapa na baadaye ukalipeleka kwenye orodha ya kero za Muungano na ushahidi unakwenda kulijadili baadaye, lakini tuliambiwa linajadiliwa na wakubwa wetu, tusipoteze wakati Mhe. Mwenyekiti.

Sasa nilichosema ni kimoja tu, kwamba tunayo ahadi na mimi siamini kwamba tutafika Oktoba kwamba Baraza la Mawaziri la Jamhuri ya Muungano litakuwa halijakutana litakuwa Baraza la Mawaziri la ajabu katika dunia hii.

Lakini Mhe. Mwenyekiti nilitoa hoja yangu na nisamehe Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu hili suala ni kubwa sana, nilitoa hoja yangu wakati nilipokuwa nikichangia, kwamba wakati sisi tunasubirishwa wenzetu wana-*move on* na hii ni biashara Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Kwa mfano, Msumbiji katika ukanda huu wa bahari tunaozungumza Msumbiji wameanza na hivi saa wako mbali, nilisema wenzetu Tanganyika wameshavumbua *trillion* tatu *cubic fit* za gesi na wala mapato hayaji huku Mhe. Mwenyekiti, na tunagaiwa ile *GBS* ya wahisani na fedha za Muungano tusidanganywe haziji hazivuki maji. *(Makofi)*

Lakini Mhe. Mwenyekiti, gazeti la jana Mhe. Rais Kikwete yuko ziarani Uingereza amekwenda kukutana na Kampuni kubwa inayochimba Gesi anawaambia Mhe. Mwenyekiti, kwamba naomba kunukuu kidogo Mhe. Mwenyekiti. "*The government is currently putting up the gas sector instruments including the gas policy, gas master plan and the gas act to prepare for an imminent, vibrate gas sector regime*". *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hawa wenzetu wana-*move* na wanaweka sera, sheria pamoja na utaratibu wa kujenga uwezo na sisi tumekaa tunasubirishwa, *by the time* wakituruhusu hawa hata ukiruhusiwa sasa kwa sababu tunaheshimu maamuzi, lakini wenzetu wameshatutangulia mbele katika huo ushindani wa kibiashara tumekuwa tumeachwa nyuma.

Mhe. Mwenyekiti, nimekutana na mwanafunzi mmoja wa Kizanzibari ambaye anasoma Chuo Kikuu cha Dodoma anasomea *Petroleum Engineering*, ananieleza tayari wameshafuatwa na hizi kampuni, kwamba wakitoka

wachukuliwe wanakwenda kusomesha kwa ajili ya kusaidia na sisi tumekaa tu.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nasema kwamba sitaki tufike pahala nikaliomba Baraza lako lipige kura katika hili sitaki, kwa sababu naheshimu sana wasia muhimu alionipa Mhe. Mwanasheria Mkuu na nimeutumia mara nyingi sana, kwamba katika masuala ya haki za Zanzibar na hatimaye kujivua na dudu hili na mashaka yake ni muhimu sana, serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Baraza la Wawakilishi na wananchi wa Zanzibar waende pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, katika hili ninachotaka kama tuna-*commitment* hii iwe ya mwisho, na wala isiwe tunachezeshwa mchezo wa kitoto. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nakubali kwamba naomba nibadilishe kwa sababu nilimuomba Mhe. Waziri kuwa Kikao cha Oktoba alete *First Reading*, mimi naamini mpaka Oktoba *Cabinet* itakuwa imeshakutana, tuwape nafasi na tuone hiyo hatua na hapo katikati patakuwa na Kikao cha Bunge, na kama watakuwa na nia ya dhati kwenda kuliondoa katika Orodha ya Mambo ya Muungano tutaiona.

Lakini ikiwa Mhe. Mwenyekiti na hapo ndipo itakuwa kauli yangu, ikiwa tumefika Januari Kikao kinachofuata cha Baraza la Wawakilishi baada cha Oktoba, ikiwa tumefika Januari hakuna hatua iliyochukuliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano kuliondoa katika Orodha ya Mambo ya Muungano, Baraza hili na Serikali ya Mapinduzi iwe ya Mapinduzi kweli ya Mzee Karume. Jana Mhe. Mwenyekiti nilisema sisi si watumwa wa Muungano ni wabiya wa Muungano.

Kwa hivyo nasema ikifika mwezi wa Januari kama bado hakujachukuliwa hatua ndani ya Kikao cha Bunge cha Oktoba, basi sisi Januari tuletewe *first reading* ya Miswada hii miwili. Kikao cha Machi tuje tujadili tupitishe hapa, yatakayobakia tutakutana mbele kwa mbele Mheshimiwa. Naomba *commitment* hiyo ya Serikali Mheshimiwa. Kama hiyo sikukubaliwa nitaomba tupige kura la si hivyo nitakubali peke yangu nitundikwe Mhe. Mwenyekiti, nibakie kuwa shahidi kwa kusimamia haki za Zanzibar na Wazanzibari. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Miye Mhe. Mwenyekiti, hayo mawazo anayoyazungumza wala sio mabaya isipokuwa tu hiki kifungu cha tatu ndio kinachonifanya ni *hesitate* katika ukurasa wa 64 ni lazima nizingatie Katiba. Hii Katiba tumeitunga sisi kwa sababu Wabunge wetu wameingia katika kufanya Katiba hii kutoka Zanzibar na tumeapa kwa Katiba hii.

Kwa hivyo anavyosema mimi nategemea sana suala hili halitochukua muda mrefu kwenye Serikali ya Jamuhuri ya Muungano, uamuzi utapatikana tu. Mimi sina wasi wasi mkubwa sana *Inshaallah*. Kwa nini tuingie katika migogoro.

Mhe. Mwenyekiti: Serikali tulifatilie kwa karibu suala hili, ili tusilete migongano wala mivutano.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, katika majibu yake moja katika alipokuwa akimwambia Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) hapa, Mhe. Waziri alisema kwamba "haki haiombwi, hudaiwa" kasema. Jana nilisema na naendelea kusema kwamba kwa njia anazozitaka yeye Mhe. Waziri na Serikali tumeshasubiri, Mheshimiwa hatukuliamua jana hili. Nimeamua mimi suala hili ndani ya Baraza hili *April* mwaka 2009. Au kuwe hakuna nia na kama hakuna nia hatuwezi kusubiri mpaka Kiama wakati wenzetu wana *move on*.

Ninachosema yeye katwambia si kuna *Commitment* ya *Cabinet* na katwambia ni *Cabinet* ya karibuni. Mimi siamini hasa Mheshimiwa, tokea Oktoba nimetoa miezi sita mpaka Januari. Naomba hili anipe *commitment* ya Serikali kama tunatoa muda huo kwa wao kuchukua hatua, hawakuchukua hatua Serikali ita–*move* yenyewe. Wacha kampuni zisije kwa kuona kwamba kuna mgogoro, lakini zitasubiri mpaka hapo tutakapokuwa tuko *active* sisi tutakuwa tumeshapitisha. Kama hakuna *commitment* Mhe. Mwenyekiti nasema tena, mimi leo niko tayari peke yangu nisulubiwe katika Baraza hili ili niwe shahidi mbele ya wananchi wa Zanzibar kwamba nimesimamia haki yao. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Nadhani tuendelee kwa maelekezo kwamba Serikali inafuatilia kwa karibu sana suala hili.

Mhe. Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru kwamba umenipa nafasi hii ya kusema machache juu ya suala hili. Namshukuru sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwa kufatilia maslahi haya ya Wazanzibari.

Nataka niseme tu kwamba tangu suala hili tulipolizungumza na hasa katika kipindi cha 2010, 2011, 2012 ndani ya Baraza hili, Serikali sio kwamba ilikuwa imekaa kimya halifatilii. Ilikuwa tunalifatilia suala hili kwa karibu sana na mimi mwenyewe nilikuwa nalifatilia kwa karibu sana ili kuhakikisha kwamba hili suala linamalizika. Mhe. Mwenyekiti, kila nikenda Dar-es-Salaam au Dodoma nakutana na Waziri Mkuu au nakutana na Makamo wa Rais tunalizungumza hili.

Katika kikao kilichopita cha SMZ na SMT nililizungumza suala hili. Mhe. Makamo wa Rais alikuwa Mwenyekiti wa Kamati hii ya pamoja akasema kwamba apewe miezi mine kulikwamua suala hili ili lende mbele. Sasa miezi mine imepita lakini sasa limekwamuka na mimi nimehakikishiwa kabisa juzi tu kwamba sasa katika Kikao kijacho cha Baraza la Mawaziri sio suala hili peke yake pamoja na masuala mengine yote hayo yatakwenda kwenye Baraza la Mawaziri. Sasa pale ndio tunaanza kwenda mbele.

Kwa sababu suala hili limeshakubaliwa, kimsingi Rais mwenyewe wa Jamuhuri ya Muungano ametoa kauli, juzi Waziri Mkuu ametoa kauli Bungeni kwamba haoni matatizo ya suala hili. Sisi kitu ambacho tutakipigania sasa hivi baada ya suala hili kupelekwa kwenye Baraza la Mawaziri. Kwa sababu sasa hivi kinadharia tumeshakubaliana kwamba suala hili litoke kwenye orodha ya mambo ya Muungano, sasa tupewe ruhusa tuanze kufanya maandalizi sisi wenyewe. (*Makofi*)

Tukishakuelezwa hivyo kwamba sasa hivi Zanzibar kwa sababu suala hili limeshakubaliwa litoke kwenye Muungano Zanzibar sasa iendelee kujiandaa pamoja na kuletwa huo Mswada wa kuunda sheria hizo. Hili suala sisi tunalifatilia na sisi tunauchungu sana wa hii nchi. Tunataka tuimarishe uchumi wetu kwa kutegemea rasimali zetu wenyewe moja wapo ikiwa hii.
Mimi nataka nimuhakikishie sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu, asifikirie kwamba sisi hatuna uchungu na hii nchi. Sote tuna uchungu na hii nchi na kila mmoja anataka kuona maendeleo ya nchi hii yanakwenda mbele kwa maslahi ya wananchi wake. (Makofi)

Kwa hivyo mimi nataka Mhe. Mwenyekiti, nimuhakikishie Mhe. Ismail Jussa Ladhu pamoja na Baraza lako tukufu kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar italifatilia suala hili kwa karibu na kuhakikisha kwamba inawezekana hata kabla ya Januari kwamba suala hili tukapata sasa hivi na sisi muelekeo wa kuunda Sheria zetu na kusimamia uchimbaji na kusimamia uundaji wa chombo ambacho kitasimamia utafiti na uchimbaji mafuta na gesi asilia. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, ni kawaida yetu kufurahi kama hivyo kwa makofi, halafu tukaondoka matupu, jana nililisema hili. Namuheshimu sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwa sababu ni mmoja katika viongozi wetu watatu wa juu wa kitaifa. Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu ya heshima hiyo leo ametoa kauli nzito ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hii imeingia katika *record* za *Hansard*, nataka niseme kitu kimoja na mimi kiingie katika *record* za *Hansard* Mhe. Mwenyekiti.

Mimi ndio niliyesimamia hoja hii leo, naamini katika hili wenzangu wote wataniunga mkono nitawaongoza kuisimamia kauli hii ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais ambayo inaheshimiwa na Baraza hili na wengineo wote. Kwa hivyo naachia kwamba tuendelee kwa kuamini kwamba hatua zilizoahidiwa zitachukuliwa.

Jana nilisema Mhe. Mwenyekiti katika mchango wangu kwamba bahari nzuri Kanuni zetu zina demokrasi nzuri sana Mhe. Mwenyekiti. Naamini tukiwa na Spika, anayeheshimu demokrasi na haki za Wajumbe kama ulivyo wewe Mhe. Mwenyekiti, kwama utaheshimu hili na utaendelea kuziheshimu kanuni hizi. Kwa hivyo natoa nafasi na jana nilisema hata Mhe. Omar Ali Shehe alisema kwamba tukifika Januari hatuoni *movement* yoyote, tukaona hatua ambazo zitapelekea kuwadharaulisha viongozi wetu wanaotoa kauli nzito kama hizi katika Baraza la Wawakilishi, mimi nitatumia haki yangu juu ya kanuni hizi kuletwa Mswada Binafsi.

Nashukuru Serikali imeshanifanyia kazi kwa sababu Rasimu nnayo waliyoiyandaa Serikali wenyewe mwaka 2009. Ikifika Januari kama hatuoni *movement* naamini wajumbe wenzangu wote wanataka kuhukumiwa na Wazanzibari kama ninavyotaka kuhukumiwa mimi. Naamini katika hilo wataniunga mkono. Ninachosema ukifika wakati huo kama sioni mimi nitaongoza wajumbe, wenzangu *back bencher* tulete Mswada naamini mpaka Mawaziri.

Mhe. Makamo wa pili alisema pale kwamba lolote litakaloletwa na *back benchers* kama lina maslahi na Zanzibar wataliunga mkono. Naamini wakati huo watatuunga mkono vile vile. Mhe. Mwenyekiti, naruhusu tuendelee. Lakini kama nilivyosema kwa sababu kuna kauli ya Waziri, naomba kwa heshima ya Baraza hili na kwa heshima ya wananchi ambao wanaliamini Baraza hili na wanaamini wananchi wao waliokuwepo katika Baraza hili. Hii hatua kwa vikao hivi, Kikao cha Oktoba tuje tuletewe angalau *progress* ya hatua zilizochukuliwa zimefikia wapi na tumefikia wapi katika utaratibu huo. Naomba Mhe. Makamo wa Pili hili alichukue na atuletee taarifa baadaye katika Kikao hichi cha mwezi wa Oktoba kwamba tumefikia wapi katika hizo hatua ambazo tunazoambiwa zimechukuliwa. Isiwe kama anavyosema Mhe. Mwenyekiti, mambo ya kuambiwa tutanyonya kesho, kesho tumechoka Mhe. Mwenyekiti. Baada ya hapo nasema tuendelee ahsante sana Mheshimiwa.

Kifungu	Idara ya Uendeshaji na Utumishi	Sh.738,000,000
Kifungu 1401	Msajili wa Ardhi	Sh.153,000,000
Kifungu 1501	Idara ya Mipango Miji Mjini na Vijijini	

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu kuna suala moja nililiacha. Mhe. Mwenyekiti, mimi na wenzangu wengi humu tumekuwa tukilieleza juu ya kutoridhishwa na vifungu na ingelikuwa sina suala zito nililoligusia punde hivi. Hoja hii ningeiibua katika Idara ya Utumishi na Uendeshaji, lakini kwa sababu linahusika kila pahala naweza kulilalamikia popote.

Mhe. Mwenyekiti hata hapa lipo. Katika mchango wangu nilimuomba Waziri akija kwa jumla aje atupe ufafanuzi kuhusu vifungu mbali mbali hivi ambavyo vinaendelea kujirejea katika kila Wizara juu ya matumizi ya safari, posho maalum, viburudishaji, mafuta na vilainisho, haya yanaendelea kupanda katika Wizara.

Mhe. Mwenyekiti, ile *proportion* ya kupanda wala hailingani, maana ingekuwa ni kupanda kutokana na mfumko wa bei kwa mfano mafuta ukitegemea kila pahala pawe na uwiano, lakini haupo uwiano katika Serikali. Katika Idara hii naomba nilizungumze na nieleweke hoja yangu katika pahala pamoja tu nitaeleweka.

Katika Idara ya Mipango Miji, ukiangalia *vote* 211100 Mishahara ya fedha taslim. Kwenye posho za vikao na Kamati mwaka jana ilikuwa milioni moja laki nne (1,400,000) mwaka huu inaukua thalathini na tisa milioni na laki tisa (39,900,000). Hapo kwenye Malipo baada ya saa za kazi, mwaka jana ilikuwa milioni mbili laki sita (2,600,000) mwaka huu ishirini na tatu milioni laki tatu sitini elfu (23,360,000). Mheshimiwa Mwenyekiti ongezeko hili halina uwiano kabisa.

Mhe. Hamza Hassan Juma, juzi alivyokuwa akichangia alisema hii sio mara dufu wala sio mara trufu na mimi nafikiri wala sio mara brufu wala sio zrufu maana yake hazina hata kiwango. Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naomba kwa kutumia fungu hili Mhe. Waziri hebu atujibu hoja yetu ya jumla. Kwa nini kunakuwa na mafungu haya maalum, posho za safari, posho ya vikao na kamati, kwa nini yanakuwa yananona na kunakuwa na uwiano usiokuwa na maelezo, katika kuongezwa huko.

Mimi naamini kama vikao vinafanywa kila Idara na kila mwaka. Sasa haiwezekani kama vikao vya mwaka huu vimeongezeka kiasi ambacho vya mwaka jana vilikuwa vina milioni moja laki nne (1,400,000) vya mwaka huu viwe na milioni 39, siamini Mhe. Mwenyekiti. Mimi naamini hapa ndio ile kwamba umepewa *ceiling,* pesa huna vya kuifanya jalizia huko, kwa sababu huko huhojiwi unaweza kutumia unavyotaka. Naomba maelezo katika hili, Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti naweza kutoa ufafanuzi mdogo tu juu ya masuala haya. Kwanza nataja suala la posho maalum ambalo lilikuwa ziro hapo limekwenda mpaka milioni 12. Ukenda katika Idara nyengine utakuta hivyo hivyo. Sababu kubwa ni kwamba tusisahau kwamba mishahara imenyanyuliwa juzi, baada ya kunyanyuliwa na posho linakwenda kwa mujibu wa mshahara wako.

Isitoshe tumeweka posho kwa ajili ya masekretari wa viongozi na madereva, vile vile wanalipwa maposho. Kwa hio bila shaka hutobakia tena kwenye ziro kwa sababu hizi posho sasa hivi zimekuwa *obligation* wameshazichukua lazima uweze kuzitekeleza.

Kwa upande wa posho la vikao na kamati. Mhe. Mwenyekiti katika idara yangu miye hasa hii ya mipango miji najua kwamba ina mikutano mingi katika masuala ya kupanga, kutathmini na mambo mengineyo. Mengine sijui, lakini hawa wanajua kwamba mipango miji ni jambo jipya ambalo linahitaji mikutano ya wadau. Hutoweza tu kuamua kufanya mpango wa mji ukasema utakwenda kutekeleza tu pale pale, wakati huo umeshapitwa na wakati. Ni lazima uwatafute wadau wa sehemu ile, uzungumze nao, uwafahamishe, wakubali, bila shaka ni lazima uwapatie posho ya namna yoyote. Ndio maana hii posho utakuta hapa imepanda.

Mhe. Mwenyekiti, kazi hiyo tunatakiwa kuifanya sasa hivi katika suala la Mipango Miji, kesho kutwa nakwenda Nungwi au tunakwenda Pemba kule na katika mikutano wadau lazima wawepo. Wadau wanakuwa sio wa pale pale tu lakini hata na wadau wengine wenye maarifa juu ya suala hili la kupanga miji, hutomlipa sh. 5,000/- yule ndio maana hii imenyanyuka kusema kweli. Mimi kwangu najua kuna matatizo ya muengezeko wa mshahara pamoja na posho, kama vile ilivyopanda NSSF nayo imepanda kwa sababu nako vile vile 10% imeongezeka ya mshahara. Maana mshahara umepanda kwahivyo 10% itakuwa kubwa kidogo. Haya ni maeneo ambayo najua yameongezeka katika kiwango hicho kwa hii wizara yangu.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwa ile lugha yetu tunasema kwa heshima zote naomba kutokukubaliana na Mhe. Waziri. Mimi hili nawaombe tena Mawaziri kama nilivyoomba kwa kila Waziri, wasikubali maelezo ya jumla jumla wanayopewa na watendaji wao, Mhe. Mwenyekiti. Kwa kuthibitisha hoja yangu nitampa mfano anielewe hapo.

Nawaomba tena Mawaziri sana hivi fedha za wananchi, masikini. Juzi Mhe. Omar Yussuf Mzee anatuletea hapa namna gani kuongeza elfu hapa, hamsini kule, kuwatafutia madeksi, kuwatafutia madawa naomba hili lifahamike Mheshimiwa. Haya maelezo wanayopewa na watendaji wao Mhe.

Mwenyekiti, hayana ukweli. Ili nifahamike Mhe. Mwenyekiti naomba nitoe mfano tu bado hoja yangu iko huku huku.
Namuomba Mhe. Waziri hebu aangalie ukurasa wa 408 na 409 buku hili, aone hiyo hoja aliyowekewa na watendaji wake kiasi gani ilivyokuwa inaanguka haina mashiko.

Mhe. Mwenyekiti, hii ni Idara ya Uendeshaji na Utumishi, litazame fungu la Mishahara mwaka jana ilikuwa mia mbili ishirini na tatu milioni, laki tatu sabini na nane elfu (223,378,000). Fungu la mishahara mwaka huu la Idara hiyo ni mia mbili sitini na sita milioni (266,000,000). Hebu aitizame hiyo *proportion* ya ongezeko la mshahara hapo halafu alinganishe na katika kifungu hicho hicho ambacho kipo katika ukurasa wa pili yake hapo 409. Ongezeko la posho maalum aitizame uwiano wake imetoka hamsini na tano milioni laki tisa thamanini na nane elfu (988,000) mwaka jana. Mwaka huu ni mia moja arubaini na saba milioni laki tano (147,500,000), nafikiri hoja yangu imeeleweka.

Mishahara imeongezeka kwa milioni labda 33 nafikiri, lakini posho maalum limeongezeka hapo kutoka hamsini na tano milioni mpaka 147, takriban 90 milioni. Mhe. Mwenyekiti, kama posho maalum linakwenda na uwiano wa kuongezeka kwa mishahara kwamba *automatic* linapanda. Mimi siamini kwamba posho limepanda kiasi hichi kwamba liathiri kiasi hichi.

Naomba maelezo Mhe. Mwenyekiti kwa sababu vyenginevyo tunaweza kufika mwisho katika kupitisha Wizara ya Fedha hapa tuje tutake kukata mafungu yote. Kwa sababu mwisho yote yanategemea kule mwisho, hebu tupe maelezo yakuwa kwa nini yanapingana pingana na yanakuwa tofauti tofauti. Naomba sana Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, naomba kidogo kuweka sawa hoja ya msingi ambayo Mhe. Ismail Jussa na pengine na Waheshimiwa wengine wanataka kuielewa. Tulipopandisha mishahara mwezi wa Oktoba mwaka jana, tulikuwa tuna utaratibu viongozi wote walioteuliwa na Mhe. Rais, kuanzia Waziri, Katibu Mkuu, Makamishna, Makatibu, watendaji pamoja na Wakurugenzi, Naibu Wakurugenzi na Manaibu Makamishna, tulikuwa tunawapa posho ya mafuta kwa ajili ya kukimu gari ambazo wamekabidhiwa.

Wakati ule tunawapa posho ya mafuta ambayo iko pamoja na mishahara, Serikali baada ya kupandisha mishahara iliona kwamba tukiunganisha na posho ya mafuta inaweza ikawa ni gharama kubwa sana tukaja tukalipa katika lile eneo la kiinua mgongo. Ile kasma ambayo alikuwa ameipata mwaka jana kabla ya kupandisha mshahara tukaiwacha kama ilivyo lakini tukasema

kwamba mafuta kwa sababu tu haya yanatolewa kwa ajili ya dhamana uliyonayo, mafuta tumeyaondoa. Mafuta sasa utayakuta yapo katika posho maalum kwa wale wateuliwa.

Kwa hivyo pale kwenye mshahara umebakia mshahara pamoja na zile posho ndogo ndogo kwa mfano posho la nyumba, lakini posho ya mafuta tumeiondoa. Kila Mkurugenzi kama ana Naibu Mkurugenzi ile posho ya mafuta iko chini ya posho maalum na kwa upande wa Idara ya Utawala pale anaingia pamoja na Waziri pamoja na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu. Kwa hivyo hii posho maalum hata ukiitaka kwa Mkurugenzi mmoja mmoja kwa kila Idara mafuta wanayoyapata ukizidisha mara 12 utakuta ndio kima hichi kilichopo hapa.

Nilikuwa nataka niwatoe wasi wasi kwa waheshimiwa wajumbe kwamba hii imekuwa imenona kwa sababu tumeiondoa kule ilikokuwepo tumeiweka *separate*. Sasa hivi kwa sababu yule Mkurugenzi au Katibu Mkuu au Waziri atakapokuwa anaondoshwa katika nafasi yake basi isiwe ile *package* pamoja na mshahara anakwenda nayo. Sasa hivi atabakiwa na ule mshahara ambao atakwenda nao lakini mafuta atapewa yule mpya ambaye anakuja kwa dhamana ile. Ndio maana tumeiondoa lakini vile vile tumehofia kile kiinua mgongo kinaweza kikawa ni kikubwa mno kwa sababu tumefanya makisio mtu ambaye kiinua mgongo chake angeweza kupata milioni 120. Baada ya kuongeza hii posho ya mafuta ukiweka pamoja baada ya kuongeza mshahara mpya ingeweza kufika hata 170 milioni. Hilo la kwanza.

La pili hili posho ambalo amelizungumza Mhe. Ismail Jussa, poso la vikao vya Kamati. Hapa Waheshimiwa Wawakilishi nataka niseme Mhe. Mwenyekiti ni kwamba muhimu sio ukubwa wa posho au udogo wa posho, muhimu ni *activities*. Mimi ningependa zaidi Mhe. Waziri akaeleza katika posho hili la vikao na kamati kuna *activities* gani. Lakini kwa Idara hii Mhe. Waziri ameifafanua sana, hawa wanaweza wakafanya mkakati wa kwenda kuangalia mpango wa Mji wa Nungwi. Huwezi ukatoa watu wa mjini ukapata maoni yao Nungwi ni lazima uwakushanye watu wa Nungwi wakupe maoni yao. Kwa hivyo posho lao linatoka katika eneo hili. Ndio kwa maana utaona hili eneo nalo vile vile limebadilika katika hii *program* ambayo tunakwenda nayo sasa hivi.

Waheshimiwa Wawakilishi nataka wakumbuke kwamba nilieleza katika hotuba yangu ya bajeti kwamba sasa hivi tunakwenda katika *project base activities* kwa maana kwamba kila *activities* itakuwa na bajeti yake. Sivyo vile ambavyo tulivyokuwa tunazoea, najua huu ni utaratibu mpya. Vile vile nimeshaiomba ofisi yangu kwamba tuje tuwaandalie Waheshimiwa Wawakilishi, semina tuwaelezee *in details* hasa, waweze kuona.

Katika *program* hii vile vile utaona safari hii mwanzo ilikuwa Mkurugenzi wa Utumishi ndio anayelipia kila kitu. Safari hii unaposafiri utakuta tiket inatoka katika kifungu chengine *per diem* yako inatoka katika kifungu chengine. Haya ndio Mhe. Mwenyekiti ningeomba *at least* Mhe. Ismail Jussa pamoja na Waheshimiwa wengine waweze kuyafahamu kwa upande huo. Ahsante Mwenyekiti.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa kunisaidia lile suala ambalo nimelitolea mfano tu ili kujibu hoja ya Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitaki hapo kwa sababu najua hata tukibishana kiasi gani hatuna jibu hapo. Mimi bado naendelea kumsisitiza Mheshimiwa Kaka yangu na hili namtupia yeye kwa sababu mwisho tunayemtupia mzigo wa kututafutia fedha ili mipango yetu iende, huduma za wananchi ziende ni yeye. Tunachokililia Mhe. Mwenyekiti, hapa ni kwamba *in put* iowane na *out put* isiwe tunaidhinisha fedha katika Mawizara na Maidara lakini huduma wananchi hawazioni. Ndio maana unakuta mafungu makubwa lakini hayahudumii huduma, ni posho za vikao, *over time*, safari, vilainisho, mafuta, zawadi.

Mhe. Mwenyekiti, jana kulikuwa kuna fungu moja, unajua mara nyengine kwa sababu ya Kanuni zetu huruhusiwi kusimama wakishakusimama watu watatu na mimi ni mtu wa kuheshimu Kanuni zako, unajua Mhe. Mwenyekiti. Kulikuwa kuna fungu linapitishwa hapa nafikiri juzi, ilikuwa ni vichekesho vitupu ningelinyanyukia miye. Kwa sababu ilikuwa fungu linaonesha kwamba zile gharama za safari ilikuwa kama laki tano (500,000) lakini eti gharama za *air port charges* milioni kumi na zaidi. Lipo fungu nitakuja kumuonesha Mhe. Omar Yussuf. Hili buku Mhe. Mwenyekiti, lina madudu mengi.

Mhe. Mwenyekiti, bado namwambia Mhe. Omar Yussuf Mzee, walitazame sana hili, nimwite kwa cheo chake Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi, Mipango na Maendeleo, nimuombe sana. Kwa sasa nakubali tuendelee kwa sababu moja tu, naamini baadae tutakuwa na kazi ya ziada mwaka huu. Siamini kama Kamati zote tuko sawa sawa katika kufanya *scrutiny* hii tunayoifanya hapa. Naamini kuna Kamati *over all* ambayo ni PAC na leo naiona hekma. Siku ile tulivyokuwa tukibadilisha kanuni tuliposimamia kwa dhati kwamba ile Kanuni ya kuipa mamlaka PAC isichunguze tu hesabu za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali lakini maagizo mengine yoyote itakayopewa na Baraza na leo naiona hekma yake.

Naomba Mhe. Mwenyekiti, Waziri akatizame, Kamati tutizame, tutake maelezo, wanachi wetu wamechoka. Wananchi wamefarijika mno kuona kwamba sasa tunahoji vitu ambavyo vilikuwa havihojiwi humu. Tunataka tusimamie fedha za walipa kodi ambazo zinatoka kwa wavuja jasho, masikini za Mungu. Nasema tuendelee kwa sasa hivi kwani hata tukibishana mpaka asubuhi sipati maelezo hapa. Nasema Kamati itafanya kazi yake ili tupate maelezo. Hiyo semina aliyotwambia Mhe. Waziri tutaisubiri tuone, turidhike kama kweli. Semina hiyo itatuyakinisha na kutushibisha kwamba unaweza ukawa na fungu kwamba laki tano la safari (500,000) lakini milioni kumi na tano (15,000,000) za *air port charge* nafikiri itakapokuja hiyo semina itatusaidia. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti: PAC na Kamati inayohusika itafatilia kwa karibu matumizi haya.

Kifungu 1501 Idara ya Mipango Miji Mjini na Vijijini Sh. 293,000,000
Jumla ya Fungu Sh.**6,708,000,000**

(Vijifungu vilitajwa hapo juu vimepitisha na
Kamati ya Matumizi bila ya mabadili yoyote)

FUNGU 25 – WIZARA YA ARDHI, MAKAZI MAJI NA NISHATI

Kifungu 0401 Idara ya Mipango Sera na Utafiti	Sh.63,694,328,000
Kifungu 0501 Idara ya Ujenzi	Sh.100,000,000
Kifungu 0801 Idara ya Nishati	Sh.200,000,000
Kifungu 1001 Idara ya Upimaji ya Ramani	Sh.9,380,400,000
Jumla ya Fungu	Sh.**73,374,728,000**

Baraza lilirudia

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha ya Wizara yangu bila ya Mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako liyakubali makadirio hayo.

(Hoja ilitolewa na iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe mimi nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kufatilia fedha za wananchi hatua kwa hatua kwa umakini mkubwa. Ni haki yenu kufanya hivyo na kwa kweli hiyo ni kwa manufaa ya wananchi.

Lakini pia nawashukuru na Waheshimiwa Mawaziri wote pamoja na Waziri huyu aliyemaliza kazi yake hivi sasa. Kwa kuwa mtulivu, kujitahidi, kujibu na hiyo ndiyo wajibu wa Mawaziri wote. Kazi hii kwa upande wa Mawaziri ni kazi ya pamoja kama tulivyoona kwamba kumekuwa na msaada kutoka hapa na pale na Serikali pia. Hivi ndivyo tutakavyofanya shughuli zetu kwa ufanisi mkubwa na kwa manufaa ya wananchi. Nakushukuru sana.

Waheshimiwa wajumbe baada ya kazi hiyo nzuri mliyoifanya sasa naakhirisha kikao hichi hadi siku ya Jumatatu tarehe 16/07/2012, saa 3:00 za asubuhi.

(Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 16/07/2012
saa 3:00 Asubuhi)